**9 NOVEMBA, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Tisa – Tarehe 9 Novemba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## KIAPO CHA UAMINIFU

**SPIKA:** Kiapo cha Uaminifu.

1. Mhe. Aziza Sleyum Ally.

*(Mbunge aliyetajwa hapo juu Aliapa Kiapo cha Uaminifu)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali.

Tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 126

### Kumaliza mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Handeni na Kilindi

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka kati ya Handeni na Kilindi katika eneo la Bondo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mbunge wa Jimbo la Handeni Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwisha tatua mgogoro wa mpaka kati ya Halmashauri ya Mji wa Handeni na Kilindi katika eneo la Bondo kwa maelekezo yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga kwenye kikao cha tarehe 25 Julai, 2023.

Mheshimiwa Spika, timu ya wataalam wa ardhi, Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama wa Wilaya na viongozi ngazi ya Tarafa,

Kata na Vijiji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi na Handeni walikutana tarehe 8 – 9 Oktoba, 2021 kwa ajili ya kupitia Tangazo la Serikali *(GN),* kuhakiki idadi ya watu, kuhakiki upatikanaji wa huduma za kijamii pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam ambapo taarifa hiyo iliwasilishwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Wakurugenzi wa halmashauri ya Kilindi na Handeni wameelekezwa kutekeleza masuala yafuatayo; kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi wa misitu, kuheshimu mpaka ulioainishwa kutokana na tafsiri sahihi ya matangazo ya Serikali, kurekebisha usajili wa shule za Msingi Bondo na Parakwiyo ili zisomeke ndani ya Wilaya husika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kupata maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, mara baada ya mgogoro huo kutatuliwa, Shule ya Msingi Bondo iliyokuwa Handeni Mjini tumeikabidhi Kilindi, na Shule ya Msingi Parakwiyo iliyokuwa Kilindi imekabidhiwa Handeni Mjini. Swali langu ni kwamba, ni lini sasa Sereikali itaweka utaratibu wa walimu wa shule hizi mbili kuhamishiwa kwenye halmashauri husika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na mimi mara baada ya Bunge hili kwenda Kata ya Kwamagome kwenye eneo linaloitwa Kwaubaka ambako sasa baada ya kuikabidhi Shule ya Msingi Bondo kwenda Kilindi, tumeanza jitihada za kujenga shule nyingine ili akajionee jitihada za wananchi na waone namna gani Serikali watatusaidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kwagilwa, kama ifuatavyo; kwanza, niwapongeza Wananchi wa

Halmashauti ya Handeni pamoja na Kilindi kwa kutatua mgogoro huu na nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kusimamia suala hilo kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nimuhakikishie tu kwamba tumeshatoa maelekezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, kuhakikisha ifikapo tarehe 30 Desemba mwaka huu Watumishi wote wa shule ya Bondo na Parakwiyo wawe wamepewa barua zao za uhamisho kulingana na eneo ambalo wanatakiwa kuwa katika halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili, niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kuona juhudi za wananchi na kuona namna gani Serikali itawaunga mkono. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mgogoro kati ya mpaka wa Mkoa wa Singida na Mkoa wa Tabora kwenye Wilaya za Uyui na Sikonge upo tangu mwaka 2002 na mwaka 2009 wataalamu walikubaliana kuchora upya huo mpaka. Sasa je, ni lini Serikali itaweka hizo *beacons* kutenganisha hii mipaka ya Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Singida ili kuondoa hiyo migogoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Natumia fursa hii kuwaelekeza Wakuu wa Mikoa ya Tabora na Singida kuhakikisha wanatekeleza maelekezo ya Serikali ya kutatua migogoro ya mipaka kati ya wilaya na wilaya, lakini kati ya mkoa na mkoa ili wananchi waweze kufanya kazi kwa utulivu na amani.

Mheshimiwa Spika, tutafuatilia hilo kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa hii miwili, nakuhakikishia kwamba Ofisi ya Rais TAMISEMI,

itahakikisha *beacons* hizo zinawekwa na kuhakikisha kwamba wananchi wanatambua mipaka yao na kufanya kazi zao kwa amani. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa nimekuona lakini hukusimama saa ya mwanzo kwa hiyo nadhani hilo nimeshaliekeza mara kadhaa. Waheshimiwa Wabunge, kama unataka swali la nyongeza, anaposimama mwenye swali unasimama na wewe ili uonwe. La sivyo nakuwa nimeshataja swali lingine.

Mheshimiwa Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hii fursa. Tatizo la mpaka lipo kule kwetu kati ya Wilaya ya Arumeru Mashariki, Hai na Siha, eneo lile linasemekana ziko *GN* kama tatu. Je, Serikali inasemaje kuhusu mpaka halisi wa Arumeru Mashariki, Siha na Hai?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Utaratibu wa mipaka unaainishwa kwa mujibu wa *GN* zinazotambullika rasmi na Serikali. Kiutaratibu *GN* ya mwisho ndiyo *GN* ambayo inatambulika, *GN* ambayo imepitishwa kwa mara ya mwisho ndiyo *GN* ambayo ina-*sound* kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue jambo hili la Mheshimiwa Pallangyo ili tuweze kuongea na Mkuu wa Mkoa wa Arusha lakini na Kilimanjaro ili waweze kuona namna nzuri ya kwenda na wataalamu kusoma *GN* uwandani, kutafsiri mipaka ya Wilaya ya Hai, Siha Pamoja na Arumeru Mashariki ili wananchi watambue mipaka hiyo lakini pia waweze kufanya shughuli zao kwa amani zaidi, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaenda swali la 128 kwanza ili Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kumaliza halafu tutarejea la 127.

Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 128

**Upungufu wa watumishi Vituo vya Afya Karatu Mjini na Kaloleni – Arusha**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza changamoto ya upungufu wa Watumishi wa Kada ya Afya katika Vituo ya Afya Karatu Mjini na Kaloleni – Arusha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023 Serikali imeajiri na kuwapangia vituo watumishi 83 wa kada mbalimbali za afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, na watumishi 79 katika Halmashauri ya Jiji la Arusha. Aidha, watumishi 14 walipangwa katika kituo cha afya Karatu Mjini na watumishi 18 katika kituo cha afya Kaloleni Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuajiri wataalam wa kada mbalimbali za Afya na kuwapanga katika vituo vyenye upungufu mkubwa kote nchini, zikiwemo halmashauri za Karatu na Jiji la Arusha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba sasa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Hospitali hii ya Kaloleni inahudumia wananchi wengi wa Jiji la Arusha lakini Kituo hiki cha Afya kina watumishi saba ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu sana kwa mkataba.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuwapa watumishi hawa ajira ya kudumu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa mtaani kuna wahitimu wengi wa kada hii wamekuwa wakisubiri ajira Serikalini na binafsi, je, Serikali haioni umuhimu wa kuwatumia wahitimu hawa wa hii Kada ya Afya wafanye kazi kwa kujitolea kwa sababu tuna upungufu mwingi katika sekta hii baadaye waje wapewe ajira rasmi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Catherine Magige, kama ifuatavyo:-

Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia huduma za afya kwa wananchi wa Mkoa wa Arusha. Namuhakikishia tu kwamba tunatambua kwamba Kituo cha Afya cha Kaloleni kinahudumia wananchi wengi lakini pia kina watumishi wanaojitolea ambao wapo pale kwa mkataba na Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia tu kwamba Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kutoa kipaumbele cha ajira kwa watumishi ambao wanajitolea. Tutahakikisha pia watumishi hawa kama vigezo vyao kwa maana ya umri tangu wamehitimu vyuo uko ndani ya kipindi ambacho tunaajiri, basi tutahakikisha kwamba tunawapa kipaumbele ili waweze kupata ajira za kudumu.

Mheshimiwa Spika, pili, tayari Serikali ishatoa Mwongozo wa wahitimu wote wa kada mbalimbali za afya kuomba kujitolea kwenye vituo vyetu vya huduma za afya na Wakurugenzi ambao wana mapato wanaoweza kuwalipa, wawaajiri kwa mikataba waendelee kutoa huduma wakati wanasubiri ajira za kudumu. Jambo hili, namuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kulisimamia kuhakikisha kwamba wataalamu hao wanajitolea katika maeneo hayo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Njalu Silanga, swali la nyongeza.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tatizo lililoko Karatu linafanana kabisa na tatizo lililoko Wilaya ya Itilima. Zaidi ya zahanati 10 tumepata vibali lakini hatuna watumishi kada ya afya, nini kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Njalu, Mbunge wa Jimbo la Itilima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ni moja ya halmashauri nchini zenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi ukilinganisha na halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika ajira za watumishi wa sekta ya afya ametoa kipaumbele katika Halmashauri na Mikoa yenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi ikiwemo Mkoa wa Simiyu na ikiwemo Halmashauri ya Itilima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo ajira zilizopita wamepata kipaumbele cha watumishi wengi, mara fursa za ajira zitakapojitokeza tutahakikisha

tunapeleka watumishi wengi zaidi Itilima ili wapate kutoa huduma bora za afya kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante, niungane na wenzangu tatizo lililopo kwenye mikoa yao, hususani katika Mkoa wetu wa Tabora hasa kwenye zahanati za pembezoni kwenye wilaya pamoja na kwenye manispaa, watumishi wa afya ni wachache sana.

Mheshimia Spika, ni lini Serikali itatuletea watumishi wa afya wa kutosha kwenye zahanati na vituo vyetu vya afya katika Mkoa mzima wa Tabora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa hakika Waheshimiwa Wabunge lakini na Wananchi wa Tanzania kwa ujumla ni mashahidi kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka hii mitatu, ameajri watumishi wengi sana wa Kada za Afya na kuwapeleka kwenye vituo vyetu vya huduma za afya.

Mheshiwa Spika, zoezi hili ni endelevu, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Munde kwamba, mara ajira za Kada mbalimbali za afya zitakapojitokeza, tutahakikisha pia tunatoa kipaumbele katika Mkoa wa Tabora lakini hasa katika vituo ambavyo viko pembezoni na vina upungufu mkubwa wa watumishi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kituo kipya cha Afya ambacho kipo katika Kata ya Misha katika Manispaa ya Tabora Mjini kina upungufu mkubwa wa watumishi lakini pamoja na vifaa. Sijui Serikali inajipangaje kukisaidia kituo kile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakasaka, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, kama ifuatavyo. Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2023/2024, tayari Manispaa ya Tabora imeshapokea zaidi ya shilingi 750,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba katika vituo vya huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, nimuhakikishie kwamba, katika eneo la vifaatiba, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha vituo vyetu vilivyokamilika lakini na vituo vya zamani vinapata vifaatiba vya kutosha kwa ajili ya kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli kituo ambacho amekitaja kina upungufu wa watumishi lakini kama ilivyo utaratibu wa Serikali, tunaendelea kupeleka watumishi kwa awamu, na tutahakikisha pia kituo kile kinapata watumishi ili waweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang, sasa aulize swali lake.

Na. 127

**Ujenzi wa barabara za ndani Katesh**

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka lami walau kilometa 10 za barabara za ndani za Mji wa Katesh ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NGEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samweli Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang' kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TARURA* imeanza utekelezaji wa ahadi hiyo ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi milioni 470.61 zimetumika katika ujenzi wa barabara kilometa 1.12 kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya kilometa 0.7 zimejengwa kwa kiwango cha lami na shilingi milioni 499.91 zimetumika. Kwa upande wa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya ya shilingi milioni 941.96 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 1.2 na utekelezaji umefikia asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kulingana na upatikanaji wa fedha ili kukamilisha ahadi hiyo ya kukamilisha ujenzi wa kilomita 10 za barabara kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali kwanza, tarehe 29 Septemba, 2022, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alitutembelea na kati ya miradi aliyokagua, alikagua ujenzi wa barabara za lami Mji wa Katesh aliahidi kwa mwaka ule wa fedha 2022/2023 ameshaongea na Mheshimiwa Rais angeongeza fedha kwa ajili ya kilometa moja na hizo fedha hazikuja kwa mwaka huo wa fedha.

Je, Serikali sasa iko tayari kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024 kutupa fedha za kilometa moja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mradi huu kidogo hauendi kwa kasi ili kufikia kilometa 10; je, Serikali ina mkakati gani mahususi ili kujenga barabara za lami katika Mji wa Katesh? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Samwel Hhayuma. Swali la kwanza na la pili yote nitayajibu kwa pamoja. Ahadi hizi za viongozi ni lengo la Serikali kuzikamilisha zote kwa wakati na kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anafahamu tayari asilimia 30 ya ahadi hii ya barabara ya kilometa 10 imeshafikiwa mpaka hivi tunavyozungumza.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ahadi hiyo ya kilometa 10 iliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ahadi pia iliyotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutahakikisha fedha inapopatikana ahadi hizi zinaenda kutekelezwa kwa ujenzi wa barabara hizi za lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Serikali iliahidi ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, kilometa tano katika Halmashauri ya Mji wa Tarime. Je, ni lini Serikali itapeleka pesa ili mradi huo uanze?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ili barabara hiyo ya kilometa tano ambayo imeahidiwa na Serikali Tarime iweze kuanza kujengwa, tutakaa na Mheshimiwa Mbunge kuweza kuona ni nini kinaweza kikafanyika na fedha ikipatikana basi ahadi hii iweze kutekelezwa mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa kilometa tano za lami Babati Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni lengo la Serikali kuhakikisha ahadi zote za Viongozi wetu Wakuu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu zinatekelezwa kwa wakati na tutaendelea kuratibu kupitia Ofisi ya *TARURA,* Mkoa wa Manyara, Ofisi ya *TARURA,* Wilaya ya Babati, kuona ni kiasi gani kinahitajika ili tuweze kutafuta fedha kuweza kutekeleza ahadi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais alipokuja Liwale

ametuahidi kutujengea barabara ya Nangurukuru - Liwale, vilevile alituahidi kutujengea barabara kilometa mbili kwa ajili ya Liwale Mjini. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ziara ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mkoani Lindi, ilifanyika muda si mrefu sana kutoka sasa. Tunaendelea kuratibu ahadi zote ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutafuta fedha kwa ajili ya kupeleka mara moja katika maeneo mbalimbali ambapo ahadi hizi zimetoka ikiwemo kule Liwale kwa Mheshimiwa Kuchauka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na jitihada za Serikali kujenga barabara za lami kwenye miji yetu, kumekuwa na shida kubwa ya ubora wa wakandarasi wanaotekeleza miradi hii hasa maeneo ya pembezoni kama ilivyo Ukerewe. Je, ni nini mkakati wa Serikali kushughulikia changamoto hii? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkundi. Ni mkakati wa Serikali sasa kupitia Taasisi yetu ya *TARURA* kuhakikisha tunanunua mitambo na kupeleka maeneo ya pembezoni ikiwemo kule Ukerewe kwa ajili ya kuweza kutengeneza barabara hizi mara kwa mara. Changamoto ambayo inapatikana kwenye maeneo kama Ukerewe, maeneo kama Mafia ni wakandarasi kuweza kupeleka mitambo katika maeneo yale na tayari Serikali imeliona hili na

itanunua mitambo yake yenyewe kwa ajili ya kupeleka kwenye maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuboresha barabara kwa kiwango cha lami katika Kata za Mikumi na Ruaha ambazo ni Kata za kimkakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itatekeleza ahadi hii ya kuboresha Barabara za Mikumi na Ruaha kwa kiwango cha lami kadri ya upatikanaji wa fedha. Nitakaa na Mheshimiwa Londo kuona ni namna gani ambavyo tunaweza tutaratibu hili kupitia Ofisi ya Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Kilosa na Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Morogoro ili tuweze kutekeleza ahadi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya kutoka Vwawa – London - Msiya hadi Isarawe, ambayo ni ahadi ya Serikali kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutaanza kutekeleza ahadi hii kadri ya upatikanaji wa fedha, lakini tutakaa tena na Mheshimiwa Mbunge, kuweza kuona ni namna gani tutaratibu hili kupitia Mameneja wetu wa mikoa na hasa Meneja wa Mkoa wa Songwe kuona tunaanzaje kutekeleza ahadi hii ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, wamejenga barabara ya kilometa 2.5 ya *breweries* kwa kiwango cha lami kwa kilometa 1.7 na kimebaki kipande kidogo cha mita 750. Je, ni lini watakamilisha ujenzi huo kwa maana sasa ujenzi umesimama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nitakaa na Mheshimiwa Mabula kuona ni namna gani ambavyo Serikali inaweza ikaliratibu hili na kukamilisha kipande hiki cha barabara ambacho kimesalia kwa kuwasiliana na Meneja wa *TARURA,* Mkoa wa Mwanza na Meneja wa *TARURA,* Wilaya ya Ilemela kuona ni kiasi gani kinahitajika ili kuweza kukamilisha ahadi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge,

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa, Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, sasa aulize swali lake.

Na. 129

**Mradi wa Umwagiliaji wa Udagaji – Mlimba**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Umwagiliaji wa Udagaji katika Kata ya Ching'anda Mlimba utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Jimbo la Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Skimu ya Umwagiliaji ya Udagaji/Mgugwe yenye ukubwa wa hekta 1,280 ni miongoni mwa skimu tatu za Bonde la Mto Kilombero ambazo zilifanyiwa upembuzi yakinifu na Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID)* mwaka 2016. Skimu zingine zilizofanyiwa upembuzi yakinifu kupitia ufadhili huu ni Mpanga, Ngalamila yenye ukubwa wa hekta 28,141 na Kisegese yenye ukubwa wa hekta 16,130 zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba katika Bonde la Mto Kilombero.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga bajeti kwa ajili ya kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na kufanya usanifu wa kina wa skimu hizo. Aidha, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ipo katika hatua za manunuzi na kumpata Mshauri Elekezi wa kutekeleza kazi husika. Hivyo, ujenzi wa Skimu ya Udagaji Mlimba unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 baada ya kukamilika kwa kazi ya usanifu wa kina ili kubaini gharama halisi za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Godwin Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Skimu ya Umwagiliaji ya Njage ilisanifiwa kutoa huduma kwenye hekta 1,750, mpaka sasa ni hekta 750 tu ambazo miundombinu ya umwagiliaji imefika.

Je, ni lini Serikali itakamilisha hizi hekta 1,000 zilizobaki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Skimu ya Idete ni skimu inayonufaisha Jeshi la Magereza tu na Idete, wananchi wa Kata ya Idete hawanufaiki; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi pia wa Idete wawe sehemu ya kunufaika kwenye mradi huu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumjibu Mheshimiwa Kunambi Mbunge wa Jimbo la Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, tunatambua kwamba Skimu ya Njage ambayo hekta ambazo zinatumika mpaka sasa hivi ni 750 na 1,000 bado hazijafanyika. Nimwondoe hofu kwamba nimezungumza na *DG* wa Tume ya Umwagiliaji kuhusu *expansion* ya mradi huu kumalizia hizi 1,000. Kwa hiyo, amesema tutaliweka katika mipango yetu ya kibajeti ili kuhakikisha tunalikamilisha kwa wakati ili wananchi wake waweze kupata faida ya kulima katika eneo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Skimu ya Idete…

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, husikiki vizuri, sijui kama ni *mic* inakuwa mbali ama ni sauti yako siku hizi umeamua kuipunguza kidogo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni *mic*. Basi naomba nirudi upya jibu la kwanza la nyongeza. Kuhusu Skimu ya umwagiliaji ya Njage ambayo bado hekta 1,000 katika 1,750 zilizokuwa zitumike tangu awali, ni kwamba nimezungumza na Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji na amekubali kuliweka katika mpango kuhakikisha kwamba hizi 1,000 nyingine zinaingia tuweze kuzikamilisha kwa wakati ili wananchi wa Jimbo la Mlimba kwenye Skimu ya Njage waweze kupata huduma ya umwagiliaji kwa ukubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Skimu ya Idete ambayo inatumika na Magereza na yenyewe tumekubaliana kwamba tutakwenda kufanya usanifu wa kina kuongeza *expansion* ili wananchi wa Kata ya Idete waweze kufaidika. Magereza watumie na wananchi wa kawaida wa Kata ya Idete na wenyewe waweze kunufaika na skimu hiyo.  Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, swali la nyongeza.

Visemeo havifanyi kazi, Mheshimiwa Naibu Waziri zima kwanza kisemeo.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona, kwa sababu Serikali imefanya kazi nzuri ya kuhimiza umwagiliaji na kadhalika. Njombe tumepata miradi hiyo na wananchi wamefaidika, wamelima mahindi na wamepata mazao mengi sana. Serikali imenunua mahindi tunaishukuru. Je, Serikali ni lini itawatamkia wananchi wa Mkoa wa Njombe itakuwa tayari kuwalipa hela walizouza mahindi yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumjibu Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Serikali ilinunua mahindi karibu tani 202,000 na thamani ya tani ambazo tulikuwa tumenunua ilikuwa ni karibu bilioni 187 na tumeshalipa na mpaka sasa hivi tudaiwa kama bilioni 56 ili kumaliza katika deni la awali.  Tuko katika mchakato wa mwisho wa kuwalipa wakulima wote nchini wenye thamani ya hilo deni ambalo nalizungumzia la bilioni 56. Kwa hiyo nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge na baada ya kumaliza malipo, Serikali kupitia *NFRA* tutaendelea kununua tena mahindi ili kutimiza lengo ambalo tumejiwekea kwa mwaka, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa wananchi wa Kata ya Muhamo na Msange katika Jimbo la Singida Kaskazini wamesubiri kwa muda mrefu mradi wa umwagiliaji. Je, ni lini Serikali itatangaza mradi huo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kwamba Mradi wa Muhamo upo katika mpango wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na nimwondoe tu shaka Mbunge kwamba, sasa hivi tuko katika mchakato na tukishakamilisha tu watapata matokeo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mradi wa Umwagiliaji wa Luamfi ni mradi muhimu sana kwa wakulima wa Ziwa Tanganyika. Je, ni lini mradi huu utakamilika kwa kuwa umekuwa unasuasua sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimwondoe tu shaka Mheshimiwa Mbunge Aida Khenani kwamba, maeneo yote yanayofaa kwa umwagiliaji ikiwemo mradi ambao ameutaja wa Luamfi ni kwamba yote tumeweka katika mipango yetu, ambayo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaitekeleza. Nimhakikishie pia kwamba, bahati nzuri Mheshimiwa Rais anatuunga mkono sana na ameweka jitihada kubwa pamoja na fedha kuhakikisha maeneo yote yanayofaa yanafikiwa. Kwa hiyo hata hilo lenyewe tutalikamilisha kwa wakati, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 130

**Ujenzi wa barabara ya Makofia - Mlandizi**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, lini barabara ya Makofia - Mlandizi itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Kesekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Makofia - Mlandizi, kilomita 35 ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imepanga kujenga daraja dogo *(box culvert)* katika eneo la Mbwawa. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali

mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; barabara hii iliyofanyiwa tathmini, je, ni lini wananchi wake watalipwa fidia zao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; miezi miwili iliyopita, nilihudhuria utiaji saini Mkataba wa *BRT*, awamu ya tatu ambao umejumuisha ujenzi wa kipande kilichobakia cha Barabara kutoka Tamko kuja Mapinga Bagamoyo. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kipande hiki cha barabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Barabara hii ya Makofia - Mlandizi tulishakamisha usanifu na tulifanya tathmini kwa maana kupata gharama ya fidia mwaka 2018, lakini hatukufika mpaka mwisho. Kwa hiyo zoezi hilo limerudiwa na Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba tayari watu wameshapita na hatua ambayo tunayo sasa hivi, ni kupata uhakiki ili jedwali la malipo liende Hazina kwa ajili ya kuandaa malipo. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, zoezi hilo linaendelea na watalipwa baada ya kuhakikiwa na kuridhika kwamba hiki ndio kiasi ambacho wanatakiwa walipwe hao ambao wataipisha hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala lake la pili ni kweli Barabara ya Tamko – Mapinga tulishatia saini na nakiri kushiriki. Mheshimiwa Mbunge, atakubaliana nami kwamba, barabara hii haikuwa na hifadhi ya kama barabara. Sasa Mkandarasi kuna mambo ya kimkataba ambayo anakamilisha na sisi kama Serikali tuko tunamfuatilia kuona anakamilisha zile taratibu ili aanze kuijenga na tuko kwenye hatua za mwisho, barabara hiyo sasa itaanza kujengwa kwa sababu tayari tulishawekeana saini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Barabara ya kutoka Tarime Mjini mpaka Mugumu ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania na Mkoa wa Mara kwa ujumla kwa sababu inaunganisha kwenda kwenye utalii na ilitengewa fedha kuanzia mwaka 2021/2022, takribani bilioni 35, lakini Serikali imekuwa ikipeleka fedha kwa kusuasua mpaka sasa hivi imepeleka bilioni tano tu.

Je, ni lini, Serikali itahakikisha kwamba inampelekea mkandarasi fedha kwa wakati ili aweze kukamilisha ile barabara kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii ni muhimu na hii barabara imegawanywa katika *lot* mbili, hatupeleki hela yote, tunalipa kulingana na mahitaji ya mkandarasi. Kwa hiyo akishaleta hati ya malipo ndipo tunapomlipa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kulipa kadri hati zinavyokuja kuhakikisha kwamba barabara yote ya Tarime - Mugumu inakamilika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yawe mafupi, Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kilometa 54 za lami kwa wananchi wa

Ushetu ambapo Serikali iliahidi yenyewe, lakini hakuna dalili yoyote inayoendelea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli kwamba Serikali iliahidi kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Barabara zote zinazofanana na hiyo ya Ushetu, mpango wa Serikali ni kuzijenga kwa kiwango cha lami, lakini utakubaliana nami kwamba hapa ndio tunapopitisha bajeti, kwa hiyo bajeti ndio inayoamua. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi tutaendelea kuweka kwenye mipango ile ahadi ya Serikali ambayo tuliahidi iweze kutimia kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Barabara ya Mgololo - Mafinga itajengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu hii barabara ni kitega uchumi katika Jimbo la Mufindi Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Mgololo – Mafinga ni kati ya barabara sita ama saba ambazo tunazijenga kwa utaratibu wa *EPC + F* na nimelijibu mara kadhaa kwamba tayari kazi zinaendelea za awali kwa wakandarasi ambao wamepatikana kuijenga hii barabara. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ni kati ya barabara ambazo zinatekelezwa kwa Mpango wa *EPC + F* na tutahakikisha kwamba hiyo barabara inajengwa kama Serikali ilivyoahidi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa, barabara ya Utegi – Shirati mpaka Kihongwe Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekwishakamilika na barabara hii tayari imetengewa fedha. Ninataka kujua kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa barabara hii itatangazwa na kuanza ujenzi wa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chege, swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli bahati nzuri barabara hii nimetembelea tukiwa na Mheshimiwa Mbunge na aliahidiwa kwamba barabara hii itaanza kujengwa. Barabara hii ipo kwenye mpango wa kuanza kuijenga kwa kipindi cha bajeti hii ya 2023/2024. Kwa hiyo, taratibu za kuandaa *tender document* zinaendelea, basi zikikamilika barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. Ujenzi wa barabara ya kutoka Kabingo hadi Kibaoni kilometa 25 kwa kiwango cha lami unasuasua sana.

Je, ni lini Serikali itakwamua ujenzi wa barabara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii inayoisema ni *Kibondo link,* barabara ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami. Nimeitembelea hiyo barabara kuangalia changamoto zilizopo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshaona changamoto zilizokuwepo za kiutendaji kwa Mkandarasi na tuna hakika baada ya kukaa nae barabara hii sasa itaanza kwenda kasi ili tukamilishe zile kilometa 25. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara ya MR – Pawaga kwa kiwango cha lami kuanzia MR – Iringa Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba katika bajeti ya mwaka huu kuna kiasi kimetengwa kwa ajili ya kuanza kilomita kama sikosei ni kilometa kama 20 kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, kadri tutakavyokwenda taratibu zikishakamilika barabara hizo zitatangazwa kwa ajili ya kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri; barabara ya Nkome – Nzela – Geita yenye urefu wa kilometa 20 mwaka wa tatu Mkandarasi amepatikana tunasubiri kusaini.

Je, huna mafuta nikuwekee ili tuende tukasaini kesho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan haiwezi kukosa mafuta ya kwenda kusaini, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunatambua umuhimu wa hiyo barabara ni suala la muda tu na ipo kwenye mipango, muda ukifika nina hakika barabara hii tutaisaini kwa sababu tayari imeishatengewa fedha na kila kitu kimekamilika. Kwa hiyo, tunachosubiri tu ni suala la taratibu zikamilike ili Mkandarasi aweze kuanza kazi hiyo ya kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 131

**Mkakati wa kuinua miundombinu ya barabara na maendeleo Lindi na Mtwara**

**MHE. TECLA M. UNGELE** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuboresha miundombinu ya barabara na kuinua maendeleo mikoa ya Lindi na Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifautavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Mtwara, Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara ya Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala – Masasi yenye urefu wa kilometa 210, ambapo sehemu ya Mtwara – Mnivata kilometa 50 ujenzi umekamilika na sehemu iliyobaki ya Mnivata – Newala – Masasi kilometa 160 pamoja na Daraja la Mwiti ujenzi umeanza na unatarajiwa kukamilika mwishoni

mwa mwaka 2026. Aidha, Serikali imepanga kuifanyia ukarabati barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi kilometa 200 ambapo maandalizi ya kutangaza zabuni za ukarabati wa barabara hii yako katika hatua za mwisho.

Mheshimwia Spika, kwa upande wa Mkoa wa Lindi, Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara ya Nanganga – Ruangwa kilometa 53.2 ambapo umefikia asilimia 74 na ujenzi wa barabara ya Nachingwea – Ruangwa kilometa 52.8 upo hatua za mwisho za manunuzi. Aidha, ujenzi wa barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale kilometa 175 utatekelezwa kwa utaratibu wa *EPC + F* na tayari mkataba wa ujenzi umesainiwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Lindi na Mtwara tunashukuru kwa jitihada za Dkt. Samia Suluhu Hassan kutuletea maendeleo na ndiyo maana akaridhia kusaini kwa Mkataba huo wa *EPC + F* hapo Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kusaini mkataba ni jambo moja na kuanza ujenzi ni jambo lingine; je, ni lini sasa Mkandarasi ataanza kazi ya Ujenzi Masasi – Nachingwea – Liwale? *(Makofi)*

Swali la pili; je, ni lini sasa barabara ya Nachingwea kwenda Kilimarondo itajengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tecla Ungele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Masasi – Nachingwea hadi Liwale kilometa 175 kama nilivyosema katika jibu la msingi inatekelezwa kwa utaratibu wa *EPC + F* na iko kwenye hatua kama ambavyo barabara zote zipo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Waziri alitolea maelezo wako wanapitia usanifu wale Wakandarasi ambao wamepewa hizo barabara na tunategemea Januari wakandarasi watakuwa wako *site* baada ya kukamilisha zile taratibu zao za kupitia ule usanifu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hilo linaendelea na barabara hizo zitaanza kujengwa. Kinachoendelea tu hapa ni kwamba ni utaratibu ambao ni mpya kwetu sisi lakini wanatakiwa wale ambao wamepewa hizo kazi nao lazima wapitie usanifu na wajiridhishe.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu barabara aliyoitaja hiyo kwenda Kilimarondo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hiyo baada ya kufanyiwa usanifu bajeti ikiruhusu basi tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami, kwa sababu lengo la Serikali ni kuzijenga barabara hizi kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nami niulize swali moja la nyongeza.

Barabara ya kutoka Mtama – Kitangali hadi Amkeni – Newala, yenye urefu wa kilometa 74 ipo kwenye zoezi la Upembuzi Yakinifu, ni lini zoezi hili litakamilika ili barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, suala la upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ni suala ambalo linategemeana na aina ya barabara yenyewe. Kwa hiyo, mandhari tumeanza tunategemea kwamba, usanifu kwa urefu wa kilometa hizi 74 haziwezi kuzidi mwaka lakini namshawishi Mheshimiwa Mbunge

kwamba, tunategemea ndani ya mwaka mmoja baada ya kuanza usanifu utakuwa umekamilika wa hii barabara, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Kwa kuwa ujenzi wa barabara ya Ifakara – Kidatu unakaribia kukamilika na kwa kuwa kumekuwa na ajali nyingi sana katika eneo la Mang'ula Kona kutokana na eneo la hifadhi kuingia barabarani, na kwa kuwa, kupitia Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Rais alililiridhia akatupatia eneo la hifadhi ili tuweze kupasafisha kusaidia magari kuonana, na kwa kuwa Waziri wa Ujenzialifika katika eneo husika akaahisi kwamba eneo hilo litasafishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa swali lako?

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, swali langu ni lini ahadi hiyo ya kusafisha Mang'ula Kona itaanza kutekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara anayoitaja hii ya Kidatu kwenda Ifakara ni barabara kuu na bahati nzuri kwenye hiyo kona ya Mang'ula Kona mimi nimefika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Wizara ilishaelekeza baada ya maombi ya Mheshimiwa Mbunge lakini pia na Waziri kutoa maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa Morogoro aende akaangalie namna ambavyo watafanya kupunguza ile kona. Kwa sababu kupunguzwa kwa hiyo kona haikuwa sehemu ya usanifu wa hiyo Barabara, kwa hiyo lazima waende wakafanye usanifu mpya wa eneo na kuona gharama ya kufanya hiyo kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya Nanganga – Nachingwea kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nilisema kwamba barabara ya Nachingwea – Nanganga ipo katika hatua za mwisho na tunategemea katika zile barabara ambazo tunategemea kuzisainia kwa pamoja hiyo barabara ni mojawapo ya Nanganga – Nachingwea. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; nini mkakati wa Serikali sasa kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Mtwara – Pachani na Nalasi – Tunduru ambayo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulishafanyika na ipo kwenye Ilani, na ndiyo tunayoisubiri barabara hii inayotegemewa na vijiji vingi zaidi ya 50 katika eneo hilo la Namtumbo na Tunduru? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua umuhimu wa hii barabara ya Mtwara – Pachani hadi Nalasi – Tunduru ambayo ina urefu wa kilometa 300. Wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami, tulichoshauri na tunachokifanya sasa hivi katika barabara hiyo ni kwanza kuhimarisha madaraja ambayo ina madaraja mengi ya mito.

Pili, ni kujenga kwa kiwango cha zege ama lami maeneo yote ambayo huwa yanakwamisha usafiri katika hiyo barabara ili

wananchi waendelee kupita kipindi chote wakati Serikali inatafuta fedha ya kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ni takribani miezi mitano imepita sasa hivi tangu mikataba ya ujenzi wa barabara ya Mnivata – Nanyamba – Newala hadi Masasi imesainiwa.

Je, ni lini ujenzi huu utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza mimi niseme kama kuna barabara ambayo wenzetu hawatakiwi kuwa na wasiwasi ni hiyo barabara ya Mnivata – Newala kwenda Masasi.

Mheshimiwa Spika, taratibu ambazo zinaendelea sasa hivi ni taratibu za maandalizi kwa maana ya *mobilization* na wenzetu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika ndiyo ambao tunasaidiana nao kuijenga hiyo hiyo barabara.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni taratibu tu zinaendelea za kimkataba lakini muda siyo mrefu watawaona sasa wakiwa wako *site* katika hivyo vipande viwili, ambavyo barabara hiyo imegawanywa katika vipande viwili, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua au kurekebisha barabara ya Kilwa kipande cha Mbagala Zakheim kutoka Zakheim

mpaka Mzinga, kwa sababu kipande hicho kimekuwa na changamoto, unatoka huko lakini unafika pale magari hayaendi, kunakuwa na msongamano mkubwa sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, barabara zote za Dar es Salaam kulingana na ukuaji wa mji zinafanyiwa *study* kuona barabara zote ambazo zina changamoto zinafanyiwa marekebisho, ikiwa ni pamoja na kuongeza upana wa barabara hizo, na siyo za Dar es Salaam tu hata barabara za Mikoani ambazo zilijengwa zamani nyingi zilikuwa na upana mdogo.

Kwa hiyo, sasa hivi hizo barabara zinapitiwa upya ikiwa ni pamoja na barabara aliyoitaja ili kuhakikisha kwamba sasa tunakwenda kwa kipindi cha sasa kuzipanua hizo barabara, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa wananchi wa Haydom wameshawapa eneo la kujenga majengo ya mkandarasi ili aanze kazi na wewe ulikuja kusaini ule mkataba.

Je, ni lini anakuja kujenga yale majengo ili barabara ianze kujengwa ya Haydom – Labay?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri hiyo barabara mkandarasi ambaye anajenga kipande cha kwanza ndiyo atakaejenga kipande cha pili. Kazi anayofanya sasa hivi ni

kufanya usanifu, kwa sababu barabara hiyo inayojengwa ni sanifu inajengwa na atakapokuwa amekamilisha nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ndipo atakapoanza sasa kujenga hiyo kambi yake eneo ambalo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Mbulu kwa kulitoa hilo eneo la ujenzi bure kabisa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Je, ni lini Serikali sasa mtaanza ujenzi wa barabara muhimu ya kutoka Lujewa – Madibila mpaka Mafinga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Bahati Ndingo, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hiyo barabara ni muhimu na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mheshimiwa Rais akiwa ziara katika Mkoa wa Iringa alitoa maelekezo hiyo barabara ianze kujengwa kwa kiwango cha lami kilomita 25. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, sasa hivi tuko kwenye hatua za manunuzi kutekeleza hiyo ahadi na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua tunao ujenzi wa kilomita moja ya lami Mji wa Karumwa, takribani miezi 24 na tuta lile limenyanyuliwa zaidi ya mita moja, mvua zinaendelea kunyesha na

maji yanaingia kwenye nyumba za watu imekuwa ni kero kubwa. Miezi 24 kilomita moja haijakamilika, nataka kauli ya Serikali ni lini kilomita moja hiyo itakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninakiri kwamba, Mheshimiwa Mbunge amekuja ofisini kufuatilia hili suala, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mji wa Karumwa, nimeongea na Meneja wa Mkoa wa Geita kwamba hiyo barabara itakamilishwa. Sasa hivi kilichokwamisha tu ni kwamba mvua inanyesha na baada ya hapo kwa sababu ipo chini ya Meneja wa Mkoa wa Geita, wataikamilisha hiyo barabara ikiwa ni pamoja na kutengeneza hiyo mifereji ambayo inaleta adha kwa wananchi wa Karumwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Mheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi na Kujenga Taifa, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na.132

**Wazee waliopata ulemavu katika Vita ya Kagera**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR. KHAMIS** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kuwasaidia wazee waliopata ulemavu wakati wa kupigana Vita ya Kagera mwaka 1979?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa wazee walemavu wa vita ya Kagera wapatao 272 wanalipwa pensheni ya ulemavu. Baada ya vita kumalizika Serikali iliwasaidia wapiganaji wote waliopigana vita. Wengi kati ya wapiganaji hao walipewa ajira katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama hususan Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza. Aidha, wapo walioshindwa kuajiriwa kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wazee walemavu waliopigana vita ya Kagera wanaendelea kupata matibabu katika hospitali za Jeshi na wanalipwa pensheni za ulemavu kwa mujibu wa Kanuni za Pensheni na Viinua Mgongo za mwaka 1966. Wizara inaendelea kufuatilia hali halisi za wazee waliopigana vita ili kuchukua hatua stahiki. Endapo kuna wazee na walemavu waliopigana vita ya Kagera ambao hawanufaiki na huduma zinazotolewa inashauriwa wawasilishe taarifa zao kwa ajili ya uhakiki na hatimaye waweze kunufaika na huduma hizo, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Sina budi kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jawabu lake zuri, litatoa matumaini kwa wazee wetu ambao kwa umri waliokuwanao sasa hivi hali yao kweli siyo nzuri tena.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya wazee hawa hawana familia, wanahitaji kuishi, lakini na bado wanaendelea kupita maofisini kuomba misaada: Je, kwa nini Serikali haiwezi kufanya

mpango wa kuwatafutia mahala pa kuwaweka na kuwatunza wazee hawa ili kumaliza maisha yao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa wastaafu Serikalini hulipwa *pension* ya uzeeni hadi kufariki kwao, lakini kwa wazee hawa wanalipwa *pension* ya ulemavu: Kwa nini nao wasichanganywe katika kupewa *pension* ya uzeeni kama wanavyolipwa wastaafu wengine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, mapendekezo ya kuwatafutia mahali au kwa maneno mengine wajengewe makazi kwa sababu hawana familia; mfumo wa uendeshaji wa Serikali zetu za Mitaa na mambo ya Ustawi wa Jamii yanaruhusu pale ambapo mtu anakuwa hajiwezi kabisa, yapo makazi yaliyokuwa *dedicated* kwa ajili ya wazee hao. Pengine naomba wale ambao wameshindwa kabisa, wawasiliane na halmashauri zao ili kuona namna ya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisera tunapendelea zaidi wazee walelewe na vijana au ndugu zao kama utamaduni na maadili mema ya Watanzania yanavyofanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwachanganya hao ambao ni wapiganaji wa vita na wazee wengine wapate *pension* ya uzeeni, hili ni suala la kisera, litafikiriwa na Wizara husika ili tuweze kuona uwezekano wa kulitekeleza, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inatoa tamko gani kwa wale maaskari wapiganaji waliopigana Vita vya Kagera ambao hawakuajiriwa na sasa wana maisha duni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, ni kwamba kwa mujibu wa takwimu tulizonazo, wazee wote ambao wanapata huduma ya *pension* na usaidizi wa kimatibabu ni 272. Kama wapo wazee ambao kwa bahati mbaya hawakuingia kwenye orodha hiyo, tumeelekeza waende karibu na vikosi vya Jeshi vilivyoko jirani na makazi waliyopo ili taarifa zao zihakikiwe na hatimaye waweze kupata huduma kama zile wanazopata wazee wenzao waliopigana vita hii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na utaratibu sasa hivi, wazee wanatufuata kule vijijini au watoto wao wakiamini kwamba wanadai fidia kutokana na ushiriki wao kwenye Jeshi lile la Mkoloni *(KAR)* au Vita ya Kagera. Nataka kufahamu kutoka Serikalini, hivi ni kweli kuna watu wanaodai fidia kutokana na maeneo hayo mawili niliyoyataja kwa maana Jeshi la *KAR* pamoja na Jeshi la waliokwenda kupigana kwenye Vita ya Kagera?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu swali la msingi ni Vita ya Kagera, naomba suala la *KAR* liweze

kuletwa kama swali la msingi ili tuweze kulifanyia utafiti na hatimaye tutoe majibu fasaha katika Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwepo wa Wazee wa Vita ya Kagera ambao pengine wanalalamika kutopata fidia, ndiyo maana nimesema, tunazo takwimu kwamba wapo 272, kama wapo wazee wa namna hiyo Mheshimiwa Mbunge, nimeeleza hapa katika moja ya jibu la msingi kwa Mbunge aliyetangulia, waripoti kwenye Makambi ya Jeshi yaliyoko karibu na maeneo yao ili taarifa zao zihakikiwe, hatimaye waweze kapata haki wanayostahili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Hili suala la wazee waliopigana vita vyetu kuidai Serikali limekuwa ni suala la muda mrefu na limekuwa kila siku likitolewa majibu: Je, ni lini sasa Serikali inaliahidi Bunge hili kwamba suala la wazee hawa litatolewa majibu ya mwisho na kutatuliwa liishe kabisa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nikirejea majibu yangu ya swali la msingi, kwa mujibu wa takwimu zilizopo kwenye Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni kwamba wako wazee 272. Sasa kama wapo wazee wengine ambao kwa bahati mbaya wanaamini kwamba wana madai ya msingi, lakini hawamo kwenye orodha hii, tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili wazee hawa wahahakikiwe taarifa zao, ikithibitika kwamba wanastahili Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, itawalipa hizo haki stahiki, ashante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, lakini utatupelekea salamu hizo kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika, kwa sababu ni kweli wazee hawa waliopigana Vita ya Kagera wako waliopata ulemavu na wapo ambao hawakupata ulemavu lakini Mungu amewajaalia umri mrefu. Sasa wanapokuwa kila wakati wanafikiria kuna jambo, ni vizuri wajue hakuna jambo.

Pia ni kwa sababu ni wachache, siyo wengi, Serikali inaweza kuona namna bora ya kuwasaidia ili maisha yao haya ya mwisho yaende vizuri. Hilo utatupelekea kwa Mheshimiwa Waziri wajaribu kulitazama kwa ujumla wake, ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, Mbunge wa Kiwani, sasa aulize swali lake.

Mheshimiwa Naibu Waziri kumbe unabaki hapo hapo. Endelea kujibu.

Na. 133

**Ujenzi wa Ofisi ya Polisi Jamii Shehia ya Kendwa**

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Polisi Jamii Shehia ya Kendwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshiniwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Ofisi ya Polisi Jamii inayojengwa Jindamiti katika Shehia ya Kendwa, inajengwa kwa nguvu na michango ya wananchi na wadau na ujenzi wake umefikia hatua ya lenta. Lengo la kujenga ofisi hiyo ni kutumiwa na vikundi vya ulinzi shirikishi vya Shehia ya Kendwa. Wajibu wa Serikali ni kujenga Ofisi na Vituo vya Polisi ambavyo hutumiwa na Askari Polisi katika kudhibiti uhalifu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge aendelee na jitihada za kuwahamasisha wananchi na wadau kukamilisha ujenzi wa ofisi hiyo ili iweze kutumiwa na vikundi vya ulinzi shirikishi kama walivyofanya wananchi wa Chambani, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Suala hili lilikuwa ni kama ukumbusho. Kipindi kilichopita niliuliza suala hili na jawabu likatoka kwamba wananchi wavute Subira, tutatumia Mfuko wa Tuzo na Tozo katika kipindi hiki ili tuweze kuikamilisha ofisi; lakini sasa majibu wa Mheshimiwa Naibu Waziri yanasema, sasa nitafute wadau; je, ni lipi jawabu sahihi la kushika? Nitafute wadau au Mfuko wa Tuzo na Tozo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kufuatana nami baada ya Bunge hili ili aende akaone nguvu za wananchi walizozitumia katika ujenzi huo ili naye aweze kuona kwamba tutumie wadau au wa tuzo na tozo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakiri swali la Mheshimiwa Mbunge kuhusu kutumia wadau au tuzo na tozo, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, ni kweli kwamba tuzo na tozo hutumika kukamilisha Vituo vya Polisi vya ngazi ya jamii kuunga mkono nguvu za wananchi au ngazi ya Wilaya, Tarafa na Mkoa kwa ajili Askari wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hivi vituo vya ulinzi shirikishi ambapo ni juhudi zinazotokana na utashi wa wananchi wenyewe, tumekuwa tukishauri watumie nguvu za wananchi na wadau kuliko kazi ya msingi ya Jeshi la Polisi haijakamilika tuhamishie rasilimali kidogo tulizonazo kwenye jambo ambalo kimsingi lingeweza kufanywa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufuatana naye, nipo tayari. Kwa kweli maeneo yake nimeshafika mara kadhaa, nadhani ratiba itakavyoruhusu tutakwenda kuangalia tushirikiane naye kuhamasisha wananchi ili waweze kukamilisha kituo hicho, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri: Ni lini atawezesha wananchi wa Mwika Kaskazini kwa kumalizia kituo chao ambacho alikitembelea na akaahidi kwamba tukimaliza kupaua, basi tutapata uwezeshaji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya kauli ile kama unavyokumbuka tulikuwa wote Mheshimiwa Dkt. Kimei, tukasema *IGP* na imewekwa kwenye mpango wa ukamilishaji katika mwaka wa fedha unaoanza 2024/2025. Hiyo ni *commitment,* tutalitekeleza Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 134

**Tatizo la kukatika umeme Manispaa ya Morogoro**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la kukatika kwa umeme katika Manispaa ya Morogoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* imechukua hatua mbalimbali katika kutatua changamoto ya kukatika kwa umeme katika Manispaa ya Morogoro, ikiwa ni pamoja na kufunga *transformer* yenye ukubwa na uwezo wa *MVA* 120 katika Kituo cha Msamvu. Kazi hiyo ambayo inagharimu jumla ya shilingi bilioni 10.5 inatarajiwa kukamilika mwezi huu wa Novemba, 2023. Aidha, sambamba na hilo, *TANESCO* inaendelea na ukarabati wa miundombinu ya usambazaji wa umeme katika Manispaa ya Morogoro ili kuondoa tatizo la kukatikakatika kwa umeme katika Manispaa ya Morogoro, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Licha ya majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kata ya Mgambazi ipo kwenye Manispaa ya Morogoro, lakini mpaka sasa hivi Mtaa mzima wa Mgambazi pamoja na Chambilazi na Vilengwe hawajapatiwa umeme, licha ya kuwa kwenye Manispaa ya Morogoro: Je, ni lini watapata umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kijiji cha Zongo ambacho kiko kwenye Kata ya Kisemo pamoja na Kijiji cha Bwakila Juu katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini, hawajapata umeme. Ni lini vijiji hivi vitapatiwa umeme? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Dkt. Christine Ishengoma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na umeme katika Mitaa ya Mungazi, Chambilazi na Vilengwe tayari tumeshaiweka kwenye Mpango wa fedha wa 2025 na mitaa hii itapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Vijiji vya Zongo na Bwakila Juu, tayari wakandarasi wamepatiwa *site* na muda wowote kazi itaanza, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Serikali iliahidi kufunga umeme katika shule zote za

sekondari na taasisi za dini, lakini zipo shule ambazo hazijaweza kufungiwa umeme; je, ni lini Serikali itafunga umeme katika Shule ya Sekondari Kimenyi, katika Halmashauri ya *Kasulu DC? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Genzabuke, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tayari kuna miradi inaendelea kwenye vijiji vyote ya kupeleka umeme. Mwanzoni ilikuwa kilomita moja, tumeongeza kilometa mbili ili taasisi nyingi zifikiwe. Kwa shule hii ya Kimenyi kama haipo katika *scope* ambayo ipo sasa hivi, tutahakikisha kwamba tunaweka fedha kwenye mwaka ujao ili na wenyewe waweze kupatiwa umeme, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wananchi wa Kilwa wamekuwa ni wanufaika wakubwa wa umeme wa gesi unaozalishwa katika Kituo cha Somanga.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukiboresha kituo hiki ili kumaliza changamoto kubwa inayokabili wananchi wa Kilwa katika huduma ya umeme? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndulane, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tayari tumeanza mkakati wa kurekebisha kufanya matengenezo kwenye visima vyetu ambavyo vinazalisha gesi na tumeshaanza *Mnazi Bay,* Songosongo pamoja na Madimba. Kwa Somanga pia tutahakikisha tunaweka kwenye mkakati ili

tuweze kukiboresha na wananchi wa Kilwa waweze kupata umeme wa uhakika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo la kukatika umeme katika Manispaa ya Morogoro linafanana na tatizo lililopo katika Wilaya na Mkoa wa Kilimanjaro, hususan Kata ya Uru Kusini; ni lini sasa *TANESCO* itarekebisha tatizo hilo kabisa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tatizo la kukatika kwa umeme halipo tu Morogoro na Kilimanjaro, limekuwepo kwa Tanzania nzima. Serikali tumechukua hatua. Mwanzoni tulianza na upungufu wa Megawati 421 wastani hapo. Mpaka kufikia leo tumefanikiwa kupunguza upungufu kwa wastani wa Megawati 218. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, nilieleza hapa kwamba Bwawa la Mwalimu Nyerere tumefikia 94.01% na tumeshaanza majaribio. Pia, nimesema hapa tumeongeza uzalishaji kwenye visima vetu vya Songo Songo pamoja na Madiba ili kuweza kuongeza gesi ili tuweze kupunguza changamoto hii ya upatikanaji wa umeme. Tayari tunafanya matengenezo kwenye mitambo yetu yote ili kuboresha hali. Nina uhakika Waheshimiwa mmeona hali ya upatikanaji wa umeme imeanza kutengemaa.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie tutaendelea kufanya kazi hii nzuri ili kuhakikisha tunaiondoa nchi katika changamoto ya umeme, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Makofi ni mengi lakini naona Wabunge bado mmesimama. Sasa sijaelewa vizuri.

Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nami niulize swali la nyongeza. Wilaya ya Uyui Makao Makuu yake…

**SPIKA:** Hausikiki vizuri Mheshimiwa.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Uyui Makao Makuu yake ni Isikizya, kilometa 35 kutoka Tabora Mjini, na lipo tatizo kubwa kweli la umeme. Watumishi pale; *DC* na Wakurugenzi hawafanyi kazi kutwa nzima, umeme unakatika zaidi ya mara tano kwa siku; je, Serikali ina mpango gani wa kuweka umeme wa kudumu pale Isikizya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Maige, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali tumechukua hatua katika Halmashauri ya Uyui na katika Mkoa mzima wa Tabora. Tumechukua hatua na tuna mradi unaendelea wa kujenga vituo vya kupooza umeme na *line* za kusafirisha umeme. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya mradi huo kukamilika ndani ya miezi 18, tatizo la kukatikakatika kwa umeme unaotakana na *line* ndefu kutoka Tabora Mjini mpaka Uyui mpaka kwenye Jimbo la Mheshimiwa Sitta tutakuwa tumelipunguza.

Mheshimiwa Spika, pia nimwelekeze Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Tabora ahakikishe ratiba wanazozipanga zinazingatia maeneo ambayo yanatoa huduma kwa wananchi hususan maeneo ambayo yanatoa hospitali, vituo vya afya pamoja na shule

na maeneo mengine ambayo yanatoa huduma kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura, swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Bunge la Bajeti, Serikali iliahidi kupeleka *turbine* ya megawati 20 kule Mtwara kama hatua za dharura za kupunguza tatizo la upungufu wa umeme ambalo linasababisha kukatikakatika kwa umeme; je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anastazia Wambura kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuliaahidi kupeleka hii taibai kutoka Ubungo kwenda Mtwara. Baada ya tathmini ya kina tulijirididha mtambo huu hautafanya kazi vizuri pale Mtwara. Tumeshaongea na Kampuni ya *CSI* juu ya kuzalisha umeme hapo na tumeshakamilisha, na tuna kituo cha kupoza umeme tunakijenga hiyari ambacho tunategemea kitakamilika ndani ya mwezi huu. Kikikamilika basi, umeme ambao utatolewa na Kampuni ya *CSI* utaweza kwenda kwenye Mkoa mzima wa Mtwara na Lindi na hivyo tutakuwa tumeondoa kabisa changamoto ya umeme kwa Mikoa miwili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Mtwara na Lindi watuvumilie kidogo mpaka mwishoni mwa mwezi huu tutakuwa tumekamilisha na kuwapatia umeme wa uhakika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ipo dhamira ya Serikali ya kupeleka umeme vijijini kote na umeme kufika maeneo ya mbali kabisa kutoka Mkoa wa Singida ambako ndio *sub-station* kubwa ilipo eneo la Rungwa, lakini umeme unafika ukiwa *faint* na Serikali ilikuwa na dhamira ya kujenga kito cha kupoza umeme kwa maana ya *sub-station* katika eneo la Mitundu. Je, Serikali inaanza lini kujenga kituo cha kupoza umeme Mitundu, ili kusaidia wananchi, ili waweze kujiwezesha na viwanda vidogo vidogo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Massare, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mpango huo upo, na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunatafuta fedha na pili, mchakato huo wa upatikanaji wa fedha ukikamilika basi tutaanza kujenga kituo hiki cha kupoza umeme, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuniona. Naomba kuuliza swali. Je, ratiba ya mgawo wa umeme katika Jimbo letu la Temeke umekuwa ni wa muda mrefu sana na ratiba yake haifuatilii kadiri ya ratiba zinavyokuja kwamba, umeme utakatika kuanzia muda fulani mpaka muda fulani, sasa umekuwa ni wa muda mrefu sana. Kuanzia jana mpaka leo saa hizi Temeke hatuna umeme, je, una tamko gani Waziri, ili kule Temeke waweze kutuletea umeme kulingana na mgawo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy Kilave, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, kidogo tumetengemaa kwenye suala la upatikanaji wa umeme, na kwa Mkoa wa Dar es Salaam tunafahamu maeneo mengi kwa sasahivi yanaweza yakapitisha hata siku mbili mpaka tatu bila kukatika kwa umeme. Kwa hili ambalo ambalo ameniambia Mheshimiwa Mbunge inaonekana ni suala ambalo ni *specific,* yaani ni mahususi. Naomba nilifuatilie, Mheshimiwa Mbunge, nikitoka hapa na nitakupatia majibu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlagila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, tarehe 10 Agosti, 2021 *TANESCO* na *STAMICO* waliasaini makubaliano ya kuzalisha megawati 200 kutoka kwenye Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira; je, mpango huo umefikia wapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Jumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango huu bado upo na tunautekeleza kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Kalogeris, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, nini mpango wa Serikali katika kupeleka umeme katika Shule ya Sekondari ya Tawa katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Kalogeris, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari tuna miradi ambayo inaendelea kwenye kila Mkoa kuhusiana na kupeleka umeme. Nitafuatilia kuona kama Shule ya Sekondari Tawa ipo katika mipango ambayo tunayo, na kama hamna, basi tutafanya jitihada za ziada, ili kuhakikisha Shule ya Sekondari Tawa inapatiwa umeme, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha maeneo ya uzalishaji pamoja na hoteli za kitalii kama za Mkoa wa Arusha hazipati adha ya ukatikaji wa umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Swai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeshatangulia kusema hapo awali, Serikali tunafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha tunapunguza adha ya upatikanaji wa umeme. Na kwa kadiri ya mipango hii, nimhakikishie, maeneo haya ya uzalishaji yataendelea kuendelea kupata umeme wa uhakika kwa kadiri ambavyo tunaboresha upatikanaji wa umeme. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mtakubaliana nami, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshajibu maswali mengi sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele, halafu tutaendelea na ratiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tangazo la wageni:-

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika, na tutaanza na wageni wanaotoka *Emirates Dar es Salaam,* na hawa ni Ndugu Abubakari Juma ambaye ni *Station Manager* ameambatana na mke wake, Bi. Abube, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ambao wako hapo na ni wageni wangu; kwanza ni, Waheshimiwa Wabunge tutulie, nimesimama.

Kwanza tutaanza na wageni wanaotoka *Professor Jay Foundation* ambayo taasisi hii inatarajiwa kuzinduliwa tarehe 24 Novemba, kupitia programu ya kushughulikia ama kuchangia tatizo la figo nchini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ugeni huu, sasa subirini kwanza, sijawatangaza wageni.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo leo ni mengi kidogo kwa hiyo tuukomboe wakati, sijawatangaza wageni bado. Nilikuwa naelezea kuhusu taasisi, kwa hiyo, mtapiga makofi saa ya wageni, ili tuukomboe wakati. *(Makofi)*

Kwa hiyo, taasisi hii inatarajiwa kuzinduliwa Ukumbi wa *Mlimani City* siku ya tarehe 24 Novemba, na lengo lake ni kwamba pamoja na mambo mengine, lakini wataanza na uchangishaji wa fedha kwa ajili ya kusaidia watu wenye changamoto za figo hapa nchini. Na sasa taasisi hiyo imewakilishwa hapa Bungeni leo na Ndugu

Joseph Haule, maarufu kama Profesa Jay ambaye ni Mwenyekiti wa hii taasisi, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Ameongozana na Florian Rutta ambaye ni *CEO* wa hii taasisi, karibu sana, lakini pia ameongozana na Nicholous Haule au *Black Rhino* ambaye ni Mjumbe wa Bodi. Haya, ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwa kusema hivyo mnakaribishwa sana *Mlimani City* siku ya tarehe 24 Novemba kwa ajili ya kwenda kuungana na Profesa Jay kwenye jambo hili. Na ninadhani sote tutashiriki jambo hili kikamilifu, hasa kwa kuzingatia kwamba Profesa Jay alikuwa ni Mbunge mwenzetu kipindi kilichopita, lakini pia amesimama hapo kwa ushuhuda wa namna ambavyo yeye alipata changamoto hii kwa sehemu kubwa na madaktari walijitahidi sana kuhakikisha wanampa matibabu na leo yuko hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunamshukuru Mungu kwa uponyaji wake kwako, pamoja na hayo tunakutakia kila la heri katika utendaji wa taasisi yako. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine ambao pia ni wageni wangu, ninao walimu 15 ambao walinifundisha Shule ya Msingi Mabonde, Wilayani Rungwe, wako hapa leo. Walimu mnaweza kusimama wote kwa pamoja, karibuni sana Bungeni na ahsanteni sana kwa kuja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimemaliza shule ya msingi siku nyingi kwa hiyo, mkiwaona walimu wako na afya namna hiyo ndio ile ile tunasema watu wote tungekuwa walimu tungekuwa na afya vizuri sana. Tunawatakia kila la heri, ahsanteni sana kwa kuja, lakini walimu hawa wameongozana na wanafunzi 15 ambao pia nilisoma nao Shule ya Msingi Mabonde, Wilayani Rungwe, Mkoani Mbeya. Wanafunzi wenzangu wasimame wote kwa pamoja na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ambao wanatoka Mkoa wa Tabora na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ni Mbunge ambaye ameapishwa leo hapa. Sasa wageni wake hawa wameongozwa na Ndugu Omary Mahita ambaye ni mume wake na huyu ni *IGP* Mstaafu, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ameambatana pia na watoto wa Mbunge mwenzetu, yupo Husna Mbaruk, yupo Fatma Mbaruk, yupo Sabrina Abdallah na Juliana Wasanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Anao wageni wengine ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Tabora, wanaweza kusimama wote kwa pamoja. Wageni wa Mheshimiwa Mbunge msimame wote kwa pamoja, haya ahsanteni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Wabunge wengine; tunao wageni 57 wa Spika Mstaafu, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai ambao ni *The Anglican Church of Tanzania* kutoka Kongwa, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Adolph Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, na hawa ni viongozi wa Taifa wa Umoja wa Wakuu wa Shule Tanzania kutoka Jimbo la Rombo, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambaye ni Waziri wa Afya na hawa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mipango kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Juma Aweso ambaye ni Waziri wa Maji, kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na hawa ni wachezaji…

Waheshimiwa Wabunge mnaozungumza, tafadhali tusikilizane.

Wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, na hawa ni wachezaji na viongozi wa timu ya mpira wa wavu ya wasichana, *Korosho Queens* kutoka Masasi, Mkoa wa Mtwara, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 35 wa Mheshimiwa Omari Kipanga ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, na hawa ni viongozi na Wajumbe wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Mafia, Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 39 wa Mheshimiwa Mwasi Kamani ambao wanatoka Mkoa wa Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage ambao ni viongozi wa vyama mbalimbali vya wafanyakazi kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Vita Kawawa ambao ni shemeji zake kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi, Vijana Makao Makuu, kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Mkurugenzi wa *Ritta Kabati Trust Fund* na viongozi wa Jumuiya ya Wazazi kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambao ni Kamati ya Mashindano ya *Ndondo Cup 2023* kutoka Dodoma Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Patrobass Katambi ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara; na hawa ni wafanyakazi wa majumbani na hoteli kutoka Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Dodoma. Baadhi yao ni wahitimu wa vyuo vikuu, wameambatana na viongozi wao na wafadhili wa Mradi wa Kuendeleza Wafanyakazi wa Majumbani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Muharami Mkenge ambao ni watumishi wa Shule ya Sekondari Bagamoyo kutoka Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Dennis Londo ambao ni walimu wa shule ya Lyahira, Kata ya Ruaha kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Boniphace Getere kutoka Dar es Salaam, karubuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Shally Raymond kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Agnes Marwa kutoka Mkoa wa Mara, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambao ni walimu na wataalam wa mazingira kutoka Sikonge, Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ramadhan Ighondo kutoka Singida, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza ni Ndugu Abednego Salalila ambaye ni Mwandishi wa Makala ya Kuelimisha Jamii kutoka Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano kutoka *Disabled Mama Africa,* karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, iko Miongozo iliyoombwa hapa ndani na tunayo miongozo minne. Kwa hiyo, nitaisoma kwa ufupi, halafu itaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kama sehemu ya maamuzi yetu hapa Bungeni.

Tutaanza na Mwongozo uliokuwa umeombwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kuhusu lugha iliyotumika na Mheshimiwa Riziki Lulida kuhusu wafugaji.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya tarehe 7 Novemba, 2023 katika Kikao cha Saba cha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kuhusu lugha iliyotumiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida wakati akimpa Taarifa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau alipokuwa akichangia Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Nimezipitia Taarifa Rasmi za Bunge na Mwongozo uliokuwa umeombwa ni kuhusu mchango wa Mheshimiwa Riziki Lulida ambapo wakati akitoa Taarifa ile kwa Mheshimiwa Olelekaita alitumia maneno ambayo yaliashiria, kwa namna alivyokuwa ameyaelewa Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba ni kama yanawajumuisha wafugaji wote kama wauaji.

Sasa baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge kutazama mchango wa Mheshimiwa Olelekaita na taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Lulida, nimejiridhisha kwamba maneno yaliyokuwa yametumika yangeweza kusababisha taharuki kama vile wafugaji wote ni wauaji.

Kwa hivyo, Mwongozo unaotolewa kuhusu alichotaka kujua Mheshimiwa Ole-Sendeka kama kinaruhusiwa ama hakiruhusiwi hapa Bungeni, hakiruhusiwi na hivyo, Mwongozo huu unaondoa maneno hayo ambayo aliyasema Mheshimiwa Riziki Lulida ambayo yalikuwa yanaashiria kwamba wafugaji wote ni wauaji. *(Makofi)*

Hakutumia neno wote, lakini kwa namna alivyoisema sentensi yake, ilisababisha kundi la wafugaji wangeweza kujiona kama wote wanatuhumiwa kwa pamoja. Kwa hiyo, ni baadhi ya wafugaji ambao wamefanya mambo hayo na taratibu za kisheria inabidi zifuate.

Kwa hiyo, huo ndio Mwongozo, maneno yaliyokuwa yametumika hayaruhusiwi kutumika hapa Bungeni na kwa hivyo, yanaondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA ULIOOMBWA NA MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA (MB) KUHUSU LUGHA ILIYOTUMIWA NA MHE. RIZIKI S. LULIDA (MB) KUHUSU WAFUGAJI – KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Waheshimiwa Wabunge**, tarehe 07 Novemba, 2023 katika Kikao cha Saba cha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Mhe. Christopher Ole Sendeka Mbunge wa Jimbo la Simanjiro aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 kuhusu lugha iliyotumiwa na Mhe. Riziki S. Lulida (MB) wakati akimpa taarifa Mhe. Edward Kisau Ole Lekaita (MB) alipokuwa akichangia Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Waheshimiwa Wabunge,** Katika mwongozo wake, Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka (MB) alieleza yafuatayo, ninanukuu:

> "…………*mheshimiwa Lulida akisema na akieleza jinsi ambavyo wafugaji wameenda mpaka huko kusini na akasema kuna wafugaji ambao wamekuwa wanaua watu. Sasa lugha*

*ya wafugaji wanaua watu, wafugaji bila shaka pia ni watu nina hakika, ni kupanda mbegu ya uhasama kati ya wafugaji waonekane ni watu wa hatari katika nchi hii, bila shaka anayeua atakuwa ni mtu mwenye jina lake mahsusi, na kama akiua mtu ambaye ni wa jamii ya kifugaji ni mtu sio wafugaji wameua……..*".

**Waheshimiwa Wabunge**, Mhe. Christopher Ole Sendeke (MB) aliendelea kueleza kuwa, ninanukuu:

"*Mheshimiwa mwenyekiti, kama unakubaliana na mimi, kauli hiyo siyo sahihi kutumika katika Bunge hili*" (***Mwisho wa Kunukuu***).

**Waheshimiwa wabunge**, kutokana na mwongozo huo, niliwaeleza kuwa nitarejea kwenye Taarifa Rasmi za Bunge halafu nitatoa Mwongozo wangu kwa mujibu wa Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.

**Waheshimiwa Wabunge**, nimepitia Taarifa Rasmi za Kumbukumbu za Bunge kama nilivyowaeleza ili kujiridhisha juu ya lugha iliyotumiwa na Mhe. Riziki Lulida (MB) ambayo ililalamikiwa na Mhe. Christopher Ole Sendeka (MB). Mhe. Sendeka aliomba Mwongozo akitaka kujua kama lugha hiyo inaruhusiwa kutumika hapa Bungeni au hapana.

**Waheshimiwa Wabunge,** kwa kurejea Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard),* Mhe. Riziki Lulida (MB) wakati wa kutoa Taarifa kwa Mhe. Edward Kisau Ole Lekaita (MB) alieleza yafuatayo, ninankuu:

"*…..kuna sheria na kuna mipaka ilishatengenezwa, corridor za wanyamapori na binadamu, **lakini vilevile hawa wafugaji leo wapo katika Mkoa wa Lindi na vurugu za wafugaji, kuvamia maeneo na mashamba ya wananchi imekuwa kubwa mpaka wananchi wameuawa na wafugaji, tusiendelee kukubali vitu ambavyo havitaki kufuata sheria**. Twende na sheria, Serikali ina*

*sheria yake na wafugaji watii sheria ya nchi hii*". (**Mwisho wa Kunukuu**)

**Waheshimiwa Wabunge**, kama nilivyoeleza na kunukuu Mwongozo uliombwa na Mhe. Christopher Ole Sendeka ambaye alilalamikia lugha iliyotumiwa na Mhe. Riziki S. Lulida. Mhe. Sendeka alidai kuwa Mhe. Riziki S. Lulida (MB) alitumia lugha ya jumla kwa kudai kuwa wafugaji wanaua wananchi katika Mkoa wa Lindi. Mhe. Sendeka alieleza zaidi kuwa suala la kuua mtu au watu siyo la wafugaji bali lazima liwe ni la mtu mahsusi ambaye anapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria yeye binafsi. Jambo hili haliwezi kuwa ni la wafugaji kwa ujumla wao, hata kama mhusika huyo atakuwa anatokea jamii ya wafugaji. Mhe. Christopher (MB) alienda mbali zaidi na kueleza kuwa kusema wafugaji ndiyo wauaji, ni kupanda mbegu ya chuki na uhasama katika jamii ili wamasai waonekane kuwa ni watu wa hatari katika nchi hii.

**Waheshimiwa Wabunge**, Kanuni ya 71 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 inataja mambo mbalimbali yasiyoruhusiwa Bungeni. Mojawapo ya mambo hayo kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni ya 71(1)(j) kuwa ni "**Mbunge kutotumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine**".

**Waheshimiwa Wabunge**, ni ukweli kwamba kutoa uhai wa mtu ni mojawapo ya makosa makubwa ya jinai hapa nchini. Adhabu ya mtu anayepatikana na hatia ya kufanya kitendo hicho ni kunyongwa hadi kufa kwa mujibu wa Kifungu cha 196 na 197 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16. Kwa hiyo basi, kosa la kuua hutekelezwa na mtu binafsi na siyo jamii ya watu fulani au kabila fulani. Kwa maana hiyo, kosa la kuua hutekelezwa na mtu binafsi na halihusiani na kabila la mtu, jamii anayotokea au kundi fulani la watu.

**Waheshimiwa Wabunge**, kwa kuwa Mheshimiwa Riziki S. Lulida (MB) alieleza katika sehemu ya taarifa yake kuwa "…***wananchi wameuawa na wafugaji, tusiendelee kukubali vitu ambavyo***

***havitaki kufuata sheria".*** Maneno yake yanaleta taswira kuwa wafugaji ni watu wenye vurugu, wauaji na wasiofuata sheria. Kwa namna ilivyotumika, lugha hii inawajumuisha wafugaji wote yaani wanaofuata sheria na wasiofuata sheria. Kauli hii ni kinyume na masharti ya Kanuni ya 71(1)(j) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 niliyoielezea hivi punde.

Ni wazi kuwa, kwa kuwa lugha iliyotumiwa na Mhe. Riziki Lulida (MB) inakiuka kanuni zetu hivyo hairuhusiwi hapa bungeni. Kwa maelezo hayo, naelekeza maneno hayo yaondolewe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Kwa kuhitimisha, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, tuendelee kutumia lugha inayokubalika katika michango yetu ili kuepusha migogoro ya tafsiri katika jamii yetu.

Huo ndiyo Mwongozo wangu.

Umetolewa tarehe 09 Novemba, 2023

Mhe. Dkt. Tulia Ackson (MB)
**SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo mwingine uliombwa na Mheshimiwa Innocent Kalogeris kuhusu Swali lake Namba 101 kutojibiwa kikamilifu. Mtakumbuka tulishapata kutoa mwongozo hapa Bungeni kuhusu maswali kutokujibiwa kikamilifu na tulisema anayeruhusiwa kuomba swali lake lijibiwe kikamilifu ni yule mwenye swali la msingi. Na katika mazingira haya Mheshimiwa Innocent Kalogeris alikuwa ndiye mwenye swali la msingi na katika maswali yake mawili ya Nyongeza, mojawapo alisema halijajibiwa kikamilifu.

Sasa nimepitia Taarifa Rasmi za Bunge, namna alivyouliza swali lake Mheshimiwa Innocent Kalogeris na namna Mheshimiwa Naibu Waziri alivyolijibu lile swali alikuwa sahihi. *(Makofi)*

Sasa nimepitia Taarifa Rasmi za Bunge, namna alivyouliza swali lake Mheshimiwa Innocent Kalogeris na namna Mheshimiwa Naibu Waziri alivyolijibu lile swali alikuwa sahihi. Kwa hiyo, Serikali kwenye swali lake la kwanza la nyongeza ilivyojibu ilikuwa imejibu kwa kadiri alivyohitaji majibu yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo nimeletewa taarifa hapa kwamba aliyoyaeleza Mheshimiwa Innocent Kalogeris wakati akiomba Mwongozo yalikuwa sahihi. Swali lake lilijibiwa kikamilifu, lakini aliomba Mwongozo kwa sababu yeye alikuwa na taarifa za ziada ambazo alikuwa anaona Serikali haijazifanyia kazi. Sasa, nimeletewa taarifa kwamba, alichokisema wakati akiomba Mwongozo kuhusu yeye kupeleka barua kwa Mkuu wa Wilaya, alikuwa kweli ameshafanya hilo zoezi la kupeleka barua na majibu yamechukua muda mrefu, ndiyo maana akaona aseme hapa ili apate majibu ya Serikali, kwa nini barua zake hazijibiwi. *(Makofi)*

Sasa, kwa sababu wakati wa kutoa ule Mwongozo alitoa hayo maelezo na Serikali imeshaanza kufUatilia, kwa sababu Serikali ndiyo iliyoniletea taarifa hapa kwamba ni kweli Mheshimiwa Mbunge alipeleka barua. Basi Mwongozo ni kwamba, swali lilijibiwa kikamilifu lakini hii sehemu ya pili ambayo si sehemu ya Mwongozo ni kwamba, tunatoa wito kwa Serikali, kwamba, Waheshimiwa Wabunge wanapoleta malalamiko kwenu muweze kuyafanyia kazi kwa wakati, kwa sababu hawa ni wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo, kama kuna jambo Mbunge amelisema ni vizuri lifuatiliwe kwa haraka ili lisichukue muda mpaka linakuja hapa ndani. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA ULIOOMBWA NA MHE. INNOCENT E. KALOGERIS (MB) KUHUSU SWALI LAKE NA. 101 KUTOJIBIWA KIKAMILIFU – KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Waheshimiwa Wabunge,** Tarehe 07 Novemba, 2023 katika Kikao cha Saba cha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Mhe. Innocent E. Kalogeris, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kuhusu Swali lake la Nyongeza katika Swali lake la Msingi Namba 101 kutojibiwa kikamilifu.

**Waheshimiwa Wabunge,** Wakati akiomba mwongozo huo, Mhe. Kalogeris alieleza yafuatayo:

> ***"Mheshimiwa mwenyekiti, katika swali langu la msingi 101. katika majibu ya serikali kwenye swali la nyongeza sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu hayo maeneo yote aliyosema kwa DC, nimeandika barua kama Mbunge na ofisi yangu ya Bunge kulalamika suala hilo. Vilevile, nimeenda kumfuata Msajili wa Mahakama aliyekuwa Ndg.Kaida na kutoa taarifa. Mheshimiwa Mwenyekiti sasa nilikuwa nataka nipate Mwongozo wako, ninapoambiwa kwamba niandike barua sasa naandika barua wakati gani?"***

**Waheshimiwa Wabunge,** nimepitia Taarifa Rasmi za Bunge ambazo zinaonesha kuwa, wakati wa kipindi cha maswali na majibu Mhe. Innocent E. Kalogeris (Mb) aliuliza swali la msingi Na. 101 kwa Wizara ya Katiba na Sheria. Baada ya Swali la Msingi kujibiwa, Mhe. Kalogeris aliuza maswali mawili ya nyongeza na maswali hayo yalijibiwa. Swali la Kwanza la nyongeza linalohusu Mwongozo huu lilikuwa kama ifuatavyo: -

> ***"Mhe. Mwenyekiti, katika Tarafa ya Bwakira Chini kuna Hakimu ambaye anaitwa Deogratius Amatungiro ni hakimu ambaye amegeuza Mahakama kama duka la kuuza haki kwa wananchi kiasi ambacho wananchi wa Tarafa ya Bwakira Chini wamemchoka. Je Mheshimiwa Waziri uko tayari kwenda na mimi katika Kata ya Bwakira Chini, Kata ya Kisaki na Kata ya Ngazi ambayo ndiyo Tarafa ya Bwakira ukasikilize malalamiko ya wananchi? kwa sababu viongozi mbalimbali wamepita lakini hakuna hatua yoyote ambayo imechukuliwa ili yeye kama msimamizi au ndiyo msimamizi katika Mahakama na***

***Wizara ya Sheria uondoke nae huyo Hakimu kwa sababu tumemchoka."***

**Waheshimiwa Wabunge,** Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu Swali hilo kama ifuatavyo:- (nanukuu)-

> ***"…Mhe. Mwenyekiti, Swali lake la Kwanza amemlalamikia Mheshimiwa Hakimu katika Mahakama hii ya Bwakira ambayo tunakwenda kujenga japo inaendelea katika eneo la godown. Naomba nimuelekeze Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wenzangu kwamba, tuna Kamati zetu za Maadili kwa Maafisa wa Mahakama na Wenyeviti wa Kamati hizi ni ma-DC wetu katika wilaya zetu lakini na Waheshimiwa ma-RC. Kwa hiyo, Mheshimiwa Innocent kwa kuwa Kanuni zetu zinatuhitaji kama kuna malalamiko yoyote kwa maafisa wetu wa Mahakama tunapaswa kuandika kwa maandishi. Nikuombe uandike kwa maandishi umpelekee Mheshimiwa DC wa Morogoro ili Kamati ya Maadili ya Maafisa wa Mahakama katika Wilaya yako sasa waanze uchunguzi kama kuna tuhuma zitakuwa zimethibitika basi hatua zitachukuliwa."***

**Waheshimiwa Wabunge**, Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 zinaweka masharti kwa Mawaziri kujibu maswali Kikamilifu. Katika kujibu swali hili, Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza taratibu za kufuata ili kuwasilisha malalamiko dhidi ya maafisa wa Mahakama ikiwemo Mahakimu kuwa ni kupitia Kamati za Maadili za eneo husika ambapo Wakuu wa Mikoa na Wilaya ni Wenyeviti wa Kamati hizo. Aidha, Mheshimiwa Waziri alifafanua kuwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni endapo kuna malalamiko dhidi ya Hakimu Mheshimiwa Mbunge anapaswa kuyawasilisha kwa maandishi na kwa Mheshimiwa DC wa Morogoro ili Kamati ya Maadili katika Wilaya hiyo waanze uchunguzi na kama tuhuma zitathibitika basi hatua zitachukuliwa.

**Waheshimiwa Wabunge**, Baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge na kutafakari majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria maswali ya nyongeza na nimejiridhisha kuwa Swali

hilo la Kwanza la nyongeza la Mhe Innocent Kalogeris lilijibiwa kikamilifu.

**Waheshimiwa Wabunge,** katika maombi ya Mwongozo wa Mhe. Kalogeris (Mb) ametaja jambo jipya ambalo halikuwemo kwenye maswali yake ya nyongeza. Jambo lenyewe ni kuwa, malalamiko yake dhidi ya Mhe. Hakimu aliyafikisha kwa Mkuu wa Wilaya kwa njia ya barua lakini hayajapatiwa ufumbuzi. Suala hili halikuzungumziwa na Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa maswali aliyoulizwa hayakuzungumza chochote kuhusu Mhe. Kalogeris (Mb) kuandika barua kwa Mkuu wa Wilaya. Katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alijikita katika kutoa ufafanuzi wa utaratibu unaopaswa kuzingatiwa katika kuwasilisha malalamiko dhidi ya Hakimu anayeonekana kukiuka maadili ya kazi yake.

**Waheshimiwa Wabunge,** mwongozo ulitaka kujua ni wakati gani Mhe. Kalogeris (Mb) aandike barua ya malalamiko? Swali hilo lilitokana na maelezo yake kwamba alishaandika barua nyingine hapo awali kwenda kwa Mkuu wa Wilaya. Mwongozo wangu katika suala hili ni kuwa iwapo Mhe. Kalogeris (Mb) alishapeleka barua za malalamiko kwa Mkuu wa Wilaya ni vema afuatilie majibu yake na iwapo ataona inafaa anaweza kuwasilisha upya barua ya malalamiko kama ilivyofafanuliwa na Mhe. Naibu Waziri ili malalamiko hayo yapatiwe ufumbuzi.

Huo ndiyo Mwongozo wangu.

Umetolewa leo tarehe 09 Novemba, 2023
Mhe. Dkt. Tulia Ackson (MB)
**SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo mwingine ulikuwa umeombwa na Mheshimiwa Phillipo Mulugo, kuhusu Mawaziri kutumia simu wakati mjadala unaendelea hapa Bungeni. Mwongozo huu uliombwa siku ya tarehe 3, tulikuwa tunajadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*, kwa hiyo

akataka kujua kama inaruhusiwa kuendelea kutumia simu badala ya kusikiliza Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, katika Mwongozo huu pamoja na kupitia Taarifa Rasmi za Bunge, lakini pia na picha zile zilizoko, kwa sababu aina ya Mwongozo ulioombwa ulikuwa unataka siyo tu upitie Taarifa Rasmi za Bunge, kwa sababu kama Waziri ama Naibu Waziri anatumia simu, huwezi kuliona hilo kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Tumetazama Kanuni zetu, Kanuni ya 73(3)(d) na (e) inazungumza kuhusu Mbunge ambaye yuko Bungeni kwamba; atatakiwa:-

(d) Kutokusoma kitabu chochote, gazeti au barua isipokuwa kama vitu hivyo vinahusu Shughuli za mjadala unaoendelea wakati huo.

(e) Kuondoa mlio wa simu na kutozungumza na simu.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Kanuni hiyo tuliyoitaja hapo juu ni kwamba, haijazuia Mbunge kusoma ujumbe katika simu yake unaohusu mjadala unaoendelea Bungeni. Hata Mwongozo huo wa Mheshimiwa Mulugo ulivyoombwa, hakuna uthibitisho. Hatujaweza kupata uthibitisho kwamba kuna Waziri aliyekuwa anasoma pengine ujumbe kwenye simu ambao hauhusiani na mjadala uliokuwa unaendelea hapa. *(Makofi)*

Kwa mazingira hayo, tufuate tu utaratibu wa Kanuni zetu. Hairuhusiwi kuzungumza na simu humu Bungeni, lakini Wabunge mnaruhusiwa kupitia jumbe za simu zenu zile zinazohusu mjadala ulio hapa Mezani. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA ULIOOMBWA NA MHE. PHILLIPO A. MULUGO (MB) KUHUSU MAWAZIRI KUTUMIA SIMU WAKATI MJADALA UNAENDELEA

## TAREHE 3 NOVEMBA, 2023 – KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI

**Waheshimiwa Wabunge,** Tarehe 3 Novemba, 2023 katika Kikao cha Nne cha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Mheshimiwa Phillipo A. Mulugo, Mbunge wa Jimbo la Songwe, aliomba Mwongozo wa Spika kuhusu mawaziri kutumia simu wakati mjadala unaendelea. Sehemu ya maneno ya Mhe. Mulugo ni kama ifuatavyo: -

***"Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge wa Chama cha Mapinduzi moyo unaniuma, Mbunge mwenzetu anapochangia taarifa kama hii, inaniuma kuona wanaohusika, mawaziri wana-chat na simu, wanaongea na simu, hawajali kile ambacho anakiongea Mheshimiwa Waitara kama vile ni jambo linapita. Mimi binafsi inaniuma sana, naomba Mwongozo wako."***

**Waheshimiwa Wabunge**, katika kutafakari maombi hayo ya Mwongozo, swali nililojiuliza na ambalo linapaswa kutolewa Mwongozo ni Je, kweli Mawaziri walikuwa wana-chat na simu, wanaongea na simu na hawajali kile ambacho Mheshimiwa Waitara alikuwa anaongea?

**Waheshimiwa Wabunge**, kwa mujibu wa Kanuni ya 73(3)(d) na (e) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inaeleza kwamba Mbunge aliyepo Bungeni wakati wa mjadala atatakiwa: -

(d) kutosoma kitabu chochote, gazeti au barua, isipokuwa kama vitu hivyo vinahusu shughuli za mjadala unaoendelea wakati huo; na
(e) kuondoa mlio wa simu na kutozungumza na simu.

**Waheshimiwa Wabunge**, kwa kuzingatia kanuni tajwa hapo juu hazijazuia Mbunge kusoma ujumbe katika simu yake unaohusu mjadala unaoendelea Bungeni. Aidha, hata katika Mwongozo wa Mheshimiwa Mulugo hakuna uthibitisho unaoonesha kuwa Mawaziri walikuwa wanaongea na simu.

Huo ndiyo Mwongozo wa Spika.

Umetolewa leo tarehe 9 Novemba, 2023

Mhe. Dkt. Tulia Ackson (MB)
**SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wa mwisho kwa siku ya leo uliokuwa umeombwa hapo kabla, ni Mwongozo uliokuwa umeombwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka tena. Huu alikuwa ameomba siku ya tarehe 3 Novemba, 2023 na ulikuwa unahusu maneno ambayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora alikuwa ameyatumia hapa Bungeni, wakati Mbunge mmojawapo akiwa anachangia, kuashiria kwamba Waheshimiwa Wabunge sisi wote tunapaswa kuwajibika kwenye yale ambayo yalikuwa yamesemwa kwenye Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Ole-Sendeka aliomba Mwongozo kwa maana ya kwamba yale maneno yaliyokuwa yametumiwa na Mheshimiwa Waziri yalikuwa yanaashiria kama vile Wabunge ni sehemu ya ule ubadhirifu au matumizi mabaya ya fedha kwenye halmashauri, kwa kuwa tu wao ni Madiwani.

Waheshimiwa Wabunge, tulipata nafasi ya kuzipitia Taarifa Rasmi za Bunge na muktadha ambao Mbunge alikuwa anachangia na akapewa taarifa na Mheshimiwa Waziri na baadaye ukaombwa Mwongozo, tumejiridhisha kwamba maneno yaliyokuwa yametumiwa na Mheshimiwa Waziri yangeweza kwa namna moja ama nyingine kuathiri Ibara ya 100 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inampa uhuru Mheshimiwa Mbunge kuchangia humu ndani na michango yake kulindwa kwa namna hiyo, kwa maana uhuru wa kuchangia.

Pamoja na hayo, tulijaribu kutazama na muktadha mzima wa jambo hili na namna Waheshimiwa Wabunge wanavyoshiriki shughuli za halmashauri. Hata wakati mwingine hata sisi Waheshimiwa Wabunge, huwa wakati mwingine tunachangia kwa namna inayoashiria kwamba Waheshimiwa Madiwani pengine ama taarifa wakati mwingine zinazotolewa kutoka kwenye halmashauri kwamba pengine usimamizi hauko vizuri.

Sasa kule huwa kuna wataalam na ndiyo wanafanya hizi kazi kila wakati na Waheshimiwa Wabunge. Siyo kwa sababu hamshiriki vikao kule, ni kwa sababu ninyi ni Wabunge na mnashiriki vikao hapa. Kwa hiyo, ratiba zikiingiliana hii ni kazi yako ya msingi, inabidi uifanye ile iliyo ya msingi. Ninavyosema ya msingi siyo kwamba ile nyingine siyo ya muhimu. Zote ni za muhimu lakini kata za kwenye jimbo lako zinao Madiwani na ndiyo wawakilishi. Kwa hiyo, wanaenda kuwakilisha kwenye halmashauri na wewe kama unayo ya Bunge na ya halmashauri, inabidi uende kwenye ile ambayo kwako ni ya msingi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa mazingira hayo maneno yale yaliyotumika na Mheshimiwa Waziri tumejiridhisha kwamba yangeweza kwa namna moja au nyingine kuzuia Waheshimiwa Wabunge kuchangia kwenye hoja ambazo zinatoka kwenye majimbo yao ama halmashauri zao. Kwa hiyo, Mwongozo ni kwamba, yale maneno yaliyokuwa yametumika ambayo kama nilivyosema hii Miongozo itaingia kama ilivyo kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, maneno hayo yataondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge ili tuendelee kulinda uhuru wa Waheshimiwa Wabunge kuweza kuisimamia Serikali kwenye ngazi zote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Miongozo hiyo minne anayetaka kuisoma ataikuta kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kwa ukamilifu wake, kwa namna nilivyoisema hapa kwa kifupi kwa ajili ya kukomboa muda, maana Wabunge wengi mnataka kuchangia hoja iliyopo mbele yetu lakini kuna mambo ambayo tuliyaahirisha

hapo nyuma nataka niyafanyie kazi sasa, halafu tuendelee na ratiba.

## MWONGOZO WA SPIKA ULIOOMBWA NA MHESHIMIWA CHRISTOPHER OLE SENDEKA (MB) KUHUSU MANENO YALIYOTUMIWA NA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA TAREHE 3 NOVEMBA, 2023 – KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI

Waheshimiwa Wabunge, mnamo tarehe 3 Novemba, 2023 wakati wa mjadala kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* katika Kikao cha Nne cha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Mhe. Christopher Ole Sendeka (Mb), alisimama na kuomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Mwongozo huo ulihusu maneno yaliyotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb). Maneno hayo ya Mhe. Waziri ni kama ifuatavyo:

***"…kwa mujibu wa sheria zetu za fedha za local government, sisi tuliopo humu ndani ni wajumbe wa Kamati ya Fedha za Halmashauri za Serikali za Mitaa na kwa hiyo, mapungufu yote yanayotokea kule. Hata sisi humu ndani ni sehemu yake…hatuwezi kutenganisha ni lazima wote tuwajibike. Haya yote yanatokea leo wote tunawajibika"***

**Waheshimiwa Wabunge**, katika maombi ya Mwongozo pamoja na mambo mengine Mheshimiwa Sendeka alieleza: (nanukuu)

> ***''…nimesimama chini ya Kanuni ya 76 kuomba mwongozo wako kwa kauli ya waziri wa nchi rafiki yangu ninayemheshimu sana comrade Simbachawene kuhusu kuwahusisha wabunge kwa vitendo vya wabunge kuwa wajumbe wa mabaraza ya Madiwani kusema kwamba sisi ni sehemu ya uhalifu huo wa dhidi ya rasilimali za nchi unaoendelea katika Halmashauri zetu…maafisa masuuli katika Halmashauri ni wakurugenzi watendaji, wana wasaidizi wao hapo chini hao ndio***

> ***wanakaguliwa. Kama kuna jambo ambalo madiwani wamepitisha kinyume cha sheria itatamkwa kwamba tumepata hasara hii kutokana na maamuzi ya madiwani iliyokiuka sheria. Kwa ripoti tuliyonayo leo sijaona mahali paliposema madiwani wa Halmashauri fulani wamelazimisha fedha ziende katika eneo lingine…. nilitaka kulinda heshima ya Bunge hili katika uhalisia sio kwa maana ya kufunika. Bunge hili sio sehemu ya uhallifu katika ripoti ya CAG …nataka kuomba mwongozo wako kama jambo hili sisi ni sehemu.''*** *(*mwisho wa kunukuu*)*.

**Waheshimiwa Wabunge,** baada ya kuomba mwongozo huo kiti kiliahidi kutoa mwongozo huo baadaye.

**Waheshimiwa Wabunge,** hakuna ubishi kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wabunge wa majimbo ni Madiwani na ni wajumbe wa Kamati za Fedha katika Halmashauri zao nchini. Hata hivyo baada ya kupitia taarifa ya *CAG* haijaonesha kuwa Wabunge walihusika katika mapungufu yaliyoainishwa katika taarifa hiyo.

**Waheshimiwa Wabunge,** Ibara ya 100 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa haki na uhuru kwa Wabunge kujadili jambo lolote ndani ya Bunge na kwamba haitakuwa haki, uhuru wa majadiliano hayo kuvunjwa au kuhojiwa. Ibara hiyo inaeleza kama ifuatavyo: (nanukuu)

> ***''Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano, au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge.''*** (Mwisho wa kunukuu)

Hivyo kwa mujibu wa Ibara hiyo Wabunge wana haki ya kujadili taarifa ya *CAG* katika kutimiza wajibu wao chini ya Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Waheshimiwa Wabunge**, maneno yaliyotumiwa na Mheshimiwa Waziri yanakinzana na masharti ya Ibara ya 100 (1) ya Katiba kwa sababu yanagusa moja kwa moja uhuru wa majadiliano na mijadala ndani ya Bunge. Iwapo maneno hayo yataachwa kwenye *Hansard* yatakuwa yanaashiria kwamba Wabunge wanahusika katika mapungufu yaliyomo katika taarifa ya *CAG*, kwa hiyo hawana haki ya kujadili taarifa hiyo, jambo ambalo linaathiri uhuru wa majadiliano. Hii ni kwa sababu Kanuni za haki za asili ***(principles of natural justice)*** zinaeleza kwamba mtu hawezi kuwa Hakimu katika shauri linalomhusu (***one cannot be a judge of his own cause)***.

**Waheshimiwa Wabunge,** kutokana na kasoro hiyo maneno hayo hayafai kuendelea kuwepo kwenye Kumbukumbu za Bunge, hivyo, naelekeza maneno "***kwa hiyo, mapungufu yote yanayotokea kule. Hata sisi humu ndani ni sehemu yake…hatuwezi kutenganisha ni lazima wote tuwajibike. Haya yote yanatokea leo wote tunawajibika"*** yafutwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Huo ndio Mwongozo wangu.

Umetolewa leo tarehe 9 Novemba, 2023

Mhe. Dkt. Tulia Ackson (MB)
**SPIKA**

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Haya. Waheshimiwa Wabunge wawili wamesimama wakiomba Miongozo. Mheshimiwa Aida Khenani.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 76, jambo ambalo limetokea Bungeni na kwa ajili ya muda naomba nisiisome.

Kulingana na ugeni mbao ulikuwa unatambulisha, umemtambulisha aliyekuwa Mbunge mwenzetu Joseph Haule, maarufu kama Profesa Jay. Kwa kutambua kazi kubwa ambayo ameifanya Mheshimiwa Rais, Wizara yenyewe ya Afya lakini kwa kumshukuru Mungu kumfikisha hatua hii aliyonayo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa kutambua majukumu makubwa waliyonayo Waheshimiwa Wabunge, kama itakupendeza na itawapendeza Waheshimiwa Wabunge, basi angalau tutoe Sh.50,000/= kwa kila mtu kwa kutambua umuhimu na changamoto iliyopo kwa huu ugonjwa wa figo kwa wananchi wetu na hili jambo ambalo limeanzishwa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, kwa sababu umesimama kuhusu Mwongozo, ni lipi kati ya hayo unataka kujua kama linaruhusiwa au haliruhusiwi humu Bungeni? Ili nijue namna ya kujielekeza vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, kumchangia kama inaruhusiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimesimama kwa Kanuni hiyo hiyo. Ni kweli tumekuwa na ugeni humu ndani kama ulivyokuwa ukitambulisha na Profesa Jay amekuwa Mbunge mwenzetu humu ndani na tumefanya naye kazi, amelisaidia Taifa kwa muda wa miaka mitano, lakini na yeye ameshiriki majanga mengi ambayo watu wengi walikuja hamu ndani Bunge tukapitisha Azimio la kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, kwa hali hiyo na kwa muktadha kwamba umetangaza atakuwa na uzinduzi wa *foundation*, siyo Wabunge wote tutaweza kwenda Dar es Salaam. Wengine hatuna nauli. Ushauri wangu naomba kwako kama linaruhusiwa, napendekeza kulingana na hali yake yeye mwenyewe alivyo Mbunge mwenzetu na sisi wote humu tunaweza kupita kwenye hiyo hali, tumchangie shilingi laki mbili. Kwa maana hii; laki moja apewe yeye mwenyewe, lakini laki moja iende kwenye *Foundation* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kama linaungwa mkono, kama utaruhusu tuendelee. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa makofi mliyopiga yanaashiria kwamba, hamjapiga wote lakini kwa makofi yaliyopigwa, yamepigwa mengi mengi. Yale makofi yanaashiria kwamba hoja ya kumchangia Profesa J tunaiunga mkono. Hata hivyo, kwa kuwa sote tuko hapa ndani na uamuzi wa namna hii ulishawahi kutoka huko nyuma na nisingependa kurejea kwenye maeneo ambayo nilishatoa uamuzi wa aina hii, wasaidizi wetu wako hapa ndani na kwa hivyo kuna pendekezo limetoka la kuhusu kiasi pia. *(Makofi)*

Kwanza, ni hoja halafu limetoka pendekezo la kiasi, lakini kiasi kwa sababu humu ndani pia kuna utofauti wetu, napenda kila mmoja atoe kwa kadiri yeye anavyoweza. Kwa sababu, wengine wanaweza kutoa zaidi ya hapo ikamsaidia zaidi. Kwa hiyo, kwa nia ile ile ambayo mmepiga makofi humu ndani, nawaruhusu hawa wasaidizi wapite huko wakusanye hiyo michango kati ya leo na kesho, halafu atakabidhiwa michango mtakayochanga. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge, Miongozo yote miwili ilikuwa inahusu jambo moja.

Sasa tusikilizane kidogo pamoja na kwamba nimekaa ili twende kwa pamoja. Kuna wageni ambao wametangazwa hapa ndani nimeletewa marekebisho ya utambulisho wao.

Wale waliokuwa wametambulishwa kama wageni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, walitambulishwa kwamba wanatokea Rombo. Hawa hawatoki Rombo lakini ni Viongozi wa Umoja wa Wakuu wa Shule Tanzania, wakiongozwa na Rais wa Umoja wa Wakuu wa Shule, Ndugu Dennis Otieno ambaye ni Mkuu wa Shule ya Sekondari Ilboru. Kwa hiyo, Taarifa Rasmi za Bunge zitasomeka kwa namna hii. *(Makofi)*

Nimeletewa pia marekebisho kuhusu wageni 29 wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani. Hawa ni Wajumbe wa Baraza Kuu, Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo. Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo.

Wageni 29 wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ni Wajumbe wa Baraza Kuu UVCCM, Mkoa wa Mwanza, kutoka wilaya zote saba za mkoa. Karibuni sana, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumamosi wakati nikiahirisha Bunge, kuna hoja hapa nilikuwa nimeziahirisha, zingine tumeshazifanyia kazi na ilikuwa bado hoja ya Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro. Sasa nampa dakika tatu aseme jambo lake halafu tulimalize.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maelezo yangu kuhusiana na jambo ambalo niliongea wakati nachangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo mwaka 2024/2025. Jambo lenyewe linahusiana na ng'ombe 806, kondoo 420 na mbuzi 100 ambao walitaifishwa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limeleta utata mkubwa sana. Jambo lenyewe, mifugo ilikamatwa tarehe 26 Oktoba, kwenye eneo

linaloitwa Olkimbai, Kijiji cha Kistalo. Ng'ombe hao walikamatwa muda wa saa 8.30 mchana na maaskari wa *TANAPA* kwa maana ya Hifadhi ya Serengeti, wakiwa wanachungwa na vijana watano kutoka katika vijiji.

Mheshimiwa Spika, Kwenye ukurasa wa kwanza wa taarifa yangu nimewaorodhesha kwa sababu ya muda. Askari wale waliswaga wale ng'ombe pamoja na wale vijana wakawaweka chini ya ulinzi na kuwapeleka mpaka kwenye eneo la Olobo, Hifadhi ya Serengeti. Baada ya kuwafikisha kule waliwaambia kwamba wajenge boma kwa ajili ya kuweka wale ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, tarehe 27, viongozi pamoja na wenye mifugo walienda hifadhini kwa ajili ya kuulizia mifugo yao. Walipofika hifadhini walizuiwa kuingia. Walikaa mpaka muda wa saa nane kuelekea saa tisa ndiyo wakaruhusiwa. Waliingia kwa kibali Na. *TNP/SEKL/00304433* na waliingia hifadhini kwa gari Na. *T241BC*. Baada ya viongozi kuingia wakakutana na Mhifadhi mmoja anaitwa Shayo, wakaenda wakaangalia ngombe wao, wakawaambia tunaomba tuhesabu, walikatazwa kuhesabu ng'ombe. Wakarudi wakawaambia tunaomba basi namna ya kuweza kulipia hawa ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, Bwana Shayo ambaye kwenye ukurasa wa pili mwenye Na. 0759373552, aliwaambia kwamba, haya, nendeni tutawapa utaratibu wa kuja kulipia ng'ombe wenu. Walikaa mpaka tarehe 28 wakiendelea kufuatilia kusubiri utaratibu wa kulipia mifugo yao. Mpaka tarehe 28 askari hawajawapa wananchi utaratibu wa namna ya kulipia mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, wamiliki wa mifugo ni familia ya Waloomukurusas ambao ni ng'ombe 460, Familia ya Sinjorematika ng'ombe 573, Familia ya Ndagusakoros kondoo na mbuzi 750.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo linaleta utata; idadi ya mifugo iliyopelekwa kwa ajili ya kutaifisha ni ng'ombe 806, lakini wenye ng'ombe wao wanajua kwamba kwa ujumla wao wana ng'ombe 1,033. Kondoo na mbuzi waliopelekwa kwa ajili ya kutaifishwa ni kondoo 420 na mbuzi 100, lakini wale wenye mbuzi na kondoo wanajua ni 750. Baada ya kujua kwamba kuna chenga nyingi, niliamua kuja kwa viongozi wetu ngazi ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kwenda huko niliwasiliana na ndugu anaitwa Bwana Moronda, muda wa saa tano siku ya 29, Saa 5.23. Bwana Moronda ni Mhifadhi wa Hifadhi ya Serengeti, nikazungumza naye kwa simu. Baada ya kuzungumza naye Saa 5.23, Saa 5.29 nilimtumia ujumbe wa maneno kumsihi kwamba awaruhusu wananchi waweze kulipia mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, Bwana Moronda anatumia simu iliyosajiliwa 0752220727. Baada ya kumtumia Bwana Moronda ujumbe huo, niliamua kumtumia Bwana Mussa Kuji ambaye ni Kaimu Kamishna Hifadhi za Taifa. Baada ya kufanya juhudi hizo zote, niliwasiliana na Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa njia ya *WhatsApp* akiwa Kigali Rwanda, nikimjulisha suala hili. Nikamwomba aweze kufuatilia. Nakiri kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri alifuatilia jambo hili na yeye nilimtumia ujumbe kupitia *WhatsApp* muda wa saa 4.18, akiwa Kigali Rwanda, akaniambia akifika Tanzania atalifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alipofika Tanzania ni kweli alinitumia ujumbe kwa njia ya *WhatsApp* akaniambia kwamba Mhifadhi wa *TANAPA* wameshafungua jalada Mahaka ya Mgumu, Wilaya ya Mgumu, yenye Namba MGM/IR/2977 ya mwaka 2023, Mugumu Wilaya ya Serengeti. Baada ya kujua hili, niliwaambia wananchi waende huko ili kama watapeleka mifugo Mahakamani, wakatoe ushahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya wahifadhi kujua kwamba wananchi wameenda Mugumu walienda kufungua kesi nyingine Wilaya ya Musoma, siku hiyo hiyo. Wakaenda Wilaya ya Musoma

ambayo ni nje ya Wilaya ya Serengeti, lakini cha kushangaza niliwasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, siku hiyo hiyo, yeye akaniambia kuhusiana na mifugo 806, kondoo 420 kesi ipo Mahakama Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kinachoshangaza ni danadana zilizochezwa, kutoka idadi ya mifugo, kutoka kesi ilipofunguliwa kwamba ipo Mugumu, ikahamishiwa kwenda Musoma na wananchi nao walienda Musoma asubuhi. Walipofika kule Musoma wakiwa nje waliuliza kuna kesi ya mifugo inaendelea, wakaambiwa hakuna. Wamekaa baada ya muda wakatoka wale watu wa hifadhi pamoja na *Court Broker* kazi inayoenda kufanyika ni kwenda kuuza mifugo ambayo wanasema haina wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea hapa ni tatizo kubwa. Kwanza kwenye idadi ya ngo'mbe…

**SPIKA:** Muda kidogo unatutupa mkono, malizia hoja yako dakika moja.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba, hakuna mtu anayepinga mifugo kuingia hifadhini kwa sababu mifugo pamoja na hifadhi zetu ni rasilimali zetu wote. Ninachoangalia kwamba baada ya mifugo kujulikana kwamba ni ya nani, mimi nimemjulisha Mheshimiwa Waziri, nimemjulisha Naibu Waziri, nimewajulisha Wahifadhi wote, lakini baadaye bado wale mifugo ilienda kuuzwa kwamba ni mali isiyokuwa na mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lipo hapa. Je, adhabu ambayo tunaweza kuwapa wananchi wetu ni kuwafilisi? Kwa sababu kwenye eneo, adhabu ambayo tunaweza kuwapa, ingekuwa mifugo, sheria zetu zinasema kama ng'ombe wamekamatwa ndani ya siku saba hakuna mtu aliyekuja kudai, Askari wa *TANAPA* waliwapeleka wale vijana na kuwarudisha Kijiji cha Ulolosokwan wao, baada ya kufungia ng'ombe wakawachukua na gari

wakawarudisha Kijiji cha Ulolosokwan, ambacho kipo ndani ya Wilaya ya Ngorongoro, Saa Moja Usiku kwa gari lao la *TANAPA*. Je, ni kwamba hawajui kwamba hawa ng'ombe hawana mwenyewe au waliamua kuwakomoa wananchi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala linauma. Mpaka sasa kwenye Jimbo langu zaidi ya ng'ombe 2,000 na kitu wameshataifishwa na wananchi zaidi ya 400 sasa ni maskini wakutupa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Haya, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tumeyasikia maelezo ya Mheshimiwa Mbunge hapo, na maelezo yake kwa kina aliyaleta kwangu ambayo yameandikwa na mimi niliikabidhi Serikali ili iweze kutoa ufafanuzi juu ya jambo hili halafu tutasema jambo. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi nasi kama Serikali tuweze kutoa maelezo kuhusiana na suala hili linalohusisha ng'ombe 806, kondoo 420 pamoja na mbuzi 100.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo yeye mwenyewe ameeleza *narration* ya mawasiliano kati yangu, kati ya Mhifadhi wetu Serengeti vilevile Naibu Waziri pamoja na viongozi wengine wa Kiserikali, ninapenda tu kuongea kwa uchache sana nisingependa kurefusha majadiliano. Bahati nzuri ni suala ambalo limehitimishwa

Kimahakama, kupitia kesi ya Jinai Namba 10 ya mwaka 2023 kwa kuingiza mifugo hifadhini isivyo halali na tayari hukumu ilitolewa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Novemba hukumu ilielekezwa dalali wa Mahakama ateuliwe kwa ajili ya kuweza kupiga mnada wa hadhara kwa kufuata taratibu kama ambavyo Sheria yetu ya Wanyamapori ya mwaka 2009, vilevile Sheria yetu inayosimamia Hifadhi ya Taifa zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa kwa mujibu wa Ibara yetu ya 27 pamoja na sheria zetu ambazo tumeziweka, kimsingi nia ya Taifa na nchi ni kuendelea kulinda hifadhi zetu pamoja na maliasili tulizonazo. Vilevile kuhakikisha kwamba pia tunalinda uoto wa asili uliopo pamoja na wanyama na viumbe vingine vilivyopo katika maeneo yetu yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia na mnada huo uliyofanyika Tarehe 01 kufuatia hukumu iliyotolewa, hukumu halali ya Mahakama Kuu Musoma, ilielekezwa mnada huo ufanyike na tayari mnada umefanyika na zilipatikana shilingi 169,264,000. Hiyo ndiyo hali ambayo tunayo kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, nieleweshe jambo moja hapa, tarehe 1 ndiyo siku hukumu imetolewa. Hukumu imetolewa Tarehe 01?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, inabidi niangalie *data*, kati ya tarehe 30 au tarehe 31 Oktoba.

**SPIKA:** Nitazamie hiyo hukumu imetolewa lini na mnada umefanyika lini.

Mheshimiwa Mbunge, wakati wa maelezo yako ya mwanzo yakuzungumza nilikuwa naandika hapa. Ulisema Askari wa *TANAPA*

wamefika Kijijini, Askari wa *TANAPA* walifika kijijini wakachukua hao ng'ombe ama ng'ombe walikuwa kwenye hifadhi ndiyo wakakamatwa huko? Ama ile sentensi yako ya Askari wa *TANAPA* walifika kijijini, yaani waliwafuata ng'ombe kijijini au ng'ombe walikuwa kwenye hifadhi?

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba Askari wa Hifadhi wamefuata ng'ombe kijijini na kuwaswaga kwa muda wa masaa manne, mpaka zaidi ya kilomita kama 50. Wakaswaga mifugo kuingiza hifadhini, siyo mara ya kwanza hata Musoma na maeneo mengine inafanyika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ngoja, ngoja, Mheshimiwa Waziri umezipata tarehe? Umenisomea hapo sasa hivi tu, mimi nimeandika hapa kwangu tarehe 01, Novemba.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, mnada ni tarehe 01, nataka tu nijilidhishe na hukumu ilikuwa tarehe 30 au tarehe 31, dakika chache tu. Hukumu ni Oktoba…

**SPIKA:** Sawa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, sasa nataka nijiridhishe 30 au 31 Oktoba, lakini mnada kama mnada kupitia dalali wa Mahakama Maulid, ulifanyika tarehe moja na kiwango cha fedha ni hicho hicho nilichokitaja.

**SPIKA:** Sawa, nimekuelewa. Nitazamie hukumu imetolewa lini na mnada umefanyika lini. Mheshimiwa Mbunge, ama unazo hizo taarifa?

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, hukumu imetolewa tarehe 31 Oktoba na ng'ombe wakauzwa tarehe 1.

**SPIKA:** Sawa. Sasa Mheshimiwa Waziri, kuna haya niliyomuomba, hukumu tarehe 30, tarehe 31? Sawa, tarehe 31

hukumu Oktoba, halafu mnada tarehe 01 Novemba? Sawa, sasa hapa naona kuna hoja mbili ama tatu, sasa Mheshimiwa Mbunge nisaidie, hii kesi wakati inaendeshwa, maana yake ni kwamba ng'ombe walikamatwa halafu kesi ikaanza Mahakamani, wananchi walishiriki kwenye hiyo kesi au hapana au wameshtukia mnada?

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, kwenye maelezo yangu nilisema, wananchi walienda Mahakama ya Mugumu ambayo ndiyo tuseme Hifadhi ya Serengeti ipo, ambako ndiyo jalada lilifunguliwa. Baada ya wananchi kufika Mahakama ya Mugumu, Askari wa Hifadhi waliamua kwenda kufungua kesi nyingine Musoma wakaachana na lile jalada la Mugumu ambako ni Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, sasa walipoenda kule wananchi wakawa wanawafuata popote pale wanapoenda, kila siku kufuatilia ng'ombe wao, mpaka hukumu inatolewa walikuwa wamesimama kwenye Mahakama ya Musoma Asubuhi, kwa hiyo, wananchi hawajashiriki. Maana yake wameenda wakaingia wakaambiwa hamna kesi inayoendelea, walishtukia tu watu wa hifadhi wanatoka Mahakamani na huyo *Court Broker*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo hapa kulikuwa na kesi mbili.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika..

**SPIKA:** Narejea kwako Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo kesi tuseme ni mbili, hii ya Mugumu ikaachwa haijatolewa uamuzi mpaka sasa, ikaenda Musoma mpya ndiyo ikatolewa maamuzi.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo. Wananchi hawajashiriki.

**SPIKA:** Sawa, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Wazri, ulikuwa umesimama.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kuweka ufafanuzi. Hiyo Mugumu anayoifanyia *citation* ya *reference* ni *IR Number* na *AG* atatusaidia. Kwenye *IR* unakuta ni jalada la uchunguzi, jalada la uchunguzi kwa kesi za Polisi na kama haujafikishwa Mahakama Kuu kunakuwa na jalada la uchunguzi, ndiyo hiyo *Investigation Report Number,* inaenda kwa *citation* hiyo, lakini kesi kama kesi ni Mahakama Kuu, kupitia *application Number* 10 ya mwaka 2023.

**SPIKA:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge hamna mtu ambaye ni mtaalam wa kila kitu. Uchunguzi umefunguliwa jalada Polisi – Mugumu, halafu kesi yenyewe ikaenda kufunguliwa Musoma, kwa kuwa ilikuwa inaenda Mahakama Kuu. Huku Serengeti hakuna Mahakama Kuu, maana hiyo nayo inawezekana labda huku Serengeti hakuna Mahakama Kuu, Mahakama Kuu ipo Musoma, ndiyo maana kesi ikapelekwa Musoma? Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 164 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mikoa zina *Concurrent Jurisdiction*. Kwa kuwa uchunguzi ulikuwa unafanywa na Ofisi ya Mkuu wa Makosa ya Jinai Mkoa, hiyo ndiyo ilikuwa *base* ya shauri hilo kwenda Mahakama ya Hakimu Mkazi.

Mheshimiwa Spika, baadae baada ya changamoto iliyojitokeza kukawa na shauri, ndiyo shauri likafunguliwa Mahakama Kuu, Kanda ya Musoma ambayo ndiyo yenye dhamana na Mahakama zilizopo Mkoa wa Mara.

**SPIKA:** Sawa. Jamani kwa sababu kama nilivyosema Mheshimiwa Mbunge aliniletea hoja ya wananchi wake kwa maandishi na mimi nimeikabidhi Serikali. Sasa ili tuweze, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge, yeye ameleta hoja ya wananchi wake na

malalamiko yaliyopo huko ili tuweze kulitazama hili jambo vizuri, tuipe Serikali muda itazame hilo jambo ili tuweze kujielekeza vizuri. Kwa sababu Mheshimiwa Mbunge, na hapa Mheshimiwa *Chief Whip* naomba uchukue hili na Mheshimiwa Waziri. Kesi imeshaamuliwa Mahakamani na Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyojua kesi ikishaamuliwa Mahakamani utaratibu ule wa kawaida unafuatwa huko. Kwa maelezo yaliyopo ni kwamba kesi imeamuliwa na kwa utaratibu kama hukuridhika unatakiwa kwenda Mahakama ya Juu.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye kesi hii kuna hii hoja ya kwamba moja, wananchi hawajashiriki aidha kwa kutokupewa taarifa. Maana kama walikuwa wanazunguka namna hii na mpaka hukumu imetoka, mpaka mnada umefanyika wao hawana taarifa, kidogo panakuwa hapajakaa sawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ili tuweze kujiridhisha, Serikali ipewe muda maana na yenyewe huenda itaeleza kwamba Mahakama iliwasiliana nao kwamba kuna kesi hii tarehe hii hapa, kama Mheshimiwa Mbunge, alivyosema. Kwa hiyo, tuipe nafasi Serikali ili hizi taarifa ulizozitoa kwanza kuhusu Askari wa *TANAPA* kutoka hifadhini kwenda kwa wananchi ili wakaswage mifugo, maana hilo nalo limesemwa hapa ndani, pamoja na kwamba kesi imeshaamuliwa Mahakamani. Sasa hilo ni jambo ambalo ni zito kidogo, *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali nayo itatupa maelezo, kwa sasa haiwezi kuwa nayo hapa ndani kwa sababu ndiyo hoja imesemwa. Hoja nyingine ni hiyo ya ninyi kupata hiyo taarifa na kwa kweli kwa mazingira ya kesi yenyewe idadi inayosemwa siyo idadi inayosemwa ni nyingine. Kwa hiyo, hayo nayo unawaza labda mifugo mingine bado ipo Serengeti, halafu mingine ndiyo hukumu imetoka na ni nani anayethibitisha. *(Makofi)*

Sasa vitu kama hivyo ili mimi nisikae hapo mbele sina hizo taarifa, tuipe Serikali muda ikafuatilie jambo hilo pamoja na hiyo

hukumu na mimi niipate pengine itanipa picha. Halafu nadhani kwa kesho hatutatoa tena nafasi lakini nikishasoma pia ya Serikali tutaweza kusema jambo kuhusu hili. Mheshimiwa Mbunge, hoja yako imepokelewa na tumewapa upande wa Serikali na Mheshimiwa Waziri, taarifa nyingine anataka kujiridhisha basi tutalimaliza hili kesho.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo Waheshimiwa wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Maelezo ya Serikali kuhusu Usimamizi na Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro *KIA- Kilimanjaro Airport Development Company (KADCO)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kauli za Mawaziri, Kauli hii inakuja mahsusi kwa maelekezo ambayo tulikuwa tumeyatoa siku ya tarehe 5, kwa hiyo siyo ile kauli ya kawaida, kwa hiyo wanakuja na taarifa kwa ajili ya kusema jambo ambalo tulilowaelekeza tarehe 5 walifanyie kazi.

Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Mbarawa.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya Serikali kuhusu Usimamizi na Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, utangulizi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa kibali cha kukutana leo tukiwa wazima wa afya njema. Naomba kutumia fursa

hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuongoza kwa ufanisi na umahiri mkubwa. Mheshimiwa Rais, ameendelea kuweka mkazo wa kipaumbele katika kusimamia, kuboresha na kuendeleza miundombinu ya uchukuzi, tunaomba Mwenyezi Mungu ammjalie Rais wetu afya njema ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais, katika kuongoza nchi yetu, ni wazi kuwa Mheshimiwa Makamu wa Rais ameendelea kutekeleza majukumu yake kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi na utendaji wao mahiri katika kusimamia shughuli za Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Dunia - *IPU*. Kwa kweli umeweka historia na umeliletea Afrika na Taifa letu heshima na sifa kubwa. Aidha ninamshukuru Ndugu Charles Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kwa kazi yake nzuri, sote ni mashuhuda wa kazi anayoifanya katika utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* na Kamati yake kwa kazi nzuri waliyoifanya ya uchambuzi wa taarifa ya *CAG*. Nichukue fursa hii kuishukuru Kamati hiyo kwa kuendelea kutoa maelezo na ushauri mzuri kwa

Wizara ya Uchukuzi. Nakiri kuwa Kamati hii imekuwa chachu kubwa katika kuongeza ufanisi katika utendaji wa Wizara ya Uchukuzi, maoni na ushauri wao umezingatiwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo machache sana kuhusu *KADCO*, baada ya salamu hizo naomba nitoe maelezo mafupi ya Serikali kuhusu Usimamizi Na Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro yaani *KIA*. *Kilimanjaro Airport Development Company (KADCO)* ni kampuni iliyosajiliwa mnamo tarehe 11 Machi, 1998 kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni Sura 212.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji nchini, chini ya Serikali ya Awamu ya Tatu, Serikali iliamua Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, kiendeshwe kupitia sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo Serikali kupitia maamuzi yake ya tarehe 6 Julai, 1998 iliamua usimamizi na uendeshaji wa *KIA* utekelezwe kupitia sekta binafsi. Maamuzi hayo ya Serikali yalitokana na sababu mbalimbali, zikiwemo za gharama kubwa za uendeshaji wa kiwanja hicho wakati huo, kwa wakati huo *TAA* ilikuwa haijaanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uamuzi huo, Serikali na *KADCO* iliingia mikataba mitatu ambayo ni Mikataba ya Wanahisa *(Shareholders Agreement)* ambao ulikuwa baina ya Serikali na Wanahisa wenza na mikataba miwili ambayo ni Mkataba wa Uendeshaji *(Concession Agreement)* pamoja na Mkataba wa Ukodishaji *(Lease Agreement)* baina ya Serikali na *KADCO*. Mikataba ya Uendeshaji na Ukodishaji ilisainiwa tarehe 10 Novemba, 1998.

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Mei, 2009 Serikali kupitia iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ilielekeza kununua hisa za wanahisa wenza wa *KADCO* na kuelekezwa kuwa *TAA* iendeshe

*KIA*. Baada ya hatua hiyo, kuanzia mwaka 2010, *KADCO* iliendelea kusimamia na kuendesha *KIA* kupitia Mikataba ya Uendeshaji *(Concession Agreement)* na ukodishaji *(Release Agreement)* ambayo ukomo wake umefikia leo tarehe 9 Novemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kiwanja cha *KIA* kinamilikiwa na Serikali kupitia *TAA;* na kwa kuwa Mkataba wa Uendeshaji *(Concession Agreement)* pamoja na Mkataba wa Ukodishaji *(Release Agreement)* ambayo ukomo wake umefikia leo tarehe, 9 Novemba 2023; na kwa zingatia maelekezo ya Bunge lako tukufu ya tarehe 5 Novemba, 2022 na tarehe 4 Novemba, 2023. Serikali imeamua kuchukua hatua zifuatazo: -

(i) Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi, itakabidhi rasmi Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro *(KIA)* kwa *TAA* kuanzia tarehe 10 Novemba, 2023 kwa kuzingatia sheria, taratibu za Serikali na kama ilivyoelekezwa na Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

(ii) Baada ya makabidhiano hayo, Serikali itaendelea kuratibu na kusimamia hatua zote za uhamishaji huo ili kulinda maslahi mapana ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naendelea kulishukuru Bunge lako Tukufu na Kamati zake zote za Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya. Serikali itaendelea kutumia ushauri unaotolewa na Bunge lako Tukufu katika uboreshaji wa utendakazi wake. Lengo ni kuendelea kuwatumikia na kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona Waheshimiwa wamesimama kuunga mkono hoja yako. Haya, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, ni kweli kuwa siku ya tarehe 5 wakati tukihitimisha hoja hapa ya kuhusu Hesabu ambazo zimekaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022, tulitoa maelekezo mahususi kuhusu hoja iliyokuwa imepelekwa Serikalini tangu mwaka jana 2022, Novemba na mwaka huu tena tukaikuta, tukawapa maelekezo Serikali, na sasa Serikali imeshaleta hii taarifa ambayo tuliwaambia watuletee. Hii taarifa imeonesha humu kwamba Serikali inachukua hatua na leo ni tarehe 9, Serikali inasema itakabidhi Uwanja wa *KIA* kwa *TAA* kesho tarehe 10. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni jambo jema na ninaamini tutasikia hizo habari za makabidhiano. Pamoja na hayo, nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kwa kusikiliza Bunge ilichosema kwenye hoja hii na kuifanyia kazi kwa haraka kuhakikisha Kiwanja cha *KIA* kinarejea kwa *TAA*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo, maadam makabidhiano ni kesho, nasi Bunge tunamaliza kesho, naamini jambo hili litakuwa limekwisha kwa sura hiyo. Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Miundombinu ataripoti jambo hili kwa utaratibu ule wa kawaida; Taarifa za Kamati zinapokuja Bunge lile la mwezi wa Februari, tutalisikia jambo hili likiwa limeshakamilika. Serikali kama kuna mambo mengine ambayo mnatakiwa kuyafanya baada ya haya makabidhiano, basi tutakapokuwa tunasikiliza Taarifa ya Kamati, mwezi Februari, tusikie Kiwanja Kipo *TAA* na *TAA* wapo pale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Waziri, kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge, tutafanya uzinduzi rasmi wa *Bunge Marathon*, ambayo itafanyika leo. Tutafanyia Ukumbi wa Msekwa (mbona sioni ukumbi hapa!). Haya tunakaribishwa sote, lakini Ukumbi utatangazwa, naona kwenye hili tangazo sioni ukumbi. Yuko wapi Mwenyekiti anayehusika? Hayupo humu ndani!

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nipo hapa Mwenyekiti.

**SPIKA:** Ukumbi ni wapi Mwenyekiti?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ni Ukumbi wa Msekwa, ahsante.

**SPIKA:** Haya, sawa. Tukutane ukumbi wa Msekwa saa 7.00. Kwa hiyo, sote tukutane huko na Spika wa Bunge atakuwa mgeni rasmi kwenye hilo zoezi. Kwa hiyo, tutaenda tuzindue hapo hiyo *Marathon* yetu. Sasa tunaendelea na ratiba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU- KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango; kwamba Bunge lipokee…

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Hebu subiri kwanza. Mheshimiwa Saashisha, kwa kifupi, muda wetu umekwenda sana Waheshimiwa Wabunge.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nami naishukuru sana Serikali kwa kutoa ufafanuzi kuhusiana na jambo kubwa lililokuwa linatutatiza sana la umiliki wa *KADCO*.

Sasa kwa kuwa Serikali imekubali na kesho inakabidhi rasmi Uwanja ule kuwa mali ya Serikali, nilikuwa naomba mwongozo wako namna ya kuondoa kumbukumbu zile za nyuma ambazo Mheshimiwa Waziri alisimama akisema, kuna sheria zinakinzana, kwa hiyo, isingewezekana; na Mwanasheria wa Serikali akatoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, zimebaki kwenye kumbukumbu, naomba mwongozo wako namna ya kuziondoa sasa ili jambo hili liwe kwenye mstari ulionyooka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha, umesema vizuri kwamba waliokuwa wamesema ni Mheshimiwa Waziri na akasema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, siyo Bunge lililosema. Bunge limesema hiki ambacho kimesemwa sasa hivi hapa.

Kwa hiyo, chochote kilichokuwa kimesemwa kabla na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kilichosemwa kabla na Mheshimiwa Waziri kinakuwa hakipo tena, maadamu maamuzi ni haya ya leo.

Kama nilivyosema, upande wa Bunge tutapata taarifa kwa njia ile ya kawaida kabisa kwamba jambo hili limekamilika tutakapokutana kwenye Bunge la mwezi Februari. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuendelee na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI.**

## KAMATI YA MIPANGO

### Mapendekezo ya Mpangao wa Maendeleo ya Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025
### na
### Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sote tunafahamu taratibu tunaposhughulikia jambo hili. Sasa nimwite tena Katibu ili tuweze kuendelea.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango

**SPIKA:** Kamati ya Mipango

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza michango yetu kama ambavyo hoja ilivyo mbele yetu, Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Ninayo orodha ya wachangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhe. Cosato David Chumi na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, niseme kwamba Wizara yetu mpya ya Mipango mahali ambapo mipango yetu inapaswa kuanzia kwa mwakani na Wizara mpya ni kuangalia mipango yetu tuliyojiwekea ambayo ipo kwenye *vision* 2025. Muhimu hapo inasema kwamba tunataka kujenga uchumi shindani halafu ifikapo 2025 pato letu la Taifa ukiligawa *GDP per capita* kila mtu apate dola 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba mipango hii lazima iwe na sura mbili. Kwanza mipango na uwekezaji ambao matunda yake yatapatikana kwa haraka sana ndani ya mwaka mmoja au miwili; halafu mpango na uwekezaji ambao matunda yake tutayaona baada ya miaka mitano na kuendelea. Sasa uchumi wetu kwa muda mrefu umekuwa kati ya asilimia tano na asilimia sita. Imedhirika kwamba ukuaji huo wa uchumi ambao tumekuwa nao

kwa miaka kati ya miaka 20 na 30, haujaweza kuondoa kwa kasi kubwa umasikini nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mipango yetu ni lazima ijielekeze kwenye uchumi unaokua kwa zaidi ya asilimia sita. Duniani kote wamepiga hesabu, uchumi huo lazima ukue kwa kati ya asilimia nane mpaka asilimia kumi. Cha pili, ikifika mwisho wa mwaka huu *GDP per capita* yetu itakuwa dola 1,113. Bado tupo mbali sana kwenye malengo ya dola 3,000. Mpango wetu lazima ujielekeze kwenye kufuta umaskini. Mipango lazima ifute umaskini na uwekezaji lazima ufute umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya sasa umaskini nchini mwetu ni kwamba takwimu zinaonesha asilimia 18.7 ya Watanzania hawa wapo *below food poverty line,* matatizo ya chakula asilimia 18.7. Kwa matumizi ya kawaida, *basic needs* yaani *poverty line* ukichukua umaskini kwenye hiyo ngazi ni asilimia 35.7. Ukichukua umaskini wote kwa nchi nzima unakuta asilimia 13, mijini watu siyo maskini; asilimia 87 vijijini ni maskini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mipango yetu ijielekeze kwenye miradi ya kufuta umaskini. Bado tuna mipango ya malengo ya Kimataifa. Niliona hapa wengine wanaongelea utajiri, hili nadhani tusiliweke huko, hatujafikia huko. Kuna tofauti ya utajiri na mtu kuwa na kipato cha kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mapendekezo yangu ni haya; uchumi wetu ukue kati ya asilimia nane mpaka kumi na maeneo ya kukuza huo uchumi, la kwanza tuwekeze kwenye uchumi wa gesi za aina tatu; ile gesi asilia halafu *Helium, Carbon Dioxide* na gesi nyingine. Kwa hiyo, miradi yetu ingeeleza sana kwenye fedha za haraka kutokana na uchumi wa gesi, halafu kwenye madini tukiacha dhahabu kuna madini ambayo yana thamani na yanahitajika sana duniani na huko tuwekeze. Mahali pengine penye kupata mapato ya haraka sana ni kwenye kilimo, uvuvi, ufugaji na

utalii. Kwa hiyo, hivi ndiyo vyanzo vya vipaumbele vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mpango tulionao, mimi napendekeza, haya yote ili yafanikiwe lazima tuwe na haya yafuatayo: Lazima tuwe na elimu bora kwa ngazi zote. Ni kwamba, tumetengeneza sera ile ambayo itaanza 2027. Hata hivyo nina wasiwasi kama Halmashauri zetu na Mabaraza ya Madiwani, yanaweza yakasimamia utekelezaji wa hiyo sera. Kwa hiyo, elimu bora maana yake ni kwamba tupate walimu na wakufunzi walio bora. Lazima tupate vifaa bora vya kufundishia na kujifunzia kama maabara na *libraries.* Kwa hiyo, mipango yetu lazima iangalie nchi ambazo zimefanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi nyingine huko duniani ningechukua nchi tatu; *South Korea, Finland* na Uingereza ambao tumerithi mtindo wao wa elimu. Kwa Afrika hapa kwa elimu bora sisi hatujawa hata kwenye tano au kwenye nane bora. Kwa hiyo, ya kwanza ni *South Africa*, ya pili ni Kenya, ya tatu ni Botswana. Hebu tujifunze kwa nini wao wanasemekana kuwa na elimu bora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili, kwenye mipango yetu na ambacho sidhani kama kimewekewa sana mkazo, ni mambo ya utafiti na ubunifu. Hakuna Taifa lolote ambalo linasema lina mipango mizuri ya maendeleo bila kuwekeza kwenye *research development* na *innovation.* Mpango wetu lazima uoneshe maeneo ya kipaumbele *(focus areas)*. Mimi ningechukua upande wa kilimo, *seed science* na *technology;* ningechukua *space science* halafu ningechukua *nuclear science* na *life sciences* kwenye mambo ya matibabu na kadhalika. Mipango yetu lazima iseme hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mipango yetu nayo ituoneshe tuna watafiti wangapi? Tuna wataalamu wangapi? Kuna viwango vinatolewa Kimataifa kwa watu 1,000 walioajiriwa, sisi tuna wangapi? Kwenye Bajeti ya Utafiti, vilevile lazima mipango yetu

iongoze bajeti. Inasemekana kwamba mwaka 2022 Tanzania tumetumia dola milioni 870, lakini majirani zetu Kenya wametumia bilioni mbili. Dunia utafiti umetumia zaidi ya trilioni 2.5. Kwa hiyo, unaona jinsi ambavyo mipango yetu haijaweka mkazo kwenye mambo ya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mbali ya hayo, lazima twende kwa vitu ambavyo Watanzania wanavihitaji kila siku. Hapa nachukua vinne tu. Watanzania Mipango yote tunayojadili wanataka wapate chakula, wanataka maji, wanataka umeme na wanataka matibabu. Kwa hiyo, mipango yetu ishughulikie hayo. Kwa mfano, suala la chakula ni lazima tujue miaka 10 au 20 ijayo tunahitaji chakula kiasi gani? Hili tumeliongelea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni maji. Kipimo hapa ni washauri. Hiyo ya kusema kijiji, wilaya fulani imefika asilimia 70, siyo kipimo kizuri. Hicho ni kipimo cha fursa, lakini kipimo kizuri ni kile ambacho mtu anatumia maji kiasi gani kwa mwaka? Hicho ndicho kipimo kizuri cha kitaalamu, lakini kile cha fursa, maji yanaweza kuwa mjini, maji yanaweza kuwa kijijini, fursa inasema asilimia 70 au 80, lakini ukija kwenye utumiaji, unakuta ipo chini kabisa. Kipimo cha kitalaamu hapa wanakiita *Water Stress Indicator,* yaani eneo ambalo mwananchi mmoja mmoja kwa mwaka hatumii zaidi ya lita 1,000,000. Duniani huko kitaalamu inasemekana kuna matatizo hapo. Kwa hiyo, ripoti za kusema tu asilimia 70, haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni umeme. Haya yote yapo kwenye *document* ya *UN, Sustainable Development Goals,* yapo *African Union* ambayo Waziri alisema wametumia kama hili la umeme ni *SDG Seven.* Sasa umeme nao tatizo ni hilo hilo, mtu anasema sehemu fulani ni asilimia fulani, lakini siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je ukisema kwamba Musoma Vijijini, kijiji changu kimoja asilimia 75 wanapata umeme, hiyo ni fursa kwamba umeme umekaribia, umesogea lakini kipimo kizuri ni umeme kiasi gani ambao mtu anautumia kwa mwaka. Kwa hiyo,

mbali na kutoa hizi asilimia Waheshimiwa Wizara mbalimbali lakini waende mbali sana watoe na umeme kiasi gani. Sasa hapa nitakuonesha jinsi ambavyo utumiaji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia dakika moja.

**PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unachukua nchi tajiri Africa ni Seychelles umeme wanaoutumia watu kwa mwaka ni *unit* 4,640 na *GDP* yake ni zaidi ya dolla 17,000. Unakuja unachukua majirani zetu Kenya, umeme wanaotumia kwa mwaka kwa *unit* ni *unit* 180, *GDP* yao *per capital* ni zaidi ya dola 2,000. Unakuja Tanzania, umeme tunaoutumia zile *zero*-unit ni 99.6 na *GDP* yetu ni karibu dola 1,100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kwamba labda nirudie kwa kusema tuwe na mipango ambayo tukiwekeza kwenye kilimo, kwenye uvuvi na mifugo tutapata mara moja lakini tuwe na mipango ya kuwekeza vilevile kwenye mabarabara na reli ambapo mapato yake yanaweza kupatikana baada ya muda mrefu. *(Makofi)*

**PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Sospeter Mhungo kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Cosato David Chumi atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Halamga, Mheshimiwa Tarimba Gulam ajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa siku ya leo pamoja na kuwa sauti yangu haipo vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali kwa sababu ya kupokea maoni ya Wabunge na maoni ya wadau; na kurejesha Tume ya Mipango lakini kuja pia na hii Wizara ambayo inaongozwa na Profesa Kitila Mkumbo ambaye wakati naanza Chuo Kikuu cha Dar es salaam alikuwa Rais wangu wa *DARUSO* na mimi nikawa Mbunge kwenye Bunge la Wanafunzi. Tulikuwa tunachuana sana pale USRC nadhani unakumbuka Makamu wako wa Rais akiwa Dkt. Francis. Kwa hiyo, nakufahamu kwa utendaji toka siku zile tukiwa pale Chuo Kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa na Mheshimiwa Kibajaji, Mheshimiwa Lusinde tulikuwa tunaenda Iringa, Mafinga kwenye shughuli pale Bwawani kwa Mchungaji Mahimbi na wachungaji wale walisema wao kama viongozi wa dini wapo na Serikali na mojawapo ya kazi wanayoifanya ni kuombea Serikali lakini pia kumuombea Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tupo na watu wanatuombea katika nchi hii sisi kama viongozi kwa hiyo ni wajibu wetu kutenda yaliyo mema kwa manufaa ya nchi hii. Siku ile ninapoongozana na Mheshimiwa Lusinde, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu akaniambia naona mmejichagua, sikumwelewa. Baadaye akaniambia si naona mnaenda wote simba huko Mafinga mmechagua, wewe simba Mheshimiwa Kibajaji nae simba. Sasa mimi baadaye nikakaa nikaona alah! Kumbe Waziri wa Mipango naye yanga, Waziri wa Fedha naye yanga, *of course* mmeteuliwa lakini imetokea nyinyi nyote yanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni simba inaeleweka niwaombe kabisa fanyeni kama yale ambayo wanafanya Max Nzegeli na Pacome katika utendaji wa kazi ndani ya Serikali, nadhani mtakuwa mmenielewa vizuri najua wana simba wenzangu hawawezi kunikubali katika hilo lakini kuna hatua tukifika lazima tukubali ili tujipaange kwa hiyo, tumekubali yote tunajipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili. Kuna mtu juzi alikuwa ananiambia naona Wabunge Bunge hili mmechachamaa nikamwambia kwa nini? Akasema ingekuwa wakati wote mko hivi hivi, nikamwambia hapana inategemeana na agenda ya wakati huo. Kwa mfano, wakati ambapo yamefanyika mambo ya kupongeza tutapongeza, wakati mambo ya kusahihisha tutasahihisha, ndiyo wajibu wetu kama Wabunge. Kwa hiyo, kwa wakati huu kwanza mimi nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake na yakupongeza yapo mengi lakini mimi kwa niaba ya Wanamafinga nitasema moja tu maana yake naweza nikamaliza muda wangu kabla sijaenda kwenye hoja ya kuchangia mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja la kupongeza ni suala katika elimu, sisi pale Mafinga tuna shule ya msingi Mwongozo; ilikuwa na watoto kama 1800. Tumepata fedha tumejenga pembeni Shule ya Msingi Muungano, tumepunguza msongamano kwa watoto lakini Kata ya Boma ambayo ina watu wengi kuliko watu wote katika Mkoa wa Iringa kwa mujibu wa sensa na hapa pia nitumie nafasi hii kuwashukuru watu wa takwimu, walikuja kutujengea uwezo watu wetu namna ya kutumia takwimu katika kupanga mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alisema jana Mheshimiwa Profesa Shukrani nadhani hapo, kwamba ile sensa ikatusaidie katika kutumia takwimu katika kupanga mipango ya maendeleo; na kuna kitu wale watu wa sensa walitufundisha pale tulikuwa na viongozi wa dini na wazee na wakaanisha kata gani ina vijana wengi, kata gani ina wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale tulijifunza kwamba hii kata yenye vijana wengi maana yake inabidi mipango mingi ya kuweka shule nyingi ielekezwe kule kwa sababu hao ni vijana ambao *population wise* wao wapo kwenye *stage* ya kuongeza idadi ya watu duniani. Lakini viongozi wa dini mmoja aliniambia; Mbunge nimejifunza hapa kwamba lazima nijue waumini wangu wazee ni wangapi, vijana ni wangapi, watoto ni wangapi hata tunapopanga mipango ya

maendeleo ya kanisa letu au ya msikiti wetu basi tunaendana na ile takwimu na mtawanyo wa idadi ya watu katika eneo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza pia watu wa sensa. Kwa hiyo, nampongeza pia Mhehimiwa Rais katika elimu tumeona madarasa, ukienda Itimo pale kwetu Mafinga, ukienda Ndolezi, sabasaba na pale Ndolezi Kata ya Boma tuna shule mpya ya sekondari ambayo ita-*accommodate* sasa hawa watoto wanaotoka kwenye shule hizi za msingi. Kwa hiyo, itoshe kusema kwamba sisi kama Wabunge na hasa Wabunge wa CCM pale pa kukosoa na kusahihisha tutasema na pale pa kupongeza tutasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye mpango. Mimi nimesoma mpango na kwa jinsi ya mpango ulivyo maana yake ni kwamba ni wajibu wangu kama Mbunge kutoa maoni na mapendekezo kama ambavyo umesema mpango. Sasa yapo mambo nitashauri kwa maana katika hii matarajio au maoteo ya bajeti ya trilioni 47 ina mtawanyo wake kuna deni la Taifa kuna mishahara kuna *OC* na kuna mambo ya maendeleo; na fedha hizi tutazitoa wapi? Tutatoa mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kikodi, ninawapongeza *TRA* wamekuwa wakikusanya vizuri unaona yale maoteo wakati mwingine wanavuka zile asilimia, kuna fedha ni mikopo na misaada kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitoe ushauri. La kwanza katika ukurasa wa 11 wa *paper* ile ya Mheshimiwa Mwingulu ukurasa wa nane amesema kwamba, Mikakati. Amesema baadhi ya mikakati ni ile kuwa na *one stop center* ili kuboresha mifumo ya ukusanyaji pamoja na kutoa namba ya malipo jumuishi. Sasa hapa nimuombe Waziri wa Maliasili na Utalii na Waziri wa TAMISEMI, sisi Mafinga Mufindi tunategemea misitu na tunategemea msitu wa Sao Hill. Sasa wakati mipango ya Serikali ni kuwa na *one stop center* maeneo ya kukusanya mapato kwa jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi utaratibu uliokuwepo, kama mimi nikipewa ile bili na *TFS* kwa maana ya shamba la Sao Hill ninakwenda kulipa mle mle ndani nalipa na fedha za *Cess* na fedha zingine katika ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *TFS* wamekuja na utaratibu kwamba ile *Cess* awepo mtu wa halmashauri ya Mufindi wa Halmashauri ya Mafinga pale kwenye shamba la Sao *Hill* awe anakusanya. Sasa tunasema makusanyo jumuishi, *one stop center* kwanza tunatawanya nguvu na *resource;* lakini pili hatuwezi kukusanya ipasavyo. Kwa hiyo, mimi naomba na ninashauri *TFS* na Waziri na Wizara ya TAMISEMI tuendelee na ule utaratibu kwa sababu ndiyo maona ya Serikali lakini ndiyo utaratibu ambao una ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina ugomvi na *TFS* na wala sijawahi kuwa na ugomvi nao naamini katika hili tukishauriana vizuri tuendelee na ule utaratibu mtu akipewa bili alipe na kwanza hata yule mlipaji unampunguzia usumbufu. Sambamba na hilo ili tuboreshe na kuongeza makusanyo, ninashauri ndugu zangu tuangalie pia kwenye *VAT* sio tu kwenye mambo ya misitu hata katika upana wake tujaribu kuona je, hatuwezi kupunguza ikawa *user friendly* watu wakalipa kwa wingi wakalipa kwa hiari kama ambavyo tumesema hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kutoka mwisho. Wapi fedha nyingine tutapata, amesema hapa Mheshimiwa Kakoso, ninawashauri watu wa Serikali, nendeni kwenye *Hansard* kasomeni haya mambo ya hewa ya ukaa aliyosema Mheshimiwa Kakoso. Labda watu hawaelewi hewa ya ukaa maana yake ni nini? Sisi wenye misitu, kuna kitu ukanda wa bahari kinaitwa *blue carbon,* ile pale misitu kila inachopumua wale wenzetu wenye viwanda ndiyo inasaidia *at least* kwenye mambo ya *climate change* ku-*regulate* hii hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna fedha na Mheshimiwa Rais kila mwaka anaenda kwenye mkutano wa mazingira. Kwa hiyo, tayari kama mkuu wa nchi tayari ameshatoa hiyo sapoti. Kwa hiyo, wenzetu tushirikiane kwenye hewa ya ukaa kuna fedha kwenye mikopo, kuna fedha kwenye misaada lakini kuna fedha kwenye biashara hiyo ya mkaa. Ninaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho. Timu yetu ya JKT *Queens* mimi ni mwanamichezo jana imeshinda ipo kule Adjan wakiwa na Masau yule msemaji na ikifanikiwa kwenye mchezo ujao ikatoka sare itaingia nusu fainali. Kwa hiyo, tunavyounga mikono michezo, tuangalie Simba na Yanga lakini tuunge pia mkono JKT *Queens* ambao wachezaji asilimia mia moja ni wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na kama mwanasimba nasema tumekubali tunajipanga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chumi kwa mchango wako. Mheshimiwa Asia, atafuatia Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuchangia katika mpango wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuipongeza Serikali kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya haswa ya kuendelea kuisimamia miradi mikubwa katika nchi hii ambayo inaendelea kutoa fursa kubwa na kuendelea kutanua fursa kwa asilimia zaidi ya sabini kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania niwapongeze sana

Mawaziri, Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango kwa mpango huu wa mwaka 2024/2025. Naomba sasa niende kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mipango hii iweze kwenda na ili mipango hii tuweze kuhakikisha inaweza kufanikiwa, kwanza kabisa lazima tujiwekeze katika miundombinu ya umeme katika nchi hii. Bwawa la Mwalimu Nyerere linakwenda kuifungua nchi, lakini Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuhakikisha inaendelea kuleta miradi mikubwa katika nchi hii ambayo yote inahitaji umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere peke yake hauwezi kuja kutosheleza bado tunahitaji tuendelee kuweka fedha nyingi za kuhakikisha tunaendelea kutengeneza njia nyingine za kuweza kuvumbua umeme ili uweze kuwa suluhisho la matatizo na changamoto kwa Wananchi wa Tanzania na hususan vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia namna ambavyo umeme unakuza pato, kukatika kwa umeme ni hasara kubwa katika nchi. Kwa sababu, wapo watu wa *welding* ambao ni vijana wanategemea, wapo watu wa *ice cream* wanafunga huko wanategemea. Kwa hiyo, umeme unagusa watu wadogo na watu wakubwa. Unagusa viwanda vidogo na viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima katika mpango tuendelee kuhakikisha watu wa nishati na haswa kwenye umeme wanatengewa fedha na umeme mwingine unaendelea kuibuliwa ili kutatua kero ya umeme katika nchi yetu na kuweza kuhakikisha hakuna siku inayosababishwa na kukatika kwa umeme mapato ya nchi yanapungua katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili nijielekeze kwenye JKT. Hapa niongelee masuala ya kilimo, kwanza ninaishukuru sana Serikali kama kijana wa Kitanzania, kwa kupitia JKT kuwatengeneza vijana wetu katika uzalendo lakini kuwatengeza

vijana wetu katika kupata ujuzi wa stadi za maisha za kuja kuweza kujipatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia gharama kubwa sana na vijana hawa wanakaa kwa miaka mitatu kambini. Wana ujuzi mkubwa mno ambao sisi wenyewe Serikali tumewaweka katika uzalendo lakini katika ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wa Kilimo kwa ule mpango wa *BBT*. Mpango wa *BBT*, JKT wengi kupitia mazao ya mnyororo wa thamani, kilimo cha JKT wangeweza kuwatumia vijana wale wanapomaliza baada ya miaka mitatu leo tungetemea JKT sio sehemu tu ya kulima bali tuone sasa JKT inaenda kuwa na viwanda vidogo vidogo ili kutoa ajira kwa vijana wale ambao tayari kwa miaka mitatu tumewapa *study* na *skills* za maisha ambazo wanaweza kabisa kusaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama asilimia 40 tu ya vijana wanaotoka JKT ndiyo wanaoweza kuajiriwa kwenye vyombo vingine vya ulinzi na usalama lakini karibu asilimia 60 inarudi nyumbani na tayari tumewapa *skills* za maisha. Sasa ni lazima tuondokane na mazoea ama kukariri ama kutumia tu kanuni zile kwamba, ni kwa mujibu wa sheria na wakimaliza waende nyumbani lakini tuna uwezo wa kuwatumia kama ambavyo *BBT* imeweza kutoa ajira zaidi ya watu 800. Tayari tuna rasilimali na nguvukazi hii ambayo tayari ina nidhamu, ina weledi na inajua inafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BBT* imefanya vizuri sana lakini kila mkoa una vijana katika nchi hii, mradi huu ukiweza kuongezewa nguvu na ukaenda kila mkoa ili kuweza kurahisiha mradi huu kwa kule mikoani utawasaidia vijana wengi katika nchi yetu ya Tanzania na haswa nikiuchukulia mfano Mkoa wangu wa Manyara, hauhitaji kusubiri uweke miundombinu ya maji bali mvua zenyewe za msimu zinakuja mara kwa mara na kwa wakati na tuna uwezo wa kufanya uzalishaji mkubwa na ukawa na manufaa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la chumvi. Tumekuwa na chumvi nyingi sana katika nchi yetui ya Tanzania na haswa nikitolea mfano Mkoa wa Lindi. Ipo chumvi kule ya kutosha ambapo Waziri wa Viwanda, tungeweza kui-*process* kuweka viwanda vidogo vidogo ingeweza kusaidia Watanzania wasinunue chumvi inayoandikwa imetoka nchi fulani wakati ndani ya nchi yetu tuna chumvi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano wa wilaya ninayotoka, Wilaya ya Hanang. Kwa mwaka mmoja inazalisha zaidi ya tani 35,000 za chumvi; hiyo ni kwa kutumia *local* kabisa huko chini (njia za kawaida kabisa za kienyeji) lakini tunatarajia Waziri wa Mipango uone namna gani aidha tunapata wawekezaji wakubwa. Pia, kuna wawekezaji mle ndani wadogo wadogo wakawezeshwa ili kuweza sasa kwa sababu tukipata vyombo vya kisasa, maana yake kwa mwaka tuna chumvi zaidi ya tani 70,000. Tutaendaje kununua chumvi kutoka nchi nyingine wakati ndani ya nchi yetu tuna uwezo kabisa wa kutengeneza viwanda vidogo vidogo, na kuwatafuta wawekezaji. Lakini nje tu ya kuwa na chumvi ya Tanzania bali ni kutoa ajira kwa vijana, kina mama na wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuendelee kuliona hili kwa mapana yake, kwa ukubwa wake. Zile rasilimali ambazo tunazo tukaweza kuzitengenezea viwanda vidogo vidogo na kutafuta wawekezaji na tukaweza kufanya vizuri zaidi na kuingiza mapato katika nchi yetu. Fedha za Kitanzania lakini pia za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ya Tanzania imebarikiwa sana. Hapa naomba niongelee upande wa mashamba na ninaomba nijikite sehemu ambayo ninaifahamu vizuri, sehemu ambayo ninayotoka. Kule Hanang kuna shamba la Basutu. Shamba la Basutu kwa sasa hivi mwekezaji ana takribani ekari 40,000 ambazo zimeanza uzalishaji lakini katika ekari 40,000 ni ekari 22,000 ambazo ameweza kuzilima na ekari 18,000 zimebaki kama msitu. Nini ambacho ninataka kukiomba? Serikali ya Wilaya kwa maana ya

halmashauri inategemea shamba ambalo ni ekari 9,000 ambalo halmashauri inalimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fedha zile za halmashauri zinaingiza mapato kwenye halmashauri na mchakato wa fedha hizo ndiyo unaotumika katika mgao wa asilimia nne kwa wanawake, nne kwa kinamama na mbili kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali katika mpango wenu shamba lile la ekari 9,000 libaki kwenye halmashauri ili halmashauri iendelee kuingiza kipato kwa sababu mpaka sasa hivi inatumia karibu shilingi bilioni moja kujiingizia kipato. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali kwamba, kwa upande wa wawekezaji tumwangalie kwanza mwekezaji wa kwanza ekari 40,000 kazilima ekari 22,000 na ekari 18,000 zimebaki hazina kazi sasa tuchukue tena ekari 9,000 tuwape tena wawekezaji? Hebu niombe kwanza *study* nzuri ifanywe kwa huyu mwekezaji wa kwanza tuone anatuingizia tija gani katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele imegongwa lakini niendelee kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anatupambania vijana. Ukiangalia kwenye elimu, miundombinu mikubwa ambayo inaendelea kutengenezwa kwenye nchi hii vijana ndiyo nguvu kazi ambayo inatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asia kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nikiangalia katika mapendekezo haya ya mpango kwa mwaka 2024/2025, tunaona

Serikali inatarajia kutenga trilioni 15.3 na hii ikiwa ni ongezeko la trilioni 1.2 kutoka kwa hesabu za mwaka wa fedha 2023/2024 ambao tuko nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha nyingi sana na endapo zitatumika ipasavyo na Bunge hiki likaridhia kutenga kiasi hiki cha fedha, narudia kupiga mstari, zikatumika ipasavyo yawezekana kabisa tukaenda kuleta mafanikio makubwa katika uchumi wetu na kuwasaidia Watanzania pamoja na Tanzania yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia kwa maono yake. Ukisoma mpango unaweza ukaona ni kwa jinsi gani maono ya Serikali na maono ya Mheshimiwa Rais yalivyoweza kuchukuliwa. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba pamoja na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, naona wametengeneza timu nzuri sana sawasawa na mithili ya ile timu ya tano, moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mapendekezo haya na hasa ukisoma katika ukurasa wa 40 wa Taarifa ya Kamati ya Bajeti, sekta binafsi inakwenda kuchangia shilingi trilioni 12.29. Vilevile, Kamati imebaini kuwa, hakuna mfumo rasmi ambao umewekwa na Serikali katika kubaini mchango wa sekta binafsi. Hii ni hatari kwa sababu sekta binafsi tumekubaliana iwe ndiyo *engine* ya kuchochea uchumi wa Taifa letu. Hivyo, ni dhamira ya Serikali na ningependa iwepo hiyo kwamba, ijitokeze kwa wingi sana kuweza kui-*support* sekta binafsi ili hakika iweze kufanya vile inavyofanya. Iwe ni *engine* ya kuusaidia uchumi wa Tanzania uweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata hiyo dhamira ya Serikali yenyewe iliyopo, ukiangalia na hili nalizungumza kwa mara nyingine tena kwamba sekta binafsi ipo kwa minajili ya kufanya biashara, lakini pamoja na kufanya biashara, yenyewe ndiyo inayotuletea viwanda na iende hadi kufikia suala la *private public partnership*. Tunaona hapo kuna kusuasua na laiti kama Serikali

ingeweza ikajipeleka kwenda kutafuta suluhisho la kuisaidia sekta binafsi kama ilivyo katika nchi jirani ambazo nitazitaja, hakika Tanzania tunaweza tukapiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiangalia katika upande mzima wa ufanyaji wa biashara ambao ndiyo unaochagiza suala la uchumi, ningependa kuangalia nchi jirani ya Rwanda. Nchi ya Rwanda, iko namba 38 katika ile orodha ya *easy of doing business*. Nchi ya Kenya, majirani zetu ni nchi ya 56. Tanzania tuko wapi? Tanzania ni nchi ya 141, tuko mbali mno. Hii ni hatari, kwa sababu ukiangalia Mpango huu, mchango mkubwa kama tulivyoona unatokana na Serikali. Serikali ndiyo inakwenda kuchangia shilingi trilioni 15 katika masuala yanayohusiana na maendeleo ambayo nimeyataja kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi ni shilingi trilioni 12. Nchi hizi ambazo zimefanikiwa ni *the other way round*. Utakuta Rwanda sekta binafsi ndiyo inayoongoza katika kuchangia, Kenya sekta binafsi ndiyo inayoongoza kuchangia katika uchumi. Natamani niione Serikali yangu inajikita zaidi katika kuisaidia sekta binafsi ili iweze ikapiga hatua kuisaidia nchi hii kutimiza malengo yake ya kuwaletea Tanzania maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba, nchi yetu hii ni nchi ya ujamaa na kujitegemea na hata kwenye Katiba, ukiisoma Katiba Ibara ya 9 inasema hivyo. Waheshimiwa, pamoja na kwamba sisi ni wajamaa *thinking* yetu itoke kule. Kwa sababu tulikubaliana na Benki ya Dunia kwenye ile *Structural Adjustment Program* kuwa *private sector* iwe ndiyo sekta inayokuwa kama vile tunaita andamizi katika ukuaji wa uchumi wa Taifa. Tuonyeshe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai kwamba, tunapoangalia mipango yetu, zile fikra za miradi kuwa miradi yote mikubwa imilikiwe na Serikali tuondoke huko, kwa sababu tunaweka fedha nyingi sana katika utengenezaji wa miradi mikubwa. *SGR*, kufua umeme, wakati fedha zile yawezekana zingeingia katika

kusaidia maendeleo ya wananchi moja kwa moja kwenye *service delivery*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta sehemu kubwa ya fedha zile zinakwenda katika miradi mikubwa ambayo ingeweza ikasaidia kabisa kuwafanya sekta binafsi ndiyo wakawa wachangiaji. Tuingie katika mambo ya *public private partnership*, inaweza ikatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuboresha *private sector* na tunaiboreshaje. Hili narudia tu, ni somo ambalo tunalizungumza wakati wote. Jambo la kwanza katika Mpango huu, wafikirie kuangalia ni kwa jinsi gani wanakwenda kupunguza utitiri wa *regulatory authorities*. Wakazipunguze hizi ili angalau kuwepo na unafuu katika ufanyaji wa biashara na sekta binafsi iweze kufanikiwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Serikali haijafanikiwa kuondoa vizuizi katika soko la mitaji. Hebu waliangalie hili, *full liberalization of capital market.* Wakifanya hivi maana yake ni kwamba sekta binafsi inaweza ikapata nguvu ya kujisogeza mbele zaidi kuliko hivi sasa. Naishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutoshindana sana katika soko la fedha la hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, Hati Fungani za Serikali kwa mwaka mmoja riba ni asilimia 9.2 na ukienda kwenye mabenki yetu hasa CRDB na NMB riba ni 9.5. Maana yake ni nini? Ni kwamba katika hali ya kawaida wawekezaji wengi wa kifedha kama hivi watazipeleka fedha Serikalini na watawatia njaa kidogo. Naomba nitumie neno ambalo siyo zuri sana, lakini ku-*suffocate private sector*. Hili ni jambo ambalo inabidi tuliangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili kubwa ambalo ningependa kulizungumza ni kuhusu mapato ya Serikali. Hapa najipeleka moja kwa moja katika mashauri ambayo yamekwama katika hizi Mahakama ya *TRAB* na *TRAT*. Hili neno lilileta maneno kidogo. Ni zile Bodi ya Rufani ya Kodi na Mahakama ya Rufani ya

Kodi. Kwa haraka kesi ambazo ziko na hii ni kwa mujibu wa *CAG;* kesi ambazo ziko kule kwenye *TRAT* ni kuanzia mwaka 2018 hadi 2022 kuna jumla ya kesi 36, thamani yake zinazoshindaniwa ni shilingi bilioni 90. Ukienda kwenye *TRAB* utakuta kuna kesi zipatazo 287 na thamani yake ni shilingi trilioni 2.2. Maana yake ni kwamba, hizi Fedha za Serikali zingekuwepo na utaratibu mzuri wa *TRA* kuelewana na wafanyabiashara katika ufanyaji wa mahesabu, fedha hizi zingeingia katika Bajeti ya Serikali. Tunavyozichelewesha kuziweka kule maana yake tuna wa-*suffocate* tena wafanyabiashara, lakini tunatengeneza *uncertainties;* kutokuwa na uhakika katika kufanikisha *private sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka, nashauri Serikali itengeneze mifumo ambayo itawafanya wafanyabiashara watambue kwa uhakika kodi zao ambazo zinatakiwa zitolewe mapema kabisa. Kwa sababu kuwavizia wafanyabiashara katika zile *audits* ambazo zinafanyika mnawapa mzigo wafanyabiashara. Hiki siyo kitu chema kabisa katika… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napongeza Serikali na niwatakie kila la kheri. Mwenyezi Mungu ajalie hiki kitu kiweze kupita. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Jafari Chege ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, kwa kuwasilisha hotuba zao zote mbili hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba niseme, kiongozi mzuri hajitengenezei ubinafsi. Narudia, kiongozi mzuri yeyote duniani hajitengenezei ubinafsi, bali anatengeneza mambo ya kuleta mabadiliko chanya ya maendeleo kwa watu anaowaongoza na kuleta *legacy*. Sasa hii imejidhihirisha kwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutengeneza na kuwafikia wananchi wa kawaida vijijini. Kuwatengenezea huduma za kijamii, shule, afya, maji na barabara na anatengeneza *legacy* kwa kuwafikia wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo anatengeneza shule na tumeona wote katika kila jimbo madarasa yamejengwa vizuri, anajenga vituo vya afya na hospitali. Naamini kwamba ukitaka kumfikia mwananchi wa kawaida maskini kijijini, wape elimu watoto wake. Ukitaka kufikia familia maskini kijijini, wape mazingira bora ya afya katika maeneo yao. Haya ndiyo anayoyafanya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa narudi kwenye hoja, kwenye suala la Mpango ulio mbele yetu. Uchumi duniani unapodorora unaathiri pia Taifa letu. Tunaambiwa sasa hivi utaathiri upatikanaji wa fedha za mikopo, kupanda kwa riba ya mikopo huko duniani na uwezekano wa kupungua au kukosa misaada kutoka katika nchi hizo. Nchi hizo marafiki zetu kihistoria, ambao wamekuwa wakitupa misaada na mikopo, Marekani, Japan, Uingereza, Canada, Ujerumani, Ufaransa, Italia, Hispania na maeneo mengine ya Ulaya; kiwango cha ukuaji wa uchumi wao kinatarajia kushuka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2022 mpaka asilimia 1.5 mwaka huu 2023, lakini ukuaji wa uchumi utaendelea kushuka tena mwaka 2024 mpaka asilimia 1.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo yote lazima tuyatafsiri kwa kukaza mkanda na kujiimarisha katika kazi zetu na kuona mpango wetu huu unajielekeza katika kukabiliana na hali hii ya mabadiliko ya kudorora kwa uchumi duniani hasa kwa nchi hizi nguli za magharibi.

Kwa kuwa watu hawa tumekuwa na mahusiano nao mazuri, ya mikopo na misaada mbalimbali na sasa riba kwao zimepanda za mabenki yao, lakini pia hali ya ukuaji wa uchumi wao umeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie, je, ni nini itakuwa athari yake kwetu sisi kama Tanzania, lakini tukikopa pia kwa wakati huu athari yake itakuwa nini kwa riba kubwa kwa nchi zile? Mpango utuoneshe maeneo yale ya misaada kutoka kwao tutakayokosa katika kipindi hiki yatatuathiri kiasi gani na tumejipangaje kuziba pengo hilo la misaada ambayo tunaipata kutoka kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, tuongeze uzalishaji mali katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji wa kilimo, lakini bidhaa mbalimbali zitakazoongezwa thamani kuuza nje. Tuongeze thamani katika bidhaa mbalimbali, nitatolea mfano katika mazao haya ya biashara ya kilimo, lakini kutokana na muda nitalisemea moja la tumbaku. Zao la Tumbaku limekuwa ni zao ambalo linauzwa kwa dola. Kwanza ni zao la kimkataba, mkulima kabla hajaingia shambani, unafanika mkataba wa ununuzi na ununuzi ule ni kwa dola lakini zao hili pia lilishanunuliwa kwa mkulima kwa dola, linaenda kuwa *processed*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viwanda hapa vya ku-*process* tumbaku, *semi-product* ambao wanafanya *blending* ya ile tumbaku. Ikishafanyiwa *blending*, asilimia kadhaa kubwa inauzwa nje ikiwa imekuwa *processed* kiasi kwa kufanyiwa *blending*. Inauzwa nje kwa dola lakini asilimia nyingine inauzwa ndani katika viwanda vya ndani, inatengeneza *final product* ambayo ni sigara. Pia, nayo hiyo sigara inauzwa nyingi asilimia kubwa nje kwa dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi nchi yetu sasa hivi tuna uhaba wa dora na tunakazania sana tupate dora. Tulitazame sana zao hili. Zao hili ni zao la kimkataba na kwa mwaka huu tu limeuza zaidi ya dola milioni 400. Takwimu zaidi sina za uhakika, lakini Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, watafute takwimu vizuri. Mwaka huu tumeuza tumbaku kwa dola

nyingi, lakini mwaka huu pia msimu unoakuja tumeingia mkataba wa uzalishaji wa tani nyingi zaidi za tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu hili zao tuliangalie kwa karibu sana, kwa sababu kama nilivyosema, linauzwa kwa dola kwa mkulima, linapokuwa *processed* linauzwa nje kwa dola, lakini pia linapokuwa *processed* hapa na kupata *final product* ya sigara nyingine kwa wingi, zinauzwa nje kwa dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachoomba, tuliangalie hili zao katika uzalishaji wake. Leo hii zao hili, mbolea yake inalipiwa ruzuku. *NPK* hailipiwi ruzuku, inauzwa kwa bei ghali Sh.160,000 mpaka Sh.170,000, lakini mbolea nyingine zozote za mazao, zinapewa ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, Serikali itoe ruzuku katika zao la hili la tumbaku ili tuweze kupata dola nyingi zaidi. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, aliwahi kutuambia hapa Bungeni, ukitaka kula, lazima uliwe. Kwa hiyo, haya madola yote wanayoyasema haya ili Serikali iyapate mengi zaidi, ni lazima tuliwe. Lazima tutoe ruzuku ya *NPK* kwa zao la tumbaku. Pia, naomba mpango ujielekeze kwenye hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunashukuru sana mpango hapa umetueleza katika Aya ya 31, Ukurasa wa 14, mafanikio yale. Serikali imetoa ruzuku katika mazao ya kilimo. Pia, ongezeko la uzalishaji wa mazao, limeongezeka kutoka tani milioni 17 mpaka 20, lakini pia wameimarisha masoko. Wameyasema wazi *NFRA* wamenunua mazao. Tunashukuru sana imenunua kweli na mazao mchanganyiko wamenunua *NFRA,* lakini bado wakulima walikuwa wanawadai Serikali bilioni 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni kipindi cha wakulima kwenda kulima na kilimo kinataka maandalizi na maandalizi ni fedha. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali, nashukuru mpaka Ijumaa Serikali imeshalipa bilioni 19 kwa wakulima waliouza mahindi kupitia

*NFRA*. Sisi Mkoa wa Ruvuma tunadai bilioni 9.9 na tumeshalipwa bilioni 4.0, bado wakulima wanadai bilioni 5.9 (Bilioni tano na milioni mia tisa). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali kupitia *NFRA* iwalipe wakulima hawa warudi tena shambani waweze kuzalisha, mazao yaweze kuongezeka. Kwa hiyo, tunaomba sana hili walichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine. Mipango yote hii tunayoifanya, yote inahitaji usalama. Ni lazima eneo la usalama tulizingatie sana katika mipango yetu ya Taifa. Tuhakikishe kwanza tunalinda mifumo yetu ya fedha. Eneo hili la usalama tuhakikishe tunalinda mifumo yetu ya fedha kwani sasa hivi kumekuwa na ushamirishaji mkubwa sana wa wizi kupitia mifumo yetu ya fedha za Serikali. Kwa hiyo, lazima kuwe na fedha za ziada ambazo zitakuwa zinalinda wakati wowote kubadilisha mifumo ili kukabiliana na wizi huu wa fedha za Serikali kupitia mifumo. Kwa hiyo, tunaomba sana uhalifu wa mifumo yetu ya Fedha za Serikali na mwingine umeongezeka sasa hivi ambao udhibiti wake… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, lakini naomba unipe nusu dakika. Mifumo ambayo udhibiti na ufuatiliaji wake wa mifumo hii, unahitaji teknolojia na teknolojia inahitaji fedha. Kwa hiyo, sasa katika mpango huu ni lazima tuweke fedha za kulinda mifumo yetu kwa ajili ya usalama wa fedha za Serikali na kuzuia hawa wahalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Chege, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, ajiandae.

Kabla ya hapo Mheshimiwa Musukuma, Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo la wageni walioko Bungeni muda huu.

Tunao wageni 75 wa Mheshimiwa Hamad Hassan Chande ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Kojani, Mkoa wa Mjini Magharibi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga ambao ni wapiga kura kutoka Jimbo la Kalenga Mkoa wa Iringa, ahsante karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 84 wa Mheshimiwa Ally Juma Makoa ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari Kwapakacha kutoka Wilaya ya Kondoa Mjini, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 41 wa Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos ambao ni Taasisi ya Wanawake na Watoto kutoka Zanzibar, ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe pongezi kubwa sana kwa Serikali kwa Mheshimiwa Rais kwa kusikiliza maoni ya Wabunge na kutoa maamuzi magumu kwenye *KADCO* ambayo imetesa miaka yote ya Ubunge wangu miaka Nane tunajadili *KADCO*, hongera sana Serikali na tunajipongeza kama Wabunge.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kumteua Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kuwa Waziri wa Mipango, mimi nakuamini sana Mheshimiwa Kitila Mkumbo kwa *research* wewe ni bingwa kabisa. Mheshimiwa Rais amefanya vizuri amewakabidhi fedha na akawakabidhi na mipango, ninyi wote mnatoka Iramba, *ndoho mayo* mkiharibu tutauana, nina imani mtafanya vizuri na wapiga kura wenu tunawategemea na kule kwa shemeji zangu wanajua sasa mambo yanaenda vizuri kwa sababu mmekabidhiwa wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Kitila Mkumbo kwa mpango mzuri lakini lazima tukushauri, kupanga siyo makaratasi, mara nyingi tumekuwa na mipango lakini mipango inakuwa haitekelezeki. Najaribu kuona vitu ambavyo baadae tutakuja kukusulubu humu kukuuliza, nakupa tu mfano mdogo. Kwa mfano, unasema tunajenga vituo vya gesi kwa ajili ya ku-*refuel* magari, lakini najiuliza wenzangu labda mnaweza mkanisaidia tunayo magari haya yanayotumia gesi Tanzania, kwenye takwimu tuna magari sijui 3000 na kitu, ni sawa. Lakini kweli mnaona jinsi ambavyo yale magari yanavyobadilishwa kutoka mfumo wa mafuta kwenda kwenye mfumo wa gesi, yaani inakushawishi nini mpaka ukaanze kujenga vituo kwa *design* ile ya magari yaliyoko Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu ametupa bahati ya kuwa na maliasili, maliasili kama tumegundua tuna gesi ambayo inaweza kutumika kwenye magari, kwa nini Waziri wa Mipango, usingeleta mpango hapa tukachukua wataalam tukawapeleka kusoma huko Japan, halafu wakaja na teknolojia ndiyo tukaanza kuliko kukurupuka. Nakupa mfano, ukipanda kwenye gari ambalo limebadilishwa mfumo wa mafuta kwenda kwenye gesi limewekewa *drum* huko kwenye buti na Wajapani walivyotengeneza gari lile buti ni kwa ajili ya kuweka mabegi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najiuliza nyinyi wenzetu Mawaziri kidogo hadhi yenu ni kubwa mnavyoanza hii teknolojia ya gesi, mimi

nilikuwa nashauri muanze na gari za Serikali za Mawaziri tuwawekee yale ma-*drum* ya gesi kule nyuma, halafu usafiri na hilo gari hupati hata usingizi! Naona kabisa tunaenda kupoteza hela kwenye vitu ambavyo haviwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu nchi zilizoendelea wanaotumia gesi wanatoa oda ya magari yao kwamba yanakuja *special* kwa ajili ya gesi, lakini angalia hata hayo malori ya Dangote mkikutana nayo watu wanachomelea ma-*drum* yanawekwa nyuma ya *cabin,* yaani kwanza gari lenyewe linakuja limeshapoteza na uzito ile *capacity* yake, kwa hiyo, mimi naona kabisa tunaenda kufeli tutaanza lakini hawa watumiaji wenyewe kwa sababu sisi wengine tunajifunza kutoka kwa Serikali, kwamba Serikali inapoona gari fulani ni zuri, kwa mafano V8, tukiona mmekuwa nazo nyingi Serikalini na sisi tunakimbilia kwa sababu Serikali imeshaona ni gari zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri gari la Waziri wa Fedha, kwa sababu wewe ni Mchumi na Waziri wa Mipango, kwa sababu wewe unatupangia tukufungie gesi kwenye buti lile *drum* liwe mfano kwa sababu wewe utabana matumizi, kuliko kwenda kuweka rehani maisha ya Watanzania kwa kuweka teknolojia za kijiweni halafu Serikali inaingia gharama kwenda kupitisha bajeti ya kujenga vituo, naona kama hatuendi sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza hapa Mbunge wa Ngorongoro, amezungumza suala la ng'ombe, ndugu zangu mimi huwa nazungumza kila siku ng'ombe huwa hawaongei lakini wana machozi, sisi tuliokuzwa na ng'ombe tunafahamu, Waziri rafiki yangu sana Mheshimiwa Kairuki, hili suala ukisimama hivi unavyosimama, mimi niliwahi kulia humu nikamlilia Mheshimiwa Magembe aliekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, hakumaliza siku tatu akala kichwa, akaja na mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba busara kwenye suala la watu maskini, hivi tunahitaji shule gani kuona kwamba watu wetu wanaonewa? Nimemsikiliza kaka yangu *AG*, anasema ukomo,

Mahakama ina ukomo, Mahakama ya Mkoa, hivi mtu wa Darasa la Saba anayefuga ng'ombe unamuambia hicho kiingereza alichozungumza hapo cha ukomo wa Mahakama, nani anaelewa hayo mambo? Huku akienda anaambiwa tunafanya uchunguzi, kumbe ninyi mnashughulika na kuuza ng'ombe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu jiulize yaani hukumu imetoka Tarehe 31, halafu mnauza ng'ombe Tarehe 01. Maana yake dalali alikuwepo siku hiyohiyo wala ile hukumu haikuwa na *alternative* lipa faini, yaani ni vitu ambavyo, kwa kweli unafika mahali unajiuliza pengine hii nchi ni ya matajiri tu maskini hatutakiwi kuwa Tanzania! Haiwezekani...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Waitara achana na taarifa kwanza …

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, kuna taarifa kwa Mheshimiwa Waitara, kwa ufupi kabisa.

**TAARIFA**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Musukuma, namuongezea kwamba *TANAPA* hao ndiyo walikamata ng'ombe, *TANAPA* walipeleka Mahakamani, *TANAPA* ndiyo walipewa hukumu kwamba wameshinda, *TANAPA* wamepiga ng'ombe mnada na ng'ombe mmoja amenunuliwa chini ya shilingi laki moja kila ng'ombe mmoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hakuna taarifa juu ya taarifa. Mheshimiwa Musukuma taarifa ya Mheshimiwa Waitara, unaipokea.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea na ninaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ndiyo kasi inaingia namba tatu hebu pumzikeni kwanza, wekeni *pause* hizo taarifa kuna wanaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahitaji kuwa na elimu ya namna gani kugundua kwamba hii ni dili kuanzia huko *TANAPA*, na watu wetu wanakuwa maskini. Halafu unapanga mpango huo mpango ukawafaidishe wakina nani? Mnataka watu wote sasa muwalishe na *TASAF*, hii kitu hakiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri achana na mambo ya kusema nisome sheria, tunajua wewe ni Mwanasheria mzuri lakini ukisimamisha Wabunge humu ndani wanaokaa jirani na mapori siyo mtu wa kwanza leo, wakikosa hela wanaenda kuswaga ng'ombe wanaziingiza kwa bunduki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiulize hukumu imetoka tarehe 31 haina hata *notice* kwamba mlipe faini au ziuzwe, zimeuzwa kesho siku hiyo hiyo zimepakiwa zimeenda Dar es Salaam, unahitaji kuwa na *degree* kujua hiyo mipango? haiwezekani! Ni lazima Mheshimiwa Waziri, toka kwenye boksi hapo ukienda hivi, wafugaji sisi huwa tuna kitu chetu tukitoa machozi Mungu atatusikia huko aliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Kaka yangu Waziri wa Mipango, niambie unahitaji kuwa na shule gani kwamba watu tunafeli, angalia Dar es Salaam, mna mwendo kasi, kuna *DART* na kuna *UDART*. *DART* anamiliki lami, ile barabara ambayo haifi miaka 100, halafu anamiliki mifumo ambayo inaweza kusimamiwa na TAMISEMI na mtu mmoja tu, unaweka Mkurugenzi, unaweka *Chief*, unaweka ma-*V8* na makorokoro mengi kwenye kitu ambacho hakizalishi. Mwisho wa siku kila mtu anasubiri mshahara tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo mmeua kwa ajili ya kupiga, magari yenyewe yameisha, sasa kama kuna mtu mmemkodisha barabara kwa nini huyu msimamizi *DART,* fukuza wote pale, weka hapo mtu mmoja tu, kwa nini tunasimamia *POS* nchi nzima unashindwaje kusimamia Mfumo wa *U-DART*? Hicho ni kitu ambacho mnatengeneza mipango mizuri halafu mashirika yetu hayaendelei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushauri pamoja na Waziri wa Mipango, fukuza wote pale, unaenda unachukua wazee wastaafu umedumbukiza ma-*V8* mpya kwenye kitu ambacho hakizalishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza suala la bangi. Leo nazungumza mara yangu ya tatu, mnaona kama naongea vitu vya ajabu, nami sishabikii bangi ya kuvuta. Huwa nawaangalia Polisi wanafyeka kule na ma-*TV,* lakini hiki ni chanzo. Angalieni Canada, Colombia, Pakistan, dunia nzima inapiga kelele na madawa ya kulevya wao ndiyo chanzo cha mapato. Sasa tunafyeka kwa ajili gani, tungedhibiti watumiaji, nchi jirani wanatumia, sasa kwa nini tunazuia, unaenda unafyeka unaonyesha na kwenye *TV*, unafaidika kitu gani wakati hilohilo zao ndilo linaweza kukuingizia kipato kutoka nchi ya Jirani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kidogo suala la *CAG*. Uliona mchakato wa CAG ulivyokuwa, nashauri ili tuende vizuri tunapofika kipindi cha kuhoji wale Wakuu wa Taasisi, kwa sababu huu ni Muhimili unajitegemea siyo wa kihuni, tuna Serikali, tunayo Mahakama na tunalo Bunge. Ninashauri ukiondoa wale Viongozi Wakuu wa Serikali wanne wa juu, hawa wengine bila kuangalia nyota au ngao za mabegani, hakuna kuja humu na ma-*bodyguard*, watu wanaogopa kuwahoji, kwani nani ataingia na bunduki huku ndani? Tunakuja tumekaguliwa mpaka mlangoni pa kuingia, sasa mtu anaitwa kuja kuhojiwa, mfano ana ngao mbili hapa mabegani, anakuja na walinzi nane mnanyanyuliwa mpaka na kwenye viti utamhoji vipi huyo mtu? Mimi nashauri wakifika pale *protocol* zao

ziishie kule, maana hata sisi tukiwa watuhumiwa kwenye taasisi zao hatuendagi na mbwembwe tunaenda mmoja, waje humu watu wawahoji bila kuwa na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Kanda ya Ziwa na nimeshangaa sana Waziri wa Mipango, umenisahau. Hivi ninyi watu wa Kanda ya Ziwa labda huwa mnatuona kama sisi ni Waganda au namna gani? Uwanja unaoingiza pesa Tanzania ukitoa Uwanja wa Dar es Salaam, Uwanja wa pili ni Uwanja wa Mwanza, kigugumizi ni cha nini kutuwekea *International* Airport Mwanza, mnieleze. Halafu mnakuja na mpango, nawaangali na Wabunge wenzangu wa Kanda ya Ziwa mnapiga makofi, sisi tunakuja kusindikiza kila siku humu ndani? Uwanja wa Ndege wa Mwanza unajiuza, una wateja tuna nchi jirani zinategemea pale. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mnajenga reli …

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** *Brother*, tuliza basi.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, muda wako umeisha naomba umalizie.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba namalizia huyu ameingilia muda wangu, kama unataka tuelewane ukinichenga hapa Mheshimiwa Waziri wa Mipango, mwaka huu ni mwisho kutudanganya mlisingizia uwanja umekataliwa na Ilemela, mmerudishiwa na hela bilioni 4.5, tunaomba kwenye bajeti inayokuja tuone hapa unakuja na hela, ukija na swaga tutazinguana. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, ahsante sana. Mheshimiwa Jafari Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Londo, Mheshimiwa Esther Matiko, ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kutoa mchango wangu kwenye Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa, niungane na wenzangu kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuridhia na kukubali ushauri wa Bunge wa kutenganisha Wizara hizi na hatimaye kutuundia Wizara mpya ya Mipango na Uwekezaji. Kipekee kabisa nichukue nafasi kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuliona hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimshukuru kwa kutupa mtu ambaye ni sahihi, tukiamini kabisa kwamba lengo na dhumuni la Wabunge tulikuwa tukilizungumza kuhusiana na Mipango kapewa mtu ambaye ni sahihi na sasa imani yetu ni kwamba Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo atatuvusha kwenye hili. Akiamini kabisa kwamba Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji inapaswa kuwa ndiyo dira, mwelekeo na *catalyst* ya kutuonesha wapi tunatakiwa kwenda kama nchi na isiwe mipango ya mwaka mmoja peke yake naamini kwamba itakuwa ni mipango endelevu ya miaka nenda rudi, yote hiyo ni kutuonesha kwamba kama Taifa tunapaswa kuelekea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, wewe ni msomi nafikiri kwa sababu wewe ni *Professor*, unajua, hakuna mipango mizuri ambayo inaweza ikafanyika, kwa uchache tu kwanza, bila kuzingatia *research*. Pili, bila kuoanisha na kutazama sera *(policy)* mbalimbali zinazoshabihiana kwenye Wizara na Sekta husika, hili ndilo inawezekana ikawa ufaulu mkubwa sana wa Wizara hii kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, mchango wangu utajikita hapa. Kwanza, ambalo ningetamani nikushauri ni kwamba pamoja na kwamba unaweza ukawa na mipango mizuri uliyotuwasilishia leo hapa lakini mipango yako ningekushauri Mheshimiwa Waziri iende ikatazame sera mbalimbali za kisekta hasa sekta za uzalishaji, ambazo kimsingi zitashabihiana na kuku-*boost* kwenye Mpango wa Taifa 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera mbalimbali ambazo zimepitwa na wakati haziwezi kusaidia Mpango wa Taifa linalokusudia kwenda miaka mitato, kumi kwenda mbele. Mfano, kuna Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995, sera hii kwa namna ambavyo ameizungumza Mheshimiwa Waziri, kwenye wasilisho lake sera hii inagusa maeneo mengi. Migogoro inayozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, ambayo iko *TANAPA*, TAMISEMI na Wizara ya Ardhi inagusa wananchi wanyonge ambao ni wananchi maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna yoyote kama Taifa likiwa lina mipango mizuri inayogusa wananchi maskini bila kutazama namna ya kutatua ile migogoro hatuwezi kupata ile furaha tunayoitamani kutoka kwa wananchi wetu tunaowawakilisha. Kwa hiyo, ningetamani sana Mheshimiwa Waziri, kama nilivyosema kwa sababu Wizara yako ni *catalyst* iende ikatazame namna ya kufanya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hauwezi kwenda na mipango ya miaka mitano mbele tunakwenda kuzungumzia 2030, huku una sera ya mwaka 1995 yaani miaka 18 iliyopita kwa *population* ambayo ilikuwa haifiki milioni 20 tuitumie kupanga mipango ya nchi ya kwenda zaidi ya mika 10 mbele. Kwa hiyo, ningetamani Mheshimiwa Waziri, uende ukakae na utoe ushauri kabisa kwenye Wizara za Kisekta hizi ambazo kimsingi ndizo zinapaswa zikusaidie wewe kuhakikisha mipango inakwenda kwenye Wizara hii, wafanye maboresho ya sera ambazo zimepitwa na wakati, ikiwemo na hii Sera ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, Mheshimiwa Waziri kwanza utapunguza urasimu kwa maana ya kwamba utaboresha Sekta ya Uwekezaji ambayo iko chini ya Wizara yako. Pili, utakwenda kupunguza migogoro ya miingiliano kati ya Wizara zote tatu ambazo kimsingi ndiyo wananchi wanyonge wanakotoka. Niliwahi kusema hapa *GN* ya eneo moja inaweza likatolewa na Wizara tatu tofauti, yaani TAMISEMI, inatoa *GN* ya kuanzisha kijiji, Wizara ya Ardhi inatoa *GN* ya kutengeneza mipaka lakini vilevile ukienda kwenye upande wa maliasili nao wana *GN* yao ya maeneo ya hifadhi. Kwa hiyo, kule kunakuwa na kelele nyingi Mheshimiwa Waziri, kwanza kelele za wananchi maskini wanaozungumza haziwekwi, lakini wewe pia Wizara yako kwa maana ya uwekezaji hauwezi kuwa na tija kama maeneo haya yatakuwa hayajafanyiwa kazi. Kwa hiyo nikuombe sana ulione hili namna ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumzia mipango sehemu ya ardhi iliyopimwa ni zaidi ya asilimia 25 peke yake, lakini mipango unayoizungumza inakwenda kupangwa kwenye eneo hilo hilo la ardhi, kwa hiyo, ni lazima uone namna ambayo unaweza kupanga eneo hili likapimwa kwa maana ya nchi nzima ili mipango yako iende sambamba na kuweza kuleta faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili Mheshimiwa Waziri ambalo ningekushauri, Bunge lililopita tulipitisha hapa Itifaki ya Huduma za Kibiashara za Nchi za Kusini mwa Afrika, ningeomba uone namna ya Itifaki hii kama Waziri wa Uwekezaji na Waziri na Mipango kutoa elimu kwa wananchi wazawa, wawekezaji wa nchi hii ili waone namna ya kuchangamkia hii fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili Mheshimiwa Waziri, ujiandae namna ambavyo Nchi wanachama ambazo zimekubaliana kufanya shughuli za kibiashara kwenye nchi hizi, namna zitakavyowekeza Tanzania na namna wananchi watakavyoweza kunufaika kama Tanzania. Mara nyingi tumekuwa tukipitisha Itifaki hizi lakini tunakosa mtu halisi wa kusimamia na kutafsiri nini

ambachoo Bunge limekusudia. Kwa hiyo, ningekuomba Mheshimiwa Waziri, uone namna ya kulifanya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu Mheshimiwa Waziri, mipango yako yote ningetamani Mipango ya Taifa lazima iendane na Mipango ya Wizara, Mipango ya Taasisi na Mipango ya Halmashauri. Hatuwezi kuwa na Mpango wa Taifa halafu huku chini kwa maana ya Taasisi, Halmashauri nazo zina mpango tofauti na mpango ambao unaendana na wewe. Kwa hiyo, kama Halmashauri zinaandaa mpango maana yake ni lazima zioane na ule Mpango wa Taifa, hatuwezi kuwa na mpango mdogo Halmashauri ambao kwako wewe hausimamii na hauna namna ya kuusimamia, maana yake tutakuwa tuna mipango mingi tu, kwamba huku Taasisi zina mipango yao lakini sisi tuna mpango mkubwa wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho Mheshimiwa Waziri, ninaomba kwa kuwa tayari tunakwenda kuinua uchumi ninayo barabara yangu ambayo nimeizungumza sana, siyo barabara yangu ni barabara ya Mkoa wa Mara, kimsingi barabara ile inatuunganisha kati ya Kenya na Tanzania. Barabara ile inapita katika Jimbo langu, nimezungumza leo nilipokuwa nauliza swali nilikuomba Mheshimiwa Waziri, barabara hizi ambazo ni kiungo cha uchumi kati ya nchi na nchi, kati ya Mkoa na Mkoa na Wilaya na Wilaya zipewe kipaumbele katika uwekezaji wa mpango ili angalau tuone namna ambavyo zinaweza kuinua uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi barabara za ndani zipo lakini barabara kubwa zinazounganisha kati ya nchi na nchi, Mheshimiwa Waziri uone namna ambavyo mnaziwekea fedha kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapo ziwekewe fedha ili angalau ziweze kuinua uchumi kutoka maeneo jirani na uchumi wa wananchi wote kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Chege, ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiku.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuendelea kuchangia Mpango.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Rais wetu, Mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa utekelezaji mzuri wa bajeti hii ambayo tunaendelea kuisimamia katika utekelezaji wake, lakini kwa nafasi nyingine pia ya kushauri Serikali maeneo muhimu ya kuwekeza katika bajeti inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mikumi, nimshukuru Mheshimiwa Rais na Bunge lako kwa msaada mkubwa ambao mmempatia mtangulizi wangu Mbunge wa Jimbo la Mikumi, Mheshimiwa Joseph Haule (Profesa Jay). Kimsingi kwa niaba ya wananchi wa Mikumi tunashukuru sana kwa mapokeo lakini pia utayari wa Bunge hili ku-*support course* ambayo anaenda ku-*fight* kwa ajili ya watu wenye matatizo ya figo, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ambayo tunaendelea nayo na mpango huu ambao tunaujadili sasa, tunaujadili katika wakati ambapo dunia ipo katika hali ya sintofahamu kiuchumi na kisiasa. Changamoto kubwa za kimfumo zinaendelea dunia nzima. Tanzania siyo kisiwa, nasi pia ni sehemu ya dunia hii. Tunaathirika moja kwa moja ama kwa namna moja ama nyingine. Ni vyema mipango yetu na bajeti yetu katika maandalizi yake, tukaangalia mwenendo wa dunia unavyoenda na jinsi gani unaenda ku-*impact* watu wetu hasa wakulima ambao ni 70% ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyozungumza, kuna vita *Middle East*, kuna vita Ulaya, kuna vikwazo kila sehemu, lakini kimsingi tunaona kabisa kila dalili kwamba mfumo wa soko huria kwa maana ya *policies* na *capitalism* ambapo sisi ni sehemu ya

dunia hii na mifumo hii ya kiuchumi inasimamia shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa katika dunia yetu tunaona imetetereka. Kwa sababu siri ya mfumo wa kibepari na soko huria ni ulinzi wa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikwazo na *confiscation* ya *private property* ambayo ndiyo roho ya ubepari, roho ya mfumo wa soko huria; tunaona Warusi mali zao zinataifishwa kwa sababu tu ni Warusi, kwa sababu tu Werikali yao imeingia vitani. Yeye sio mwanasiasa, sio mshiriki wa Serikali, wala hajashiriki katika maamuzi ya kwenda vitani, lakini mali zake zinabinafsishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni ndwele ambazo zinaashiria jambo kubwa kwa sisi Waafrika ambao kazi yetu ni kuchukua fedha ndani na kwenda kuwekeza nje. Fedha hizo hazitakuwa na maisha kesho kwa sababu uchumi wa dunia yetu wote tunaujua, umejengwa katika hali ya *primitive accumulation of capital*. Sheria zimejengwa kwa ajili ya ku-*confiscate* mitaji ya watu kwa njia ambayo ni *legally*. Kwa mfano hiyo ya kuweka vikwazo na kuchukua mali za watu binafsi kwa makosa ya Serikali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linatupeleka kwenye kile ambacho Francis Fukuyama alizungumzia *Clash of Civilization,* kwamba baada ya migongano kati ya Ubepari na Ujamaa, kitakachofuata ni migongano ya imani, kiitikadi na kimtazamo. Ndiyo maana tunaona dunia hailali kwa sababu damu ya watu fulani inamwagika, lakini wakati huo huo inalala damu ya watu fulani ikimwagika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria na mipango na mifumo imejengwa kwa ajili ya kumuumiza asiyenacho. Ndiyo maana mwaka 1837 Bunge la Uingereza lilipitisha sheria ya kuzuia biashara ya utumwa, pia ilipitisha sheria ya ku-*compensate* wale Waingereza wote ambao wanakwenda kupoteza mali zao kwa maana ya watumwa, yaani Waafrika katika makoloni ya Mwingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walitenga zaidi ya pauni 20,000,000 ambayo ni sawa sawa 40% ya bajeti yao, sawasawa na 5% ya *GDP* ya nchi kwa ajili ya ku-*compensate* watu ambao walikuwa wanamiliki watumwa. Deni hilo lilikuwa ni kubwa na la kihistoria, na Serikali ya Uingereza kwa maana ya walipakodi wa Uingereza wakiwemo Wabunge ambao wamesoma Uingereza, wameshiriki kwenye kulipa deni hilo mpaka 2015, ndipo wamemaliza kulipa deni hilo. Mwaka 2015, maana yake ni miaka saba iliyoisha, ndiyo wamemaliza kuwalipa wale ambao walikuwa wanamiliki watumwa kuwaachia huru watumwa hao. Kwa hiyo, tumeshikiri katika kampeni ya kuwapa uhuru babu zetu na bibi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ilipitishwa kwa ajili ya ku-*compensate loss* kwa hawa wamiliki wa watumwa, lakini katika kuwajengea mitaji Waingereza, mitaji ambayo sasa hivi tunaitumia kama mikopo ambayo tunailipa kwa riba kubwa kwa nchi zetu. Hilo linaonesha kwamba kuna umuhimu wa sisi pia kwa bajeti yetu tusione aibu kutenga fedha kiasi cha kutosha kwa ajili ya kuwaweza watu wetu kwa kisingizio chochote kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutegemea Sheria za Kimataifa kutupa fedha ama *leeway* ya kupendelea watu wetu katika ku-*accumulate capitals* hazitatufikisha mbali. Pamoja na hayo yote, naomba nizungumze kitu kimoja. Sheria nyingi ambazo zipo, hata hizi Mahakama za Kimataifa ambazo Serikali inakosa haki na tunapaswa kulipa mabilioni ya hela, zinaturudisha nyuma badala ya kutupeleka mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo tunalipa kama *compensation* kwa sababu ya kuvunja mikataba ni aina nyingine ya unyonyaji ambayo imejikita katika mifumo ya unyonyaji ya dunia yetu. Hatuwezi tukaa hapa tukapanga mipango ya kukusanya fedha za walipakodi wetu kwa ajili ya kulipa fidia au kwa ajili ya kuendelea kuimarisha mifumo ya kinyonyaji duniani. Ni lazima mipango yetu iangalie pia jinsi ya kudhibiti mianya ambayo

inavujisha fedha zetu kwa ajili ya kuimarisha masoko ama mitajji ya mabepari. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dennis, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa Taarifa Ndugu yangu Londo kada wa chama chetu kwa maneno mazuri sana anayozungumza. Tusipochukua tahadhari sasa dhidi ya watu wanaotuingiza kwenye mikataba ambayo sasa tunakuja kudaiwa kupitia Mahakama za dunia ambayo sasa ni kiwango cha mabilioni ya fedha, kesi nyingi tumeshapigwa na kesi nyingine zipo njiani na tutashindwa, lakini waliotuingiza kwenye hasara hizo bado wapo kwenye Utumishi wa Umma na hawaondolewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri umefika wakati sasa tukilipa fedha za mikataba hii, wahusika wenyewe wachukuliwe hatua ikiwa ni kuondolewa wao na wale madalali waliokuwa wanapita Wizarani kuwaombea kazi hao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dennis Taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko tunakoenda, hatuwezi kubeza kilimo, lakini hatuwezi kukaenenda na mwenendo huu tukategemea matokeo ya tofauti. Tuna ekari zaidi ya milioni 26 ambazo tunaweza tukamwagilia kilimo cha umwagiliaji, lakini tuna *highly suitable land*

ekari zaidi ya milioni 2.3. Kiasi ambacho tutatumia sasa hivi kwa ajili ya umwagiliaji ni 1.6%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama 70% ya Watanzania wamejikita kwenye kilimo, ni vizuri bajeti yetu ikajikita kuona ni namna gani tunaenda kumkwamua huyu mkulima maskini wa Kitanzania, kilimo chake kiongeze tija kwa kumpunguzia gharama za uwekezaji, kwa maana ya kumjengea miundombinu ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za *TARURA* ambazo zinaunganisha mashamba na masoko, mashamba na barabara kubwa ni lazima zipatiwe bajeti ya kutosha. Mwaka jana 2022 tulipitisha hapa shilingi bilioni 11 kama dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishuhudia mvua zikinyesha, zikiondoa madaraja na Barabara, fedha hizo sidhani kama zilienda. Mwaka huu kuna fedha ambazo tulipanga kwa ajili ya ujenzi wa Barabara, kuna zaidi ya shilingi bilioni 350 ambazo zilipangwa kwenda, sina hakika kama zimeenda. Barabara hizi ni muhimu, siyo kwa ajili ya *luxury* ya wakulima, ni kwa ajili ya kumpa mkulima uhakika wa kuondoa mazao yake mashambani kwenda sokoni ili Serikali ipate mapato yake na huyu Mtanzania apambane na umaskini wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ambacho tunakiona katika sekta ya kilimo, tuna wafanyabiashara wakulima zaidi ya milioni mbili. Asilimia 94 ni wazalishaji, ni 1.4% tu ambao unaweza kusema kwamba wanashiriki kikamilifu katika zoezi la kuongeza thamani mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ndiyo msingi kwa wakulima. *A certainty* ambayo inatokea inatokea migogoro ya mipaka, *a certainty* ambayo inatokea katika suala zima la umiliki wa ardhi katika maeneo mbalimbali, siyo suala la kupuuza. Kama tunataka tumwezeshe Mtanzania kiukweli, ni lazima tusimamie migogoro yote

na vyanzo vya migogoro ikiwemo kuchukua hatua watumishi wote ambao wanasababisha kuingia katika migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunaingia kwenye migogoro hii ya ardhi? Sheria Na. 8 ya Ardhi inaitaka TAMISEMI kupima, kupanga na kumilikisha. Nani anapitisha hayo? Ni Afisa Kamishna wa Ardhi kule juu, lakini msimamizi wa sera ni Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro ukitokea unaenda Baraza la Ardhi ama Mahakamani, lakini huku kwenye halmashauri ambapo ndiyo wana sheria ya kusimamia hii ardhi unaona kabisa kuna makampuni yanaenda yanapima pale, yakishapima pale yalipeleka mchoro huku juu baada ya kuwalipisha wananchi, wanaambiwa kwamba hapo tayari hilo eneo lilishapimwa na lilishatwaliwa tayari na mtu. Kwa hiyo, tumeingia kwenye mgogoro mpya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza…

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa dakika 30.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kilosa kuna barabara ya kutoka Kilosa – Mikumi kile kipande kinaunganishwa na *SGR* Stesheni ambayo yamewekezwa mabilioni ya fedha pale. Kile kipande cha kilometa 72, hii sasa hivi ni bajeti ya tano kinaingia na hakijawahi kushughulikiwa. Barabara mpya zinakuja, zinatangazwa, zinajengwa. Kipande hiki kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefikia hatua wananchi wa Mikumi wameanza kukata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dennis Londo kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia kwenye Mpango wa Maendeleo wa Nne na Mwongozo wa Maandalizi wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Nitaanza kwa kuangalia uhalisia wa Mpango ambao tunaletewa *versus* utekelezaji kwa maana ya bajeti zinavyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mathalan, kwa mpango wa mwaka 2022/2023 kwa maana ya bajeti tulikuwa na bajeti ya shilingi trilioni 41 na fedha za maendeleo ambazo zilipelekwa kwenye utekelezaji wa mpango ilikuwa shilingi trilioni 15, sawa na 36%, walau hapa tulitenga vizuri. Ukija mwaka 2023/2024 ilikuwa na bajeti shilingi trilioni 43.3 lakini tukatenga shilingi trilioni 14 sawa sawa na 32.4 tu. Mwaka 2024/2025 tuna-*project* kutenga bajeti yetu kuwa shilingi trilioni 47.4 lakini bado tunatenga shilingi trilioni 15 tu. Kwa hiyo, utaona kuna ongezeko kati ya bajeti hii, yaani takribani shilingi trilioni nne na kitu, lakini kwenye fedha za maendeleo tumeongeza shilingi trilioni 1.2 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mingi ambayo Mpango unatakiwa u-*reflect* kwenye sekta ya afya, kilimo, nishati na hata elimu. Mathalan, sasa hivi Bunge lako Tukufu limepitsha hapa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, tukasema ili iweze kutoa huduma bora na kufanya kazi vizuri, tutahitaji tuwe na miundombinu kwa maana ya vituo vya afya zahanati, watumishi toshelezi, vifaa tiba, dawa na vitendanishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango wa mwaka 2022/2023 mathalan, Serikali ilipanga kujenga zahanati 495, lakini mpaka tunamaliza mwaka ilikuwa wamejenga zahanati 228 tu sawa na 46%. Sasa utajiuliza, kama usipotenga fedha toshelezi, hii Bima ya Afya kwa Wote itaenda kutendeka vipi kwa uhalisia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Serikali, mpaka Machi, 2023 mahitaji ya Wahudumu wa Afya ni 219,000, waliopo 106,000 pungufu 112,000. Ni lazima Serikali ijiwekeze kuhakikisha kwamba inatenga fedha ili sasa zile sekta zote muhimu ambazo zinaweza kuchagiza kwenye uchumi zinapelekewa fedha ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, sote tunajua kwamba kwenye sekta ya nishati mathalan, tuna tatizo kubwa sana la umeme kukatika na pia nishati ya mafuta inapanda bei kila kukicha. Tuna gesi ya asili hapa Tanzania ambapo pia mzunguko utakuwa unafanyika Tanzania tu bila ku-*import* fedha na kupelekea upungufu wa dola nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika gesi asilia, nimejaribu kupitia hapa kwenye Mpango, tunajua, gesi asilia inatumika majumbani, kwenye viwanda, kwenye magari, na pia kufua umeme, na tunayo hapa Tanzania. Kwa hiyo, nilitarajia Mpango ujielekeze zaidi kutenga fedha toshelezi ili sasa tuweze kuchakata hii gesi kuhakikisha kwamba Watanzania wengi wanaunganishiwa magari yao na kutumia gesi ya asili ambayo itakuwa ni *affordable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mafuta; petroli ni shilingi elfu tatu na kitu, lakini gesi ya asili tumeelezewa pale. Ukijaza gesi ya asili kwa shilingi 20,000 au shilingi 30,000 unafika mpaka Morogoro, zaidi ya kilometa 200. Kwa hiyo, itapunguza gharama za maisha kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia majumbani. Mpango unaonesha kwamba wameunganisha nyumba 209 tu kwa Dar es Salaam, nyingine zimekamilika 980 na hata hii ya vituo vya mafuta ya gesi ime-*concentrate* tu huko Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara; Tanzania hii, mikoa mingine huwa mnaiacha ya nini? Kwa hiyo, lazima mweke fedha nyingi. Tuwe na vituo vya kutoa gesi katika kila wilaya, katika kila mkoa ili mimi nikiweka gari langu niki-*convert* liweze kuweka Dar es Salaam likinifikisha Morogoro,

likinifikisha Dodoma kote na-*fill*. Kuacha hizo faida za kiuchumi lakini pia faida za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipange tu ilimradi tunapanga tu, tumesoma hapa imependeza, lakini kiuhalisia unakuta haina mafanikio chanya kwenye uchumi wa Taifa letu. Katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na umeme toshelezi, lazima tuwekeze fedha nyingi, lakini mpango hau-*reflect* hayo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwenye *NIDA*. Sote tunatambua umuhimu wa Vitambulisho vya Taifa na sasa hivi kila idara ukienda, kila sehemu ukigusa unaombwa Kitambulisho cha Taifa. Mamlaka ya Kitambulisho cha Taifa ilianzishwa tarehe 1/8/2008, mpaka sasa hivi ni miaka 15. Kwa takwimu ya sensa, Watanzania wapo zaidi ya milioni 61 walio na stahiki ya kupata vitambulisho nimeangalia hapa, ni zaidi ya milioni 35. Kwa mujibu wa Kamati yako ambao wameainisha hapa, inaonesha vitambulisho vya Taifa kwa maana kadi zilizochapishwa ni milioni 12 tu kwa Watanzania ambao wamepewa, waliosajiliwa ni milioni 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni *just* 50%. Ndani ya miaka 15 tumefanikiwa kutengeneza kadi milioni 15 tu, bado milioni 23 kwa mujibu wa sensa. Kama ndani ya miaka 15 tunatengeneza kadi milioni 12 hizi milioni 23, Kitambulisho cha Taifa tunasema ni muhimu sana na tunatarajia kutengeneza zaidi ndani ya miaka 30 au 35 ijayo. Hii ni kitu ambacho hakiwezekani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na zaidi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mchangiaji kuwa tumeshalipia fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka 2022, shilingi bilioni 42.5, zinazalishwa kadi milioni 11 ambazo zikija zitakuwa zimemaliza tatizo la mahitaji ya kuwapa kadi wote ambao wana namba za vitambulisho. Idadi yao siyo kama alivyotoa takwimu; ni 25,000 na siyo 35,000 kama alivyosema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Angenisikiliza vizuri. Nimesema mpaka sasa hivi ni milioni 24 *something,* uki-*round off* inakuwa ni milioni 25 ambazo mmesajili. Sasa kuna Watanzania ambao hamjawasajili mpaka sasa hivi. Nimechukua takwimu ya sensa, watu ambao wako *eligible* kupata vitambulisho ni 35 *million plus.* Kwa hiyo, una *about 11 million* hujawasajili. Hizi ni takwimu zenu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi hawa watu walikuwa na deni, wakalipiwa deni shilingi bilioni 17, kodi wameondolewa kwenye zile kadi, vi-*tip* sasa hivi siyo adimu sana…

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, atulie, atulie Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikosea siyo elfu, ni milioni. Ninachosema ni kwamba, takwimu yake ya shilingi milioni 35, haipo sahihi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ananipotezea muda kusema, anabishana na sensa. Mheshimiwa Waziri, kaa chini nipokee taarifa. *Would you sit down please*?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kila Mtanzania anastahili kupata kadi ya *NIDA,* ni umri wa miaka 18 kwenda juu kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko taarifa unaipokea?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu ya sensa watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea ni takribani *35 million, just google*. Hapo ulipokaa chukua *google and do the analysis and statistics* utapata uhalisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu ulindwe. Sasa wana *gap* ya watu milioni 11 hawajasajiliwa, ukijumlisha ni takribani milioni 23 hawana kadi. Mmepewa msamaha wa kodi, mmelipiwa deni shilingi *17 billion,* unasema hapa mnakaribia kuchapisha. Kamati imeenda imedhihirisha kwamba mtambo huo unaweza ukazalisha kwa saa kadi 4,500 lakini kwa mwaka mzima imezalisha kadi 1,800,000 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kadi 4,500 kwa saa mlikuwa mnatakiwa kwa mwaka walau m-*produce* kadi milioni (nimefanya hesabu zangu hapa), ni *almost 11 point something million* kama mtu anafanya kazi kwa saa tisa ndani ya siku tano kwa miezi 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kama Taifa tuhakikishe Watanzania wote wanapata kadi tena ambazo zipo *centralized*. Mfuko wa Bima ya Afya unakuwa mle, leseni zinakuwa mle, huduma…

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther naomba ukae. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa mchangiaji anashindwa kuelewa. Nimeeleza kwamba tumeshalipia shilingi bilioni 42.5 kwa ajili ya kuweza kuzalisha vitambulisho milioni 11 ambayo ni pungufu. Hivi tunavyozungumza, kadi hizo zimeshaingia zaidi ya milioni 17. Yaani watu milioni 17 ukijumlisha na zile 11,000 ambazo zipo njiani, kwa hiyo, tunatarajia mwisho wa mwezi Desemba tatizo la *NIDA* la kadi litakuwa limepatiwa ufumbuzi kwa watu milioni 24 ambao wanastahili kupata kadi, waliokuwa na namba za utambulisho.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Esther Matiko, taarifa unaipokea?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo Waziri apunguze kujitetea. *You are talking about the future,* mimi naongea *current* ambacho kimeripotiwa hapa. Sasa hayo mengine utakuja kuyasema huko baadaye. Naongea sasa hivi, hayo maneno mengine unakuta mnaongea ni *unreality,* ukija tena unaambiwa aah, zilikuja, zikakwama, hazikuprintiwa, zikapotea, *we don't need that*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na unilindie muda wangu. Mwisho kabisa ni kwenye huu mpango, lazima u-*reflect* na

maendeleo ya watu. Tumezungumza hapa hasa sisi ambao tunapakana na hizi hifadhi, tunapata kero nyingi sana kiuhalisia. Achilia mbali kutekwa, kuchukuliwa mifugo yetu, watu wetu kutekwa na kunyanyaswa na kupotezwa, ni kweli imekuwa ni taratibu wanaswaga ng'ombe *some kilometers*, ambapo hata hazipo hifadhini, wanaenda wanaziingiza. Mbaya zaidi, wakikamata ng'ombe milioni moja, watasema zilikuwa ng'ombe laki nane. Sijui hizi laki mbili zinaenda wapi? Wakikamata mbuzi 2,000 atakwambia zilikuwa mbuzi 500…

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther taarifa, japo kengele imegongwa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kumpa taarifa Mheshimiwa kwamba kule kwetu tunamwita Msubati Mara, hivi ninavyozungumza, Kata ya Kuzugwa ng'ombe 500; juzi ng'ombe 63, wanalipa faini, Serikali haitaki kuachia ng'ombe na yenyewe eti ina- *lobby* ooh, tutakata rufaa, wanashindana na wananchi kuwafilisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa.

**MWENYEKITI:** Malizia, muda wako umeisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa *we need to say no to this*. Lazima tujue. Kwanza inashangaza, eti *ruling* inatoka leo, *then* kesho yake unaambiwa ng'ombe zote mia nane na kitu zimeuzwa. Hao wanunuzi walikuwa wako *standby* waje kununua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther ahsante sana, muda wako umeisha. Nashukuru sana.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu ume…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther muda umeisha, naomba ukae chini. Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linarejea.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa ratiba ya mchana huu na jioni tutaanza na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mheshimiwa Ally Mlaghila, Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea na wengine watafuata jinsi muda unavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha tangazo lililotolewa asubuhi kwamba mara baada ya shughuli kusitishwa mchana huu,

tutakutana ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya uzinduzi wa *Bunge Marathon*.

Baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.57 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Regina Ndege, jiandae Mheshimiwa Eng. Ulenge, jiandae Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mpango wa Serikali. Kwa kuanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kuipambania nchi yetu kwa kutuletea maendeleo katika kila sekta. Lakini nimpongeze sana kwa kurejesha Tume ya Mipnago, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Wizara hii ya Mipango. Kupitia Wizara hii ya Mipango, tunaamini kabisa kwamba sasa maendeleo na mipango itaenda kupangika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta inayobeba watanzania wengi ni kilimo, uvuvi na ufugaji, na mimi nimeweza kupitia katika ripoti ya kamati na niungane na kamati kwamba bado kasi ya sekta ya umwagiliaji iko chini mno. Serikali inahitaji kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika sekta hii ya umwagiliaji, kwa sababu nchi yetu mpaka sasa suala la mvua sio suala lenye mashaka. Kwa hiyo, Serikali ikiwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji tuna uhakika wa kupata chakula cha kutosha lakini pia sekta ya mifugo itakwenda kustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kila jambo lazima Serikali ifanye, Serikali inaweza kutengeneza mazingira wezeshi katika *private sector*, wakawekeza katika *private sector* kwenye sekta hii ya umwagiliaji. Uwezeshaji wake huo ni kupunguza kodi katika mitambo ya uchimbaji wa visima na mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kupata mabwawa ya kutosha, tuna uhakika wafugaji watafuga vizuri. Tuna uhakika tunaweza kufuga Samaki, tuna uhakika tutapata maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Lakini hivyo hivyo tukiweza kuwekeza kwenye visima tutakuwa tumetatua tatizo la kilimo na uzalishaji. Kwa hiyo, ushauri wangu mkubwa ni kwamba bado Serikali iwekeze kwa nguvu kubwa katika kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali na kuishukuru sana kwa kuendelea kutupatia mbolea ya ruzuku, kwa sababu wananchi wanapata mbolea, lakini bado ninatamani kuona kwenye mpango, Serikali iende kwenye kuwekeza katika viwanda vinavyochakata gesi asilia. Tukiwekeza kwenye viwanda vya kuchakata gesi asilia tunapata nishati mbadala lakini tunapata mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nchi yetu tunaagiza mbolea aina ya *urea* nje ya nchi kwa asilimia mia moja, jambo ambalo linafanya gharama kubwa Serikali kuagiza hiyo mbolea ya *urea*, lakini tukizalisha hapa nchini ni uhakika kwamba mbolea hiyo itapatikana kwa urahisi na wananchi watakuwa wamepata hiyo mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunatakiwa kuwekeza kwenye matumizi ya mbolea ya asili kama mbolea ya samadi na mboji kwa kuwaelimisha wananchi wakulima na wafugaji kwamba baada ya mavuno zile takataka za mashambani, wapewe elimu namna ya kuhifadhi na baadae kuzitumia kama mbolea katika kilimo. Pia, mbolea ya samadi tunaweza kupata kupitia mifugo, mifugo nchi hii bado ni mingi sana lakini wananchi bado hawajapata elimu ya kutosha namna gani tunaweza kutumia mbolea ya samadi katika kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inaweza kuwekeza katika majiji makubwa kama Jiji la Dar es Salaam, Jiji la Dodoma, Jiji la Mwanza, kwa sababu haya majiji makubwa kuna ukusanyaji mwingi wa taka ngumu, lakini Serikali ikiamua kuwekeza kwa kupitia viwanda, tukawekeza kwenye kuchakata taka ngumu kupata nishati mbadala, hapo hapo tuna uwezo wa kupata mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, badala ya taka ngumu kutupwa na kuziba mitalo na nini. Serikali ianzishe viwanda ambavyo vitaweza kuchakata hizo taka ngumu ili kujipatia nishati mbadala, lakini pia tuna uwezo wa kuzalisha mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu hasa wakulima wadogo wadogo wamekuwa wakilima kilimo kisicho na tija na hii inasababishwa na nini? Hii inasababishwa na kwamba wakulima wanalima bila kujua ardhi yao inahitaji kustawishwa mazao ya aina gani. Wakulima wanalima bila kujua kwamba udongo ule unafaa kustawisha mbegu za aina gani na hii kazi ilitakiwa ifanyike, kwamba maabara zetu zifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, maabara zimewekwa katika ofisi za kanda, maabara ziko mbali na wananchi. Mfano, sisi Mkoa wa Manyara, maabara tunayoitegemea ni maabara iliyoko Arusha Serian Tengeru au uende Tanga. Jambo ambalo unampa mkulima gharama kubwa kwenda kufanya vipimo vya udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, amewawezesha Maafisa Ugani pikipiki pamoja na vifaa vya kupimia udongo lakini jambo la kusikitisha sana, Maafisa Ugani mpaka sasa ukienda kuuliza huko kwa wakulima kazi hiyo haifanyiki. Kwa hiyo, wakulima wamekuwa wakilima bila kujua kwamba udongo wake unatakiwa kustawisha zao gani lakini mbolea ya aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri ifike wakati Maafisa Ugani warudishwe chini ya Wizara ya Kilimo ili waweze kusimamiwa ipasavyo, kwa sababu sasa hivi wanawajibika kwa Mkurugenzi, jambo ambalo linakuwa gumu sana kuwafuatilia mpaka ngazi za chini. Hivyo, wakulima wadogo wanatakiwa wapewe elimu kwa sababu wakulima wakubwa wana uwezo wa kupeleka hizo *sample* za udongo katika maabara na kuweza kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishauri vile vituo vyetu vya utafiti viboreshwe, hata vile vifaa vinavyotumika bado havikidhi haja. Wakati mwingine hawapati majibu yanayoendana na uhalisia. Hata mtu akisema apeleke udongo, ukiwa na hekari kumi, ukichukua udongo wa sehemu moja yawezekana ndani ya hekari kumi labda una udongo wa aina tatu, kuna udongo wa kichanga, labda una

mfinyanzi, ukipeleka udongo wa aina moja maana yake hutapata matokeo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kilimo cha mbogamboga. Kilimo hiki cha mbogamboga ni kilimo ambacho watu wanalima bila kuwa na usimamizi hawana bodi ni watu wanaamua kujilimia tu lakini ndio kilimo ambacho kinazalisha kwa wingi zaidi, kwa hiyo niombe Serikali iwawezeshe wakulima wadogo wadogo kupata mbegu kwa urahisi.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumetokea…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ndege kwa mchango mzuri.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Namwita Mheshimiwa Eng. Mwanaisha Ulenge, jiandae Mheshimiwa Msongozi, jiandae Mheshimiwa Ally Mlangila Jumbe.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa muda na wakati kama huu, lakini kipekee pia nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Neema zake kubwa kubwa alizozineemesha katika Taifa letu. Kama neema hii mpya iliyoingia wanasema, "*the state of at* neema" ya kupata Rais wa Bunge la Dunia. Ni neema kubwa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Bunge la Dunia kwa mimi kuwa sehemu ya uzoefu nilioupata bila yeye kutaka kwenda tusingepata uzoefu ambao tumeupata. Nashukuru sana kwa nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza sana Serikali kwa jitihada kubwa za kuhakikisha maendeleo ya Taifa letu yanasonga mbele. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji. Katika mchango wangu nakwenda moja kwa moja katika hitimisho na vile vile nitarudi nyuma ya hotuba iliyotolewa na Waziri waWizara hii ya Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa hitimisho zuri kabisa ambalo kwa hakika limeonesha dhamira ya Wizara hii kuwa *think tank* ya Taifa hili, ameeleza vizuri kabisa kwamba tunapaswa kuweka mipango na kuipa vipaumbele na kama Taifa kuridhia kwa pamoja namna gani tutaviendea vipaumbele hivyo ambavyo tumekubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndio maana halisi ya kuwa na Wizara ya Mipango kama *think tank* ya Taifa hili. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri. Nimekwenda zaidi ulivyosisitiza kwamba, mipango hii ni mipango ya maendeleo ya Taifa letu na sio mipango ya Serikali, maana yake ni kwamba umelenga kabisa kuhakikisha Taifa hili linasonga mbele kimaendeleo na sio kuwa na mipango ambayo haitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Kamati yetu ya Miundombinu tulikuwa na kikao pamoja na Kamati ya Wizara ya Fedha. Suala lililoniumiza kwa uchungu na nilisema kwa uchungu kabisa ni kuwepo na miradi mingi ya maendeleo ambayo fedha zake haziendi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya fedha alielezea vizuri sababu ya kwamba miradi hiyo inakuwepo na nani hataki miradi, kila mtu anataka miradio. Sasa ifike wakati tuangalie vipaumbele vya Taifa letu ili tuweze kusonga mbele na bila kupanga mipango ya Serikali bali tupange mipango ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba katika hoja hiyo nzuri aliyoitoa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, mimi naiunga mkono asilimia mia moja, lakini ili mipango ile itekelezeke ni lazima kuwepo na ufuatiliaji na tathmini ya mipango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo ambacho sikubaliani nacho ni Wizara hii ya Mipango kujifanyia ufuatiliaji na tathmini, naona hii haiko sawa. Mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ni lazima ifanywe na Wizara nyingine ambayo itaweza kuangalia vizuri utekelezaji wa mipango ile, lakini italeta *contradiction* na kutakuwa na *conflict of interest* au *actions* kwa maana mimi nimepanga mwenyewe halafu mimi nijitathmini mwenyewe, hatutaweza kwenda sawa. Ni lazima jambo hili liangaliwe kwa namna nzuri ambayo litaweza kuwekwa na lilete tija kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* amesema wazi fedha nyingi ambazo zinapotea katika Taifa letu, na tulikuwa tunaamini mifumo kwamba itatusaidia kupunguza mianya ile, lakini mifumo nayo inachezewa. Kama mifumo inachezewa basi ni lazima tuje na ufuatiliaji wa mara kwa mara na tathmini za mara kwa mara za miradi ya maendeleo. Kuna mambo mbalimbali ambayo katika Taifa letu tumeyaona ni maendeleo, kwa hiyo naomba kama Taifa ni kwa nini tunaogopa kuingia katika ufuatiliaji na tathmini? Ni nani anayeogopa kivuli chake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona tumetoa mifano mingi kwenye Afrika yetu hii. South Africa wanayo, Uganda wanayo…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa *Engineer* Ulenge kwa sababu ni kati ya Wabunge ambao ninaweza kuwaita ni ma-*champion* wa *monitoring and evaluation* na amekuwa akitusaidia ushauri wa mara kwa mara. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kutokana na mawazo yake na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge wengine na hasa utendagi kazi mzuri wa mtangulizi wangu Mheshimiwa Simbachawene, kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 Serikali imeamua kuanzisha *Directorate* mpya ya *monitoring and evaluation* na iko ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Sheria ya mipango tuliyopitisha tumempa nafasi Waziri wa Mipango yeye kuiangalia ile miradi mikubwa ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kazi ya kufanya *monitoring* na *evaluation* kwa utendaji kazi na shughuli zote za Serikali kwa mujibu wa *Directorate* mpya imebaki kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na tunaomba Waheshimiwa Wabunge, muendelee kutushauri na tukiweza kujaaliwa mwakani tutakuja na ripoti mpya ya ufuatiliaji na tathmini ambayo itaangalia utendaji kazi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Mbunge…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa *Engineer,* taarifa hiyo.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea taarifa hiyo na ninafahamu kwamba Serikali imechukua hatua. Ni kweli kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, hiyo *Directorate* ya *monitoring and evaluation* ipo. Shida yake ni nini? Iko chini ya Mkurugenzi wa Mipango, uongo au ukweli? Nafikiri hii ndio *contradiction* ambayo mimi naizungumzia, kwa hiyo, nashukuru kwa taarifa ya Mheshimiwa *Chief Whip*, kwamba Serikali mtalianglia

vizuri, mimi nimeridhika na hilo na ninaamini Serikali yetu ni sikivu na inapokea maoni yetu ipasavyo.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uzingatie muda wangu tafadhari.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nataka nimpe dada yangu taarifa kwamba sheria iliyopitishwa na Bunge hapa iliyoanzisha Tume ya Mipango na kwa mujibu wa sheria hii, Bunge hili liliipa nguvu hiyo Tume ambayo ndio ya Taifa ifanye tathmini ya sera zingine zote za wizara zote ili tuweze kujua kama tunakwenda kwa mujibu wa sera ya Taifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Eng. Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, napokea taarifa hiyo. Naifahamu hiyo Tume na ndani ya hiyo Tume kwenye hiyo sheria, inaonesha pia inafanya *monitoring and evaluation,* ndio kitu ambacho mimi naona ni *contradiction*. Niliiona ile sheria, kwa hiyo mimi naomba Serikali wataliangalia vizuri, wakiona inafaa, wakichukua na maono ya uzoefu wa nchi nyingine za Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu uuzingatie umepotea muda mwingi tafadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wetu ambao umewasilishwa na Waziri mwenye dhamana umeweka mkazo katika kuimarisha

uzalishaiji katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Mimi naomba nizungumzie sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali hii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha imekopesha boti kwa wavuvi na sisi Mkoa wa Tanga tumepata boti kumi na nne zenye thamani ya bilioni 1.2. tunaishukuru sana Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenye dhamana ameeleza vizuri kwamba malengo au msisitizo ni kuhakikisha thamani inaongezwa katika mazao yatakayouzwa nje ya nchi, sasa sisi tumepata boti, *alhamdulillah* tunashukuru, lakini je, boti zikishazalisha zaidi tunaongezaje thamani kama ukanda wote wa Pwani ya Bahari ya Hindi, kilomita takribani 1400 kutoka Tanga mpaka Lindi hakuna viwanda vya kuchakata Samaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini viwanda visijengwe ukanda wa Bahari ya Hindi, ili kuweza kuongeza thamani katika mazao ya uvuvi ili yaweze kusafirishwa nje ya nchi? Ni lini Serikali watajenga viwanda ukanda wa Bahari ya Hindi ili tuweze kuongeza thamani ya Samaki wanaozalishwa kwenye Bahari ya hindi waweze kwenda nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani tani laki saba na thelathini elfu zinazalishwa huko. Kwa nini hatuoni maana ya kuhakikisha uchumi wa *blue* tunaupa thamani ya kutosha kwa kujenga viwanda katika ukanda wa Bahari ya Hindi? Hili linashindikana vipi? Mbona Ziwa Victoria tumeweza? Ni wapi pa kubwa ukanda wa Bahari ya Hindi na Ziwa Victoria, mbona kule imewezekana? Tunaiomba Serikali katika mipango yake na hili walipe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kuzungumzia Bandari. Tunaipongeza Serikali, tumeona mikataba imekwishaingiwa ya kuendeleza Bandari ya Dar es Salaam. Sasa, wote tumekubali. Pia, nchi nyingi ambazo zimeendelea mfano Singapore na *south*

Korea ni kutokana na rasilimali bahari. Sasa Serikali iweke macho yake pia kwenye bandari za pembezoni. Ni lazima tuchechemue uchumi katika yale maeneo ambayo yana Bandari. Ni kweli fedha zimepelekwa takribani bilioni 500 katika Bandari ya Tanga na kweli kina kimeongezwa. Hata hivyo, bila kuchechemua uchumi wa maeneo yale meli kubwa haziwezi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima yale yote yanayopatikana katika maeneo yale kama Mtwara – Liganga na Mchuchuma, Tanga, yote ambayo yanaweza kufanyika Mkoani Tanga ili kuchechemua uchumi wa Tanga ili meli kubwa ziweze kwenda Serikali ipange kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Serikali imeweka mpango kwenye Bandari ya Mwambani, nafikiri sasa ni wakati sahihi. Sheria ya *PPP* imekwishakamilika, Bandari ya Mwambani ipatiwe mwekezaji na uchumi uchechemuliwe katika Bandari ya Tanga ili tuweze kunufaika na rasilimali bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, ukiangalia Nchi ya China ina bahari katika maeneo mbalimbali lakini siyo mizigo yote inapita Guangzhou, siyo mizigo yote inapita Shanghai. Lazima kama Taifa tuamue kupanga mizigo ipi ipite wapi. Pia kwa *nature* ya Tanga ilivyokaa na ukizingatia Mradi wa Bomba la Mafuta unaokwenda, Tanga iwe *dedicated* kwa ajili ya mafuta na hilo linawezekana. Kwa nini hatutaki kufanya hivi? Hakuna Taifa ambalo litaendelea bila bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata pale Bagamoyo walipofikiria kuanzisha upya Bandari ya Bagamoyo, wanafikiria pamoja na viwanda…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haiendi peke yake. Kwa hiyo, naiomba pia waangalie namna ya kuchechemua uchumi wa maeneo yenye bandari ili tuweze kunufaika na bandari zetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, jiandae Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe na jiandae Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mpango huu wa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuleta maendeleo kwa kasi kubwa sana katika Nchi yetu ya Tanzania. vile vile, jambo la pili niwapongeze Mawaziri wawili hawa, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango. Nilipokuwa nawatazama hapa kwa haraka nilimtambua Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, lakini yule Waziri mwingine wa Fedha sikumtambua kwa sababu ya mabadiliko makubwa sana aliyonayo pale usoni kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichukue nafasi hii kuishauri Serikali kwamba, tumekuwa tukitumia kitu kinaitwa *force account* kwa ajili ya kupeleka fedha za miradi kwenye ujenzi wa miradi mbalimbali ikiwemo Miradi ya Afya, Elimu, Maji na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nishauri kama Mjumbe wa Kamati ya *PAC* kwamba, tumekuwa tukitembelea miradi hiyo ufanisi wake kwa kweli ni mdogo. Sasa, ni kwamba hii *force account* mimi nilikuwa nafikiria kwamba ingetazamwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa wakitumika mafundi wa kawaida ambao kimsingi ukija kuangalia majengo unakuta yana *crack*. Pia, huwezi kwenda kukamata fundi wa kawaida labda ni mtoto wa mjomba au wa shangazi ndiye alipewa ile kazi, badala yake inakuwa ni hasara na mzigo mkubwa sana kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii *force account* tuiangalie upya na ikiwezekana basi tupate watu wenye *qualifications* kabisa wawe na vyeti sahihi kabisa…

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa, hapana. Umeshachangia bwana unanipotezea muda…

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Kiti unaniongoza. Naomba kumpa mchangiaji taarifa kuhusiana na hiyo hoja yake nzuri. *Issue* ya *force account* ningependa Bunge hili na Watanzania wafahamu kwamba, hatuikatai *force account*. Shida kubwa ya *force account* ni *double handling*. Hii *double handling* ya kwamba wakati huo huo rasilimali za ndani zinatumika….

**MWENYEKITI:** Ameshakuelewa. Ahsante.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** …na rasilimali za nje zinatumika, ndipo upotevu wa fedha unapotokea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ulenge ungechangia kwenye mchango wako. Ulikuwa na dakika 15 au ulikuwa unataka uje utietie maneno hapa …

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Nimekuongezea nyama, siyo kukuponda.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki bwana, tafadhali sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea. Ziwa Nyasa na maziwa mengine katika nchi yetu hii ya Tanzania. Naona iko haja ya kufanya uboreshaji kwenye maziwa yetu haya. Kwa mfano kwenye Ziwa Nyasa ukiangalia Bandari ya ile ya pale Mbamba Bay, bado haijakamilika. Kwa hiyo, tunaomba pesa zipelekwe pale ili kuweza kuiboresha ile Bandari ya Ziwa Nyasa pale Mbamba Bay ili ile bandari iwe na sifa ambayo itakuwa kweli na uwezo mkubwa wa kuweza kusafirisha mizigo mbalimbali katika bandari ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti jambo lingine niombe sana Serikali, tunapozungumzia kupeleka pesa za miradi ya maendeleo, basi ziharakishwe. Tumezungumza hapa katika bajeti iliyopita kwamba, pesa zitagawiwa kupelekwa kwenye maziwa mengine ambazo zilitengwa na Mheshimiwa Rais, ambapo Mheshimiwa Rais alitoa pesa hizo kupitia Wizara ya Mifugo. Karibu bilioni 20 zimekwishapelekwa katika Wizara, lakini kwa nini zinacheleweshwa kupelekwa kwenye Maziwa hayo ikiwemo Ziwa Nyasa ambalo pia tumepata kuambiwa kwamba tutatengewa bilioni tatu. Pia, mpaka sasa hivi tunavyozungumza tumefikia nusu ya mwaka, lakini bado pesa hazijaenda. Kwa hiyo, tunaomba sana tunapokuwa tunazungumza, pesa ziende mara moja zikafanye kazi, ilihali Mheshimiwa Rais amekwishatoa hizo pesa, basi ziharakishe utekelezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka niishauri Serikali yangu kuhusiana na Mradi wa Reli. Reli ya Mwendokasi ya kutoka Mtwara mpaka Mbamba Bay. Hii reli ni muhimu sana kwa ajili ya kuchochea uchumi wa Tanzania katika ukanda wa kusini kwa sababu reli hii itasaidia kusafirisha mizigo mbalimbali ambayo itatokana na:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tutakuwa na Mradi wa Liganga na Mchuchuma pale. Kwa hiyo, reli hii itasaidia kusafirisha chuma kutoka pale Liganga kupeleka Mtwara na kusafirisha kwenda maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunayo makaa ya mawe katika Mkoa wetu wa Ruvuma. Hiyo nayo pia ingesaidia sana kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe yale katika kuchochea hali ya uchumi katika nchi yetu. Vile vile, niseme kwamba, pamoja na kwamba tunatengeneza miundombinu ya barabara lakini kuongeza reli itasaidia sana kuzifanya zile barabara ziendelee kutumika kwa muda mrefu bila kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda katika upande ule wa kwetu Mikoa ya Kusini, Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma pamoja na Njombe barabara zimekuwa zikichimbika sana kwa sababu ya magari mengi, malori mengi ambayo yanatumika kwenye zile barabara kubeba makaa ya mawe, kubeba korosho, kubeba kahawa, kubeba mahindi, maharage na vitu vingine vingi kwa sababu ukanda ule wote sisi ndiyo tunaoilisha Nchi yetu hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana reli hii ikajengwa ili kuweza ku-*balance* hii miundombinu na kuweza kuifanya Serikali, pesa inayowekeza miundombinu, siyo unawekeza kwa muda mrefu kwenye miundombinu ya Barabara, halafu unaacha kwenye reli. Kwa hiyo, mpaka barabara inaharibika unarudi sasa na kuanza kutengeneza barabara wakati reli bado hujanza kuitengeneza. Kwa hiyo, nadhani kwamba uko umuhimu wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la Liganga na Mchuchuma. Limesemwa sana na Wabunge wengi hapa, naomba Serikali itueleze katika Mpango huu wamejipangaje kuhakikisha huu mradi unaanza mara moja ili huu wimbo tunaoimba hapa kila siku sasa upungue na twende kwenye utekelezaji, hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu ukianza kutekelezwa utaongeza ajira katika nchi yetu ya Tanzania lakini pia utachochea uchumi kwa kasi sana. Hata hivyo, chuma kile klitakachochimbwa pale ndicho kitakachotumika katika kutengeneza magari, vipuri mbalimbali na mambo mengine kadha wa kadha. Niombe sana, ajira ni muhimu sana, lakini pia uchumi wetu kuimarika ni muhimu pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda sasa kwenye suala la viwanda. Ili uchumi wetu uweze kuimarika ni lazima tuwe na viwanda hivi ambavyo vitachochewa na Sekta ya Kilimo. Kwa hiyo sasa, hebu mtuambie, Waheshimiwa Mawaziri watakapokuja ku-*wind-up* watueleze wamejipangaje kuhakikisha kwamba tunapata viwanda katika Nyanda za Juu Kusini na maeneo mengine katika nchi yetu ya Tanzania ili tuweze ku-*balance* kila eneo tuwe na viwanda, kwa sababu tukiwa na viwanda moja kwa moja tutachochea ajira kwa wananchi wetu lakini pia tutazalisha bidhaa ambazo tutaziuza ndani na tutaziuza nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uzalishaji huu utakuza uchumi kwa kasi sana. Mheshimiwa Kitila Mkumbo, tunamtegemea sana, tunaona amekuja na kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya. Kwa hiyo, tunategemea tutapata matokeo chanya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kwenye masuala ya viwanda, kwa kuwa sisi tumekuwa tukizalisha sana mazao ya nafaka katika ukanda ule wa kusini, basi tunataka tuone Mheshimiwa Kitila anatupelekea viwanda vingapi katika kipindi hiki cha Mpango huu kufikia 2024. Mheshimiwa Waziri ana uwezo wa kutafuta wadau ambao watakuja kujenga viwanda vikubwa kule, tupate viwanda vya kukamua mafuta. Sisi kwenye uzalishaji hatuna shida. Shida ni namna ya kupata masoko, namna ya kuongeza thamani ya mazao yetu, hiyo ndiyo shida tuliyonayo lakini kwenye uzalishaji hatuna shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mvua za kutosha. Karibu nusu ya mwaka sisi mvua zinayesha tu. Hata sasa tunavyozungumza watu wako shambani. Kwa hiyo, nataka niseme nguvu za wananchi hawa zisipotee bure. Tuletee viwanda vya kuchakata mafuta, tukachakate sembe, tunayo soya ya kutosha, tukamue wenyewe mafuta ya soya. Vile vile, tunao ufuta wa kutosha. Nataka niseme tukifanya hivyo kwa kweli itakuwa imesaidia sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kiwanda cha Sonanko.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekunde moja tu. Kiwanda cha Sonanko, Kiwanda cha Tumbaku pale Songea Mjini. Kiwanda hiki kimekuwa kinaajiri wananchi wengi sana zaidi ya 3,000. Hata hivyo, sasa hivi ni zaidi ya miaka nane, tumeambiwa kiwanda kitafufuliwa mpaka leo hakijafufuliwa…

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mengine andika.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wageni walioko Bungeni jioni hii ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wanafunzi 72 wa *American British English Center* kutoka Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, yale mafunzo ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhusu mfumo wa uwasilishaji tamko kwa njia ya mtandao *online declaration system* yanaendelea katika chumba kilichoko jirani na Ofisi ya *Searjent-At-Arms* kuanzia jana. Mafunzo

hayo yatahitimishwa kesho tarehe 10 Novemba. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote kwa makundi madogo madogo wanahimizwa kutembelea wataalam hao kwa ajili ya kupata mafunzo hayo muhimu ya ujazaji fomu kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Ally Mlaghila, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea.

**MHE. ALLY A. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii, lakini kabla ya yote naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo ambapo tunazungumzia mambo makubwa ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ustawi na maendeleo ya nchi hii na pia hasa katika utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo tunaweza tukajisahau nini kinaendelea. Unapomwona Rais wa *IPU* ni matunda ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndiye ambaye amefanya kwa sasa tuwe na Rais huyo. Kwa hiyo, hiyo ni kazi kubwa, lakini pia ushawishi mkubwa alionao kwenye mataifa ya nje na jinsi ambavyo watu wanavyomheshimu yeye na kuliheshimu Taifa hili. Kwa kweli tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipowashukuru hawa Mawaziri wawili Dkt. Mwigulu Nchemba na Profesa Kitila Mkumbo. Wamefanya kazi kubwa na wametuletea Mpango mzuri sana ambao kwayo utaleta mambo makubwa na maendeleo makubwa kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hawa Mawaziri wawili tu, naomba nikiri wazi kwamba, nimekaa hapa kwa hii miaka mitatu, nimefuatilia Mawaziri wetu wanavyofanya kazi. Naomba

niwashukuru hawa Mawaziri. Wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Hawa Mawaziri hawalali usingizi. Kuna watu nimewahi kuongea nao wananiambia wengine wanalala wanapigiwa simu mpaka usiku kwa ajili ya kunusuru Taifa hili ili liweze kuendelea. Waheshimiwa Mawaziri, watembee kifua mbele na wao ndiyo Askari wa Mwamvuli wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Pia, mambo yote yanayotendeka pamoja na watendaji wenu ninyi ndiyo mnaoyafanya. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wote na mambo yote tunayoyazungumza hapa leo na hata tangu tumeanza, lengo letu kubwa ni ustawi wa jamii zetu na ustawi wa wananchi walioko kule chini. Vile vile, tunapoyafanya haya tunafanya mambo makubwa. Mheshimiwa Rais amejitolea moyo wake wote kwa dhati kuhakikisha mambo mengi yanakwenda kule chini na sasa tunatembea kifua mbele. Kila tunachokiomba kwa Mheshimiwa Rais kwa kweli kinafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo madogo sana ambayo ningeomba tushauriane vizuri sana tena kwa maneno ya staha sana na ndugu zetu wanaoshiriki katika mipango hii. Mambo hayo ni yale ambayo yanawahusu wananchi hasa kwenye sehemu zile ambazo niseme zinaleta kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kero ndogo ndogo ambazo kwa kweli wakati mwingine siyo za lazima. Kwa mfano, kule kwangu kuna malalamiko ya Wastaafu hasa wanajeshi. Wanaambiwa waende kuhakikisha taarifa zao, watoke vijijini kwa nauli zao waende Mbeya kilomita 118 na unapanda milima, kwenda na kurudi bila kula ni zaidi ya shilingi 25,000. Sasa hao watu walilitumikia Taifa, walipigana vita na tayari wamekwishazeeka. Hili la kuhakiki badala ya kuweka *centers* kwenye wilaya, wanawaambia waende mikoani ndiko wakahakiki taarifa zao. Ndiyo nasema hivi ni vitu ambavyo huwa vinahitaji kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *TASAF; TASAF* imekuja kuwakomboa watu maskini, lakini kuna malalamiko makubwa sana huko kwamba, wanaopewa siyo wale ambao walistahili na mfumo unaotumika ni mfumo wa kisomi. Sasa, wale wazee wetu walioko huko chini ukiwaletea mfumo wa kisomi unakuwa ni shida. Maswali wanayoulizwa na majibu yanayoingia kwenye *Computer* ili *computer* ichague, hayaendani na uhalisia. Mtu mwingine hata umri wake haujui, hata kwamba anapata shilingi ngapi kwa siku hajui. Sasa, unapomwingiza kwenye *computer* ndiyo achague kwa kweli inakuwa ni ngumu.  Ningeomba ifanyike kama ilivyokuwa ikifanyika zamani. Wananchi wenyewe ndiyo watoe majina ya hao watu. Pia wakitoa kusiwe na haja ya mfumo kuchambua tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Serikali kulipa madeni ya wakandarasi lakini na haya madeni madogo madogo yanayohusu wananchi. Kwa mfano, kuna sehemu zinapitishwa barabara, mpaka mnakwenda mnagombana na wananchi kwa kitu ambacho hakina maana ambapo tayari tulikuwa tumekwishapanga barabara ipite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mmoja kwenye barabara ya Ibanda – *Itungi port*. Tunaishukuru sana Serikali inajenga barabara ile lakini tangu wananchi wake wamefanyiwa *assessment* mpaka leo hawajalipwa fedha zao na barabara inaendelea kujengwa. Kwa hiyo, vitu kama hivi huwa vinawaudhi sana wananchi, ningeomba Serikali inapopanga mipango, ipange na mipango ambayo itakuwa inaondoa hizo kero ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kero kubwa kubwa pia. Leo tunapozungumza kulikuwa kuna kero za wananchi kupigwa, wananchi kufanywa nini na *TANAPA*. Mimi ni shahidi, nilibahatika kuwa kwenye timu ya kamapeni kule Mbarali. Wakati wa ufungaji wa kampeni kule Mbarali pamoja na kata nane nilizozunguka, nilipangiwa Kata ya Madibila kwenye Vijiji vya Ifuchilo na Ukwavila. Hata hivyo tulipowambia Mheshimiwa Rais na Makamu kupitia Chama Cha Mapinduzi wamesema, wananchi sasa wataendelea kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walinivuta vijana wachache walikuwa kama mia moja hivi pembeni hivi baada ya mkutano, wakaniambia Mheshimiwa Mbunge tumekubaliana na wewe, sisi kura kwa CCM tutatoa lakini suala la kwamba tuende tukalime, hatuwezi kwenda kule tumepoteza ndugu zetu, tumepoteza vifaa vyetu vya kulimia, labda aje yeye mwenyewe aje atupeleke kule, *otherwise* tunapigwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine nataka nisistize, wataalam wetu hebu wachague moja kuishauri Serikali kwa weledi, wenzetu walioko Ulaya wamekuwa na ubunifu mkubwa sana kwa sababu ya matatizo. Leo sisi tuna matatizo kwa mfano kule Mbarali, kuna tatizo la ardhi, kuna matatizo ya maeneo oevu, mimi naona hakuna haja ya kuanza kupigana kikubwa ni kwamba, Serikali wataalam washauri ni jinsi gani tunaweza tukatokana na hilo wakiwashirikisha wananchi. Kuna mambo mengine yanafanyika bila kushirikisha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni nchi ambayo ni ya umoja hebu tuende tuwe tunawashirikisha wananchi katika mambo mengine ambayo yanafanyika. Kwa hiyo mimi naomba wataalam wetu waishauri vizuri Serikali kule chini Mbarali watu wanasema achana na kitu chochote kile sisi ni ardhi. Kwa hiyo watu wabuni ni jinsi gani tutatumia ardhi pamoja na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kule Kyela kuna suala la *cocoa,* kuna matatizo pamoja na Serikali yetu na Mkuu wetu wa Mkoa kujitahidi kwa dhati ya moyo wake kuhakikisha anaondoa matatizo yanayotokea, lakini imekua ni ngumu kwa sababu ya *nature* ya zao lenyewe lilivyo. Kwa hiyo mimi ningeomba kuna vitu vingine ambavyo hakuna haja ya kuingizia kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani, kwa sababu lile zao ni zao ambalo haliwezi kumnufaisha mkulima, kwanza ni zao la wazee, ni zao ambalo watu wanalima kwenye nyumba zao. Kwa hiyo inakuwa ni ngumu sana kulifanya liingie kwenye stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ili tuendelee tunahitaji sana nishati, kuna miradi mingi ambayo inahitajika ili kuweka nishati vizuri. Tusitegemee Bwawa la Mwalimu Nyerere tu, kule kwetu Mbeya kuna mradi wa *River Songwe Basin* mara nyingi hauongelewi lakini ni mradi ambao unakuja na *Megawatt* 90 za umeme ukikamilika. Mimi ningeomba sasa iwe ni wakati sahihi Serikali kuanza kuutekeleza huo mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale *Kiwila Coal Mine* kuna megawati 200 ambazo zingefanyiwa kazi saa hizi tungekuwa tunapata umeme na tayari tusingekuwa kwenye matatizo haya ambayo Kyela kila siku ni giza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine nitachangia kwa maandishi lakini kuna Kiwanda cha Urafiki ni aibu tena ni kwa Mheshimiwa Kitila Mkumbo kule.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. ALLY A. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Urafiki pale imekuwa ni sehemu ya kupangisha badala ya kutengeneza nguo ambazo tulinuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono, hoja ahsante sana kwa nafasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kimea jiandae Mheshimiwa Shigongo ajiandae Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo ya tarehe 09/11/2023, na mimi kuchangia kwenye Mpango huu wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa ushauri wangu hasa nimejielekeza kwenye Sekta ya Kilimo. Ninaomba nitumie fursa hii

kueleza mambo machache sana ya nyumbani kwetu nikimaanisha kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya miaka mitatu kama siyo minne tuliahidiwa kujengewa barabara kwa kiwango cha lami, barabara ambayo inaunganisha Majimbo muhimu matatu kwenye Mkoa wa Tanga Jimbo langu la Korogwe Mjini, Jimbo la ndugu yangu Timotheo Mnzava Korogwe Vijijii lakini Kimbo la Kaka yangu Dunstan Kitandula. Barabara hii tumeahidiwa mara nyingi, Serikali ilituahidi kwamba mwaka huu wataenda kumaliza upembuzi yakinifu ili barabara ile iweze kutangazwa. Mwezi wa Sita walituahidi watamaliza mwezi wa Sita umepita hawajamaliza, wakasema mwezi wa Tisa, mwezi wa Tisa umepita haijamalizika baada ya hapo wanatuambia mwezi wa Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ahadi zimekuwa nyingi tunaomba Serikali itimize ahadi hiyo, upembuzi yakinifu umalizike barabara hiyo itangazwe ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami kama tulivyoahidiwa. Kibaya zaidi Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mkuu kwa nyakati tofauti walimuahidi Kiongozi wetu mkubwa kabisa wa dini kwenye nchi hii kwamba wataenda kujenga barabara ile, Mufti Mkuu wa Tanzania. Tunaweza tukaacha kutimiza ahadi lakini mpaka kwa Viongozi wetu hawa wakubwa wa dini haileti picha nzuri. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kwenda kufanyia kazi barabara ile haswa kipindi hiki cha mvua imeharibika sana haipitiki kwa hiyo waende kuingalia na waone namna gani wanawasaidia wananchi wa Korogwe Mjini kwenda Magoma, kwenda Mabwepande ambayo inaunganisha Majimbo matatu muhimu na ndugu zangu Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Mnzava pamoja na mimi tumekuwa tukiliongelea mara nyingi. Ahsante nimeanza na utangulizi huo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mkubwa ni kwenye Sekta ya Kilimo siku ya leo, nimejipanga kuchangia sehemu saba kwenye Sekta ya Kilimo, muda ukinitosha nitachangia zote muda ukiniishia katikati hapo nitakapoishia nitaishia hapohapo, kikubwa

ninachotaka kuchangia moja ni Mikopo kwenye sekta ya kilimo, riba ya mikopo ya sekta ya kilimo, pembejeo kwenye sekta ya kilimo, bima ya kilimo, masoko, miundombinu ya umwagiliaji, uongezwaji wa thamani kwenye mazao ya kilimo. Hayo ni mambo saba ambayo nataka kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na jambo la kwanza ambalo ni mikopo kwenye sekta ya kilimo. Kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan jinsi anavyoendelea kuongeza bajeti kwenye sekta ya kilimo tunaona miundombinu mingi kwenye sekta ya kilimo ikiwemo miundombinu ya umwagiliaji ikijengwa siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni uwekezaji mkubwa ambao Mama Samia Suluhu Hassan anaifanya kwenye sekta ya kilimo lakini bado tuna changamoto kubwa kwa wakulima wa nchi hii kukosa mitaji ili waweze kujikita kwenye sekta ya kilimo. Tumekuwa tukihubiri sana kwamba Benki zetu za Biashara pamoja na Benki yetu ile ya Kilimo inatoa mikopo kwa wananchi lakini kwenye *ground* hali haiko hivyo, vijana wetu, wamama na wakulima wadogo imekuwa ni vigumu sana kupata mikopo kwenye taasisi hizi za mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali moja kuendelea kuongeza bajeti au fedha kwenye Benki yetu ya Kilimo ili kuhakikisha tunaongeza wigo wa wananchi wa Kitanzania ambao wanapenda kulima wapate mikopo ili waendeleze sekta ya kilimo. Nilikwisha kushauri kwenye Bunge hili kwamba hizi Benki za Kibiashara zinafanya biashara na hazitaki kupata hasara.

Mheshimiwa mwenyekiti, sekta ya kilimo ni kati ya sekta ambazo *risk* iko kubwa hivyo ili kuongeza *appetite* ya hizi benki kuweza kukopesha wakulima ni lazima Serikali ije na bajeti na *fund* kuwepo na mfuko ambao *risk* ambayo inatokana na kukopesha sekta ya kilimo iwe inakuwa *covered* na hiyo *fund* ambayo Serikali imeiweka. Tukifanya hivyo benki zetu za kibiashara zitaongeza mikopo kwa wakulima kwa kuwa wanajua endapo wakulima wata-

*default* mikopo hiyo kuna *fund* kutoka Serikalini ambayo ita-*cover risk* hiyo. Nilikwisha kushauri ninaomba ndugu zetu hawa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango waone namna Mfuko huo unakuja ili kuongeza mikopo kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili kama nilivyosema ni riba. Tunashukuru Serikali kupunguza riba kwenye sekta ya kilimo kushuka mpaka *single digit* asilimia tisa lakini bado tunaweza tukafanya zaidi riba ikapate kupungua benki zetu zinapata faida kubwa, tupunguze riba kwenye sekta ya Kilimo ili tupunguze gharama ya kilimo, hilo ni jambo la pili tuangalie namna tunapunguza riba kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo nataka kuchangia ni pembejeo kwenye sekta ya kilimo hasa pembejeo muhimu kama mbegu pamoja na mbolea. Watanzania wengi, wakulima wengi wa nchi wanashindwa kuingia kwenye kilimo kwa ajili ya kukosa Pembejeo muhimu haswa Mbegu. Mheshimiwa Bashe atakuwa shahidi mwaka jana msimu uliopita nilikuwa nikimsumbua sana wananchi wangu wa Korogwe Mjini ambao walikuwa wanatafuta mbegu bora za mahindi kwa ajili ya kupanda hawakupata mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali ije na mkakati ili pembejeo hizi muhimu mbolea na mbegu ziwe za kutosha nchi hii na gharama ipate kupungua lakini ushauri wangu angalau najua watu wengi wanaweza kupinga kusema gharama ni kubwa lakini nchi hii ina uwezo wa kufanya mbegu kuwa bure kwenye nchi hii, mtu yeyote ambaye anataka kulima akapate kupata mbegu bure. Kama haiwezekani basi wakati wa kilimo wananchi wakopeshwe mbegu wakati wa mavuno wapate kurudisha fedha hizo walizokopeshwa kwa ajili ya kupata mbegu. Kama hilo haliwezekani basi ruzuku kwenye mbegu na mbolea ipate kuongezeka ili gharama ya pembejeo hizi muhimu kwenye nchi hii zikapate kushuka ili gharama ya kilimo ikapate kupungua, hilo ni jambo langu la tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne la muhimu ni bima kwenye sekta ya kilimo. Watanzania wakulima ambao wamekuwa wakilisha Taifa hili kwa muda mrefu, wamekuwa wakilima bila uhakika, wanalima kwa kubahatisha, hawajui watavuna au hawatavuna. Wakulima wamekuwa wakiingiza fedha nyingi wamekuwa wanaingiza nguvu nyingi kwenye kilimo..

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa

**TAARIFA**

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nimpe taarifa. Kwa bahati mbaya wakulima hata watakapovuna hayo mazao ambayo wamelima kwa shida, Serikali ikinunua haiwalipi fedha kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Hiyo ni taarifa kweli? Endelea na mchango.*(Kicheko)*

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Kwa hiyo nilichokuwa nataka kuongelea hapa wakulima wamekuwa wakiingiza nguvu, wakiingiza fedha kwenye kilimo lakini kukija na majanga kama wadudu, majanga kama ukame na vitu vingine wanakuwa wanapoteza kila kitu kwa kuwa hatuna bima ya kilimo kwenye nchi hii, tuna makampuni machache sana yanayotoa bima na hawa wanatoa bima ni aghari sana wananchi hawawezi ku-*afford* lakini watanzania wengi hawana uelewa wa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshauri moja ni kwamba, tuje na mikakati ambayo itasaidia kuwa na taasisi nyingi zinazotoa bima lakini bima hizo zikapate kutolewa kwa bei rahisi ili wakulima wengi wakapate ku-*cover risk* ambazo zinatokana na kilimo.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kengele ya pili.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shigongo ajiandae Mheshimiwa Ndulane ajiandae Mheshimiwa Salim Hasham

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mungu muweza wa yote kwa kunipa nafasi ya kusimama jioni hii ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo mengi ambayo amelitendea Jimbo langu la Buchosa. Wananchi wa Buchosa wote kwa ujumla wao wanamshukuru Mheshimiwa Rais wao kwa barabara, maji, vituo vya afya na mambo mengi na kwa kweli tunasubiri utekelezaji kulipa fadhila zetu mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa leo nizungumze kile ambacho mimi naamini kwamba ni ukweli wangu. Nafahamu katika nchi yenye watu milioni 60 hatuwezi kufanana Mawazo yetu wakati wote. Tunatofautiana Mawazo, huyu atakuwa na Mawazo haya, mwingine na Mawazo yale. Kwa hiyo, nimepewa nafasi hii niweze kusema kile ambacho mimi naamini kitaweza kulisaidia Taifa langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkononi mwangu hapa nimeshika kitabu, kitabu hiki kinaitwa *The Checklist Manifesto, How to Get Things Right*. Kitabu hiki nilikisoma baada ya kuona kwamba sifanikiwi kwenye mambo mengi. Nilikuwa nikifanya mambo mengi lakini sipigi hatua na wala nikienda nasimama, nikienda nasimama nikalazimika kutafuta kitabu hiki nikakisoma. Baada ya kusoma kitabu hiki kimebadilisha kabisa maisha yangu na ninaamini kwamba kama nchi ya Tanzania ilivyo na ninawashauri Waheshimiwa Wabunge tutafute kitabu hiki tuweze kukisoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama nchi inahitaji *checklist manifesto*, orodha ya mambo ambayo tunataka kuyafanya, wazee wetu mwaka 1961 walikuwa na *Checklist Manifesto* baada ya uhuru wakasema tunayo madini mengi ardhini lakini tunayatunza yatachimbwa na watoto wetu. *Checklist Manifesto*, wameyatunza madini yale tumekuja kuyachimba sisi. Kwa hiyo, leo tunapokaa hapa kukaa kuzungumza tunajadiliana *checklist manifesto* ya nchi yetu. Tunataka kufanya nini ndani ya miaka mitano, tunataka kufanya nini ndani ya miaka 20 *checklist manifesto. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila *checklist manifesto* hatuwezi ku-*achieve* kitu chochote. Binafsi sina mashaka yoyote na Mheshimiwa rafiki yangu Profesa Mkumbo kwa uwezo wake na kwa uzalendo wake, lakini lazima tupange nini tunataka tukifanye ndani ya muda gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa nikiamini ya kwamba tunayo kazi kubwa ya kubadilisha Taifa letu, lakini hatuwezi kubadilisha Taifa hili kwa wakati mmoja kwa mambo yote. Ningependa tujiulize leo tunataka Tanzania ya namna gani? Tunataka Tanzania yenye nini baada ya miaka 50 au miaka sitini ijayo? Hilo ndilo jambo la kujiuliza leo na tunaanza kufanya kazi moja baada ya nyingine kwenye *checklist* yetu tuna-*tick* kitu kimoja kimoja hatimaye tutimize vitu vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *checklist manifesto* yetu sisi kama Watanzania tunataka kufanya nini ambacho watoto wetu watakaokuja watakuja kutusifia nacho, kwamba wazazi wetu walitangulia walifanya mambo haya ambayo yamekuwa na faida kwetu. Kwa hiyo, tumekutana hapa kujadili Mpango na Mpango nimeusona una mambo saba Mheshimiwa Mkumbo ameyaorodhesha pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza sisi kama Watanzania, sisi kama Wabunge, sisi kama watu waliotumwa tunataka ku-*achieve* kitu gani, tunataka tukumbukwe kwa jambo gani kama Bunge la

Kumi na Mbili, tunataka Rais wetu wa Awamu hii ya Sita akumbukwe kwa kipi? Lazima tuwe na vipaumbele, hatuwezi kuyamaliza matatizo yote kwa wakati mmoja lazima tu-*set priorities,* kipi katika *list* yetu yote ile tunataka tuanze na kipi kifuate nini? Hilo ni jambo ambalo nimelikosa wakati nasoma Mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji tukubaliane tunataka tuanze na barabara, tunataka tuanze na maji, tunataka tuanze na umeme ili mwisho wa siku tumalize kimoja baada ya kingine. Tukifanya hivyo tutamaliza mwisho wa siku itajulikana kwamba Rais wa Awamu ya Sita alishughulika na *healthcare,* Rais wa Awamu ya Saba alishughulika na barabara, Rais wa Awamu ya Nane alishughulika na maisha ya watu, hiyo ndiyo *checklist manifesto*, nimefanya hivyo maishani mwangu na maisha yangu yamebadilika. Tunayo sababu ya kuwa na *checklist manifesto*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimeusoma Mpango huu na nimeuelewa ya kwamba tunatakiwa tupange kipaumbele ninachokitafuta tunaanza na nini, kinafuata nini, tunakuja nini na tunamalizia na nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo nataka kuliongelea hapa leo ni suala zima la mapato, ukurasa wa 21 pameandikwa tutaongeza mapato katika Mpango huu. Ninao ushauri wa kutoa, jambo pekee litakaloongeza mapato katika nchi ni kuboresha sekta zetu. Sekta zetu zimeshindwa kuchangia vya kutosha kwenye Pato la Taifa. Nchi hii ni Tajiri sana na wote tunafahamu lakini sekta zetu zimeshindwa kabisa kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi huwa natoa mfano wa Venezuela nikiongea, Venezuela ni nchi tajiri sana ya mafuta namba moja Duniani inafuatiwa na Saudi Arabia lakini Venezuela ni nchi maskini kuliko Tanzania kwa sababu wameshindwa kutumia utajiri wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utajiri tuliopewa na Mungu tuutumie kuingiza fedha kwenye kapu la Taifa. Tukiingiza fedha kwenye kapu la Taifa nataka kukuhakikisha ya kwamba fedha zitakuwa nyingi na mwisho tutakuja kufikiri hata kupunguza kodi kwa wafanyabiashara wetu. Tuwapunguzie *VAT* tukipinguza *VAT* lazima tutaongeza *compliance* ya wafanyabiashara waweze kulipa kodi kwa wingi, tukifanya hivyo tutakuwa tumesaidia sana nchi yetu, *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwawezesha wazawa kiuchumi tuwawezesheni watu wetu washikilie uchumi wa nchi yao, nimeshaongea sana jambo hili mara nyingi, tuwapeni fursa Watanzania washiriki kwenye kukuza sekta binafsi tuwape mitaji, tuwape fursa mwisho wa siku wakipata fedha Watanzania wataitumia hapahapa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee jambo la mwisho, *National Innovation Fund,* nimeshazungumza sana hapa, kwamba tuna vijana wengi wabunifu kwenye Taifa letu hawana mitaji, kama tuna Mfuko wa Kilimo, tuna Mfuko wa Filamu, tunayo Mifuko kadhaa tumeanzisha, tunashindwaje kuanzisha *National Innovation Fund?* Tuwasaidie wabunifu wetu wanatoka Chuo Kikuu hawana mitaji, watengeneze *products*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina vijana wengi sana wabuni. Kuna mtu ametengeneza mashine za kusaga, mtu wa Darasa la Saba. Leo hii huko Iringa hawanunui mashine za Kichina wananua mashine za mtu huyo. Asaidiwe. *National Innovation Fund* itakopa fedha kutoka *Global Innovation Fund*. *Global Innovation Fund,* ni mfuko wa dunia ambao matajiri wakubwa kama akina Bill Gates wanapeleka fedha pale. Fedha hizi siyo mkopo, unaandika tu barua, unapeleka maombi, unapewa *grant,* na unawapa watu wako bila riba yoyote. Naamini tukianzisha *National Innovation Fund,* tutawasaidia sana vijana wetu wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Profesa Mkumbo, tumekuamini, tumekupatia

jukumu la kutuendeshea mipango ya ychi yetu. Nataka nikwambie kaka, fanya jambo hili kwa uaminifu wako wote, kwa akili zako zote. Kwa sababu tumekupa *responsibility* na *authority,* mwisho wa siku tutaku-*hold accountable*. Tukifeli kama Taifa tutakushika mkono wewe. Bahati nzuri uliwashawahi kuwemo ndani halafu ukatoka, tumekurudisha tena, ukituharibia tutakutoa tena. Tukikutoa safari hii hatukurudishi tena. Kwa hiyo, nataka nikwambie Mheshimiwa Prof. Mkumbo, fanya kazi yako kwa akili zako zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshatoa ushauri, Waziri aunde kitu kinachoitwa *National Economic Planning Think Tank.* Wako watu kwenye Taifa hili wana akili nyingi japo hawana *certificate* wala *degree,* wala *Ph.D.* Wachague hao watu wakuzunguke wawe wanakupa ushauri. Ninaamini kabisa ya kwamba ukifanya hivyo utapata mawazo mazuri sana kutoka kwa watu na utafanikiwa kwenye kazi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni wizi. Sikuchangia kwenye Ripoti ya *CAG,* niliamua niache kwa sababu mara ya mwisho niliongea sana kuhusu wizi, lakini ngoja niligusie tena leo. Tunakusanya fedha lakini zinaibiwa. Kwenye Taifa hili ni kama kuna pepo wa wizi anazunguka. Kila mtu anataka aibe, lazima mpango huu unioneshe ya kwamba wizi utadhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hapa ni *pen*. Kwa watu wengi hii ni kalamu, lakini wasomi mtanisamehe, simaanishi wasomi wote. Kwa wasomi wengi hii siyo kalamu, hii *SMG*, hii *AK-47*

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Wanatumia hii kuiba fedha zetu. Ni lazima tuwathibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu utamke kwamba watu watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria tulizonazo. Tuna sheria tano tumetunga ndani ya Bunge hili; Sheria ya Fedha, Sheria ya

TAKUKURU, Sheria ya Manunuzi, Sheria ya Watakatishaji Fedha, Sheria ya Uhujumu Uchumi na bado kuna Sheria ya Jinai. Tutumie sheria hizi kuwadhibiti watu wanaotuibia,

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anisikilize. Nataka nimwambie jambo, kuna bomu linakuja mbele. Ndani ya Wizara yake kuna Kitengo kinaitwa *TSA* kama sikosei, watu hawa wanaiba fedha, wanazituma kwenye halmashauri, halafu zinatoka kwenye halmashauri zinarudi kwao. Naomba kaka yangu ninakupenda, nenda kawadhibiti Watu wa *TSA* watakuingiza kwenye matatizo. Wanatuma pesa kwenye halmashauri… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili, ahsante.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mengine mwandikie. Mheshimiwa Ndulane, jiandae Mheshimiwa Salim Hasham.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2024/2025. Awali ya yote napenda kumpongeza *schoolmate* wangu wa *Pugu High School*, Profesa Kitila Alexander Mkumbo, pamoja na rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Waziri wetu wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ambaye pia ni *schoolmate* wangu katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza kwa sababu wametuletea taarifa nzuri zenye mwelekeo mzuri, lakini sana nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa kutuonesha dira kupitia hotuba yake aliyoitoa tarehe 19 mwezi Machi mwaka 2021 wakati alipoapishwa kushika hatamu za uongozi wa nchi yetu. Pia, kwenye hotuba yake aliyoitoa hapa Bungeni siku ya tarehe 22 mwezi Aprili, mwaka 2021, kwa kweli imezingatiwa kwa kiwango cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ningependa kuchangia katika sekta mbili tu; Sekta ya kwanza ni ya utalii na sekta ya pili ni ya mifugo. Tumeona kwenye taarifa ongezeko la mapato na idadi ya watalii katika nchi yetu imeongezeka sana na mapato ya Serikali yetu yameongezeka sana kupitia sekta hiyo. Takwimu zinaonesha kwamba mwaka 2021 watalii waliongia hapa nchini walikuwa 922,692, lakini mwaka uliofuata mwaka 2022, waliongezeka hadi kufikia 1,454,920 sawa na ongezeko la watalii takribani 500,000 hivi sawa na asilimia 57.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili limewezesha ongezeko la fedha zilizopatikana kutokana na sekta hii toka dola milioni 1.31 mwaka 2021 hadi kufikia dola milioni 2.53 mwaka 2022. Ni ongezeko kubwa na hili linaonesha namna ambavyo tumekuja kunufaika kutokana na maono ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia ile Filamu ya *Royal Tour*. Narudia kumpongeza Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia vizuri hizi taarifa zote tatu, sijaona mwendelezo wa *Royal Tour.* Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri tuone namna ambavyo tutaendeleza mwenendo mzuri uliotokana na Filamu ya *Royal Tour.* Kwa sababu hata taasisi za Kimataifa ambazo zilifanya *assessment* ya shughuli za utalii zinavyoendeshwa hapa Tanzania na nchi nyingine za kiafrika imei-*rank* nchi yetu kuwa namba moja kwa vivutio vingi vya utalii. Duniani imekuwa *ranked* kama namba 12. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa. Haya hayatufanyi tubweteke, tunatakiwa tubuni vyanzo vipya kama ambavyo malengo yetu ambayo yameandikwa kupitia huu mpango yalivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza au naishauri Serikali, tuwe na mkakati wa kuwa na *Royal Tour* Na. 2 au *Phase II*. Naomba tuweze kuzingatia maeneo yafuatayo: moja, katika hii *Royal Tour* Na. 2 tuyatazame maeneo ya hifadhi zetu za Taifa, tukianzia na ile ya Ruaha, tuangalie kule misitu ya Udzungwa, pori la Akiba la *Selous,* twende tukaioneshe dunia maajabu ambayo Mwenyezi Mungu alituumbia sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niliona tunahitaji kuwekeza katika malikale kupitia hiyo *Royal Tour* Na. 2. Pale Kilwa kuna Magofu ya Kilwa Kisiwani yaingie, Songo Mnara yaingie, viboko *albino* pale Pindiro, Makangaga yaingie, viboko katika Bwawa wa Maliwe au Ziwa la Maliwe pale Mitole liingie, vilevile kumbukizi za mambo mbalimbali ya kale kama vile Vita vya Majimaji kule Kilwa pale Nandete, Kibata na maeneo mengine na kule Songea pia, yaingie katika *Royal Tour*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi hapa alikuja hata Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Shirikisho la Ujerumani, alifika mpaka Songea. Hiyo inaonesha kwa jinsi gani hata watu walio nje ya nchi ambao tulikuwa tunashirikiana kwa majukumu mbalimbali siku zilizopita, bado wanaikumbuka Tanzania na wanaona kuna fursa nyingi za kuweza kushirikiana nasi. Kwa hiyo, naomba hilo nalo liingie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna utalii wa mapango. Kati ya mwaka 1994 na mwaka 2000 kulikuwa na Wataalam wa Kijerumani walikuja hapa nchini wakafanya utafiti kwenye mapango 25, wakiongozwa na Albert Daniel Galabawa. Walianzia Tanga, wakafanya *exploration* ya mapango tisa yakiwemo nane ya Amboni, lakini kulikuwa na mapango mengine Zanzibar moja, kule wanaita Mangapwani, pia walikwenda katika Milima ya Matumbi ndani ya Jimbo langu Kilwa Kaskazini, walifanya *exploration* na utafiti kwenye mapango 15, likiwemo Pango la Nang'oma ambalo ni kubwa, namba moja katika Afrika Mashariki kulikuwa na Pango la Naliotoke, kulikuwa na pango la Kiongolo, Mpachawa, Kilindima,

Namaingo, Lupondo, Kibwe, Shingya, Kimambo, Nampombo, Likolongomba pamoja na pango la Mtumbukile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu ule utafiti umefanyika, hakuna uendelezaji wowote uliofanyika. Hata Waheshimiwa Mawaziri tu, nakumbuka Waziri mmoja tu alifika mwaka 2021 katika Pango la Nang'oma lile ambalo nimesema ni kubwa kuliko yote Afrika Mashariki. Kwa hiyo, nilifikiri hapa tunapaswa kujenga *Information Center,* lakini vilevile tuone namna ambavyo tutaendeleza hivi vyanzo vya utalii. Nina hakika nchi yetu itapiga hatua katika sekta ya utalii na vilevile tutaweza kupata pesa mara tatu hadi mara nne inayotokana na hivi vyanzo ambavyo inaonekana vimesahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikenda kwenye sekta ya mifugo, naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Sisi Tanzania hapa hatufugi, tunachunga. Hii imepelekea changamoto kubwa. Kuna uharibifu wa mazingira ambao unapelekea kuwepo kwa athari za tabianchi lakini pia kumekuwa na mapigano ya mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha tuna mifugo isiyopungua milioni 28.3, lakini mifugo hii inachungwa, imezagaa tu nchi nzima. Ni lazima tuwe na mipango mizuri ya kuendeleza sekta hii ya mifugo, vinginevyo tutaendelea kushuhudia majanga, tutaendelea kushuhudia matatizo; achilia mbali migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imejaa kule hasa Mkoa wetu wa Lindi katika Wilaya za Kilwa, Nachingwea pamoja na Wilaya ya Liwale. Pia hata miundombinu ya hii mifugo haipo. Tumesomewa hapa kwenye taarifa, kuna ujenzi wa majosho 246. Sasa majosho 246 kwa mifugo milioni 28.3, wapi na wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utoaji wa chanjo, mifugo 696 imetolewa kwa mwaka uliopita. Hii mifugo 696 kwa mifugo milioni 28.3 wapi na wapi? Bado hatujafanya juhudi za kuhakikisha kwamba tunaidhibiti hii mifugo, lakini tunaifuga katika namna ya

kisasa ili iweze kuzalisha kwa kiwango cha kutosha. Kwa hiyo, nimeangalia hata ulaji wa nyama, inaonekana sisi katika *top ten* hatumo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali ichukue hatua za kutosha ili kuzuia haya mapigano ya wafugaji na wakulima, na pia kuruhusu sekta nyingine nazo ziweze kushamiri na kutuleta fedha nyingi, kuzalisaha ajira na kutuletea maendeleo katika nchi yetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Salim Hasham, jiandae Mheshimiwa Kembaki na Mheshimiwa Balozi Mulamula.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi siku ya leo ya kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake kwa sababu wanafanya kazi nzuri sana. Nawapongeza kwa sababu kazi zinaonekana na sisi Wabunge wote humu ndani ni mashahidi wa kazi ambazo zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajielekeza kwenye kuchangia kwenye Wizara ya Afya na nikiapata nafasi nitachangia kwenye Wizara nyingine. Tunaishukuru sana Serikali na tunamshukuru sana Mama Samia Suluhu Hassan kwa sababu kiukweli tumepata vituo vya afya vingi sana pamoja na zahanati za kutosha sana kwenye majimbo yote ambayo Wabunge wanayamiliki. Haipingiki kwamba kazi hizi nzuri zinafanywa na Serikali ya Awamu ya Sita lakini haina maana kwamba hakuna changamoto ambazo zinaendelea kwenye maeneo yetu hasa kwenye huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mifano kadhaa kwa sababu changamoto hizi bado zipo. Kwenye mwaka wa fedha 2023 tulipata

pesa shilingi milioni 200 kwenye jimbo langu. Nakupa mifano kwa sababu kuna changamoto nimeiona kati ya *MSD* na Serikali yetu. Nilipata shilingi milioni 200 ziligawanywa kwenye makundi mawili. Shilingi milioni 50 ilikuwa imeenda kwenye Zahanati yangu ya Minepa lakini shilingi milioni 150 imeenda kwenye kituo cha afya kipya kabisa kwenye Tarafa yangu ya Lupilo Kata ya Iragua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018/2019 tulipata pesa shilingi milioni 300 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye Kituo cha Afya cha Lupilo. Mpaka hivi ambavyo ninaongea, shilingi milioni 50 kwenye Zahanati ya Minepa tumepata vifaa vya shilingi 3,800,000 toka mwezi wa Tano tumewalipa *MSD,* lakini pia kwenye vifaa tiba, kwenye Kituo changu cha Afya cha Iragua tumepata vifaa vya shilingi milioni 25 kutoka kwenye shilingi milioni 150 tangu mwezi wa Tano. Kwenye fedha tuliyoipata tangu mwaka 2018/2019 tumepata vifaa, bado tunadai vifaa vya milioni shilingi 106 kutoka *MSD*. Sasa hilo ndilo ambalo nililokuwa nataka kulizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa upana kabisa, kwanza kuna tatizo kwa sababu inaonekana pia Sheria za Manunuzi zimekiukwa kwa sababu *supplier* huyu anaonekana alilipwa kabla ya ku-*supply* vitu ambavyo sisi tunavihitaji. Muda unaenda kwa sababu limeshapita, tufunike kombe mwanaharamu apite, ameshalipwa, lakini kwa nini ha-*supply?* Kitu ambacho nimekiona kwa *MSD,* na hapa Wabunge wenzangu wapo ni mashahidi, ukizungumza na Ma-*DMO* wanakwambia kabisa tatizo lipo *MSD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *MSD* ni kazi inayofanyika kati ya Serikali na *MSD*. Labda Serikali ituambie kuna tatizo gani kati ya *MSD* na Serikali? Kwa sababu inaoneka *MSD* wanafanya kazi vile ambavyo wao wenyewe wanajisikia kufanya. Unalipa hela mwaka 2019, leo miaka mitano vifaa vya shilingi milioni 300 havijafika kwenye hospitali yetu. Leo hii tunataka tudumishe afya bora na huduma bora za afya kwenye maeneo yetu. Namwomba sana dada yangu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa sababu amesikia changamoto hii, naomba anisaidie niweze kupata vifaa tiba ili

wananchi wake na wananchi wangu pia waweze kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimesimama hapa karibu mara mbili kwenye Bunge hili hili nikitoa maelezo juu ya hospitali yangu ya wilaya ilivyochakaa, ina miaka zaidi ya 60. Mnamo mwaka 2017/2018 tulipata pesa za ukarabati, shilingi milioni 400, ilishindikana kufanya ukarabati kwenye hospitali ile kwa sababu ni hospitali kongwe na ni chakavu. Matokeo yake tukalazimika kuongeza majengo kwenye hospitali ile. Hivi ninavyokwambia sasa hivi, eneo lote limejaa na hatuwezi kufanya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali kwa sababu ni kongwe, watu walikuwa 50,000 sasa hivi wameshafika kwenye 200,000, hospitali ile haiwezi kuhudumia tena wananchi wale. Ukiacha hilo pia, kuna kaka yangu, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Biteko, Mheshimiwa Naibu Waziri alijitahidi sana kutafuta wawekezaji kwenye jimbo langu na tumepata makampuni karibu mawili na yote yameshasainiwa mkataba. Wanaenda kuajiri wafanyakazi zaidi ya 1,000 waajiriwa rasmi, na ajira ambazo siyo rasmi ni zaidi ya 3,000 mpaka 5,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni aibu kubwa sana leo hii wawekezaji wale wanaenda kutafuta hospitali kwenye wilaya inayofuata au mkoani kwa sababu sisi hospitali ya wilaya hatuna. Dada yangu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu nilikuomba mara ya mwisho hapa, kama huamini haya ambayo nakwambia, twende ukajionee mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nimeletewa shilingi milioni 900 za ukarabati tena kwenye hospitali ile ile ambayo nimesema kwamba haikarabatiki. Tunashukuru tumepata, lakini tunawaambia kwamba changamoto yetu haikuwa hiyo. Halafu mimi niliyesimama hapa mbele ndio Mwakalishi wa Wana-Ulanga, ndio najua shida za Wana-Ulanga. Leo hii hamnisikilizi mimi, sasa sijui mtakuwa mnamsikiliza nani? Kwa hiyo, namwomba dada yangu, Mheshimiwa

Ummy Mwalimu na hili nalo alichukue tusaidiane. Tuna shida ya kupata hospitali ya wilaya kwa sababu kwetu imeshakuwa ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda wangu bado unanitosha, naomba nichangie kwenye sekta ya kilimo. Hatuna budi kuwekeza kilimo chetu kwenye skimu za umwagiliaji. Kama tunataka tupate tija kwenye kilimo nchi hii kwa sababu asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima, basi ni lazima tuwekeze kwenye skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu kuna skimu kama nne ambazo zinahitajika kwenye Jimbo langu. Kuna Skimu ya Minepa ambayo haijaisha, lengo iishe iweze kuwafikia wananchi wengi zaidi. Kuna Skimu ya Lupilo ambayo imeshafanyiwa *study*, kuna Skimu ya Lukana ambayo imeshafanyiwa *study* na kuna Skimu ya sehemu moja Kata ya Euga ilijengwa tangu nikiwa mdogo haijawahi kutumika mpaka imeharibika na sijui tatizo ni nini? Huu unaonekana kabisa ni uharibifu wa fedha za Serikali kwa sababu zilitumia fedha kujenga ile skimu lakini haikutumika kwa sababu haikuisha, leo hii tunaenda tena kuianza kuijenga upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo la pili ambalo linaendelea kwenye maeneo yetu kwenye majimbo yetu; suala la stakabadhi ghalani. Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyokuwa Singida alielekeza watendaji wake kwa maana ya Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi waende wakaangalie namna sahihi ya kuliingiza zao la mbaazi kwenye kuliuza kwenye stakabadhi ghalani. Jamani haikuwa sheria, kuna baadhi ya watendaji wetu na viongozi wana tabia ya kumfurahisha Mheshimiwa Rais, hatuko hapa kwa ajili ya kumfurahisha Mheshimiwa Rais jamani. Tuko hapa kwa ajili ya kumsaidia Mheshimiwa Rais na wale ambao huwa wanafanya maamuzi ya kumfurahisha Mheshimiwa Rais mkifika wakati wa uchaguzi hawaingii uwanjani kucheza, wanatuletea shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo wananchi hawako tayari kulifanya, halina afya kwa wananchi wala halina afya kwa sisi viongozi ambao wa kuchaguliwa katika maeneo yetu, kwa sababu ukifanya hivyo wananchi hawa kuna mwananchi analima yuko sehemu ya mbali kabisa ana debe zake mbili ghala liko kilometa 50 kutoka alipo, abebe debe mbili aende akauze, nauli peke yake shilingi 20,000? Hii mimi naona kwa kweli kwa upande wetu halina afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata maghala hayapo, mnataka mtu anafanya *implementation* kuhakikisha kwamba anatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais lengo amfurahishe Mheshimiwa Rais lakini halijamsaidia Mheshimiwa Rais kwa sababu anaowafanyia vile ni wananchi ambao Mheshimiwa Rais mwaka 2025 tunategemea kwamba ataingia uwanjani na wale wananchi tunatakiwa kupata kura kwa ajili yake. Naomba Mheshimiwa Bashe kama unanisikilza hili suala halina afya kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna budi kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake lakini ndani ya hivyo hivyo vitu pia, ndani ya vitu ambayo wanavifanya changamoto bado zipo ndiyo kama hizi ambazo tunazieleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Michael Kembaki, ajiandae Mheshimiwa Balozi Mulamula, ajiandae Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu.

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo anawajali wana wa Tarime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana kwa sababu kulikuwa na tatizo kubwa sana katika Jimbo letu la Tarime Mjini ambapo kulikuwa na madai ya muda mrefu ya fidia katika Mtaa wa Kinyambi na Bugosi ambapo kulikuwa na mgogoro kati ya Jeshi na Wananchi wa Mtaa ule. Mheshimiwa Rais alitoa pesa na wale wananchi wakalipwa. Kwa niaba ya wana wa Tarime nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo aliweza kusikiliza kilio chao na kuweza kuwalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tulikuwa na tatizo kubwa la ukosefu wa soko katika Mji wetu wa Tarime. Ametoa zaidi ya shilingi bilioni 9.5 na ujenzi ule sasa unaelekea kukamilika na sisi tunategemea wafanyabiashara wa Tarime wapate sehemu ya kufanyia biashara ambayo ilikuwa ni tatizo kubwa katika kipindi cha muda mrefu. Hizi ni baadhi ya mambo makubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya katika kipindi cha miaka mitatu cha uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nichangie Mpango kuelekea katika upande wa vijana. Ukizingatia kwamba vijana ni wengi katika nchi hii na vijana wengi hawana ajira, ningependa niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango pamoja na Waziri wa Fedha kwa namna ambavyo wamekuja na Mpango mzuri ambao umezingatia vile vile vijana kwa upande wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2024/2025 ulikuwa umelenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi ambao ni jumuishi unaopunguza umasikini, unaozalisha ajira kwa wingi, unaotengeneza utajiri na unaochochea mauzo ya bidhaa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa nilenge sana upande wa ukosefu wa ajira kwa vijana. Tatizo la ajira katika Nchi yetu ni kubwa sana na ni kubwa, kubwa, kubwa, kubwa. Imekuwa tatizo kubwa mpaka watu wanapoanza kuomba ajira wanadanganya kwamba ni walemavu ili waweze kupata

upendeleo wa kupata ajira. Mwaka uliopita waombaji kazi 419 walidanganya kwamba ni walemavu ili waweze kupata ajira na hii inadhihirisha ni namna gani tatizo hili ni kubwa katika Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walioomba kazi walikuwa 171,916 na waliopata kazi katika upande wa walimu walikuwa 13,130. Katika upande wa Afya waliopata kazi walikuwa ni 5,319. Kwa hivyo jumla ya waliopata ajira kati ya 171,916 walikuwa 18,449. Kwa hivyo waliobaki 153,512 hawa walibaki bila ajira wakienda mtaani. Jumla mwaka 2014 watu 1,000,000 kwenda kuomba kazi katika idara ya uhamiaji na huku watu 70 ndiyo walikuwa wanahitajika kwa mwaka huo. Kwa hivyo watu 930 walitoka pale bila ajira na walienda mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ripoti ya Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umasikini Tanzania *(REBOA)* ya mwaka 2019, vijana 1,000,000 wanahitimu katika vyuo mbalimbali na uwezo wa Serikali pamoja na Sekta Binafsi wa kutengeneza ajira ni 2,500. Unaweza kuangalia namna tatizo hili lilivyo kubwa ndiyo maana tunao machinga wengi mitaani, tunao boda boda wengi ambao hawapendi kufanya ile kazi lakini kwa sababu hawana kazi ndiyo maana wamejiingiza katika kazi ile ili waweze kupata *at least* kipato cha kuwaweka waendelee kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo letu la Tarime Mjini wapo watu waliojiwekeza kuchimba madini wadogo wadogo. Katika kuchimba wanapokuwa wametoka shimoni wamechimba madini yao, wanapotoka nje tayari wanatozwa ushuru bado hawajauza lakini bado hata hawajapata chochote kutokana na wanatozwa kulingana na udongo waliopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna vijana ambao wanatoa bidhaa Kenya wanakuja kuuza Mji wa Tarime. Kutokana na kwamba bidhaa nyingi ambazo zinatoka Kenya kuja Tarime pale *at least* bei yao inakuwa chini. Anapokuwa amepita na *cement* 10 kwamba aje

auze Tarime hawezi kulipa kodi kwa sababu mfumo hauruhusu kulipa kodi bidhaa ndogo ndogo. Hii inasababisha vijana wale wapite kwa njia ya magendo na Serikali inapoteza fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ndilo lililosababisha Serikali ikaja na Mpango wa Maendeleo 2024/2025 na katika Mpango huu kuna *Program* ya Taifa ya kukuza ujuzi Nchini lakini pia kuna Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Ningependa nizungumzie *Program* ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini. *Program* hii iliandaliwa kwa ushirikiano kati ya Serikali pamoja na Sekta Binafsi kwamba waweze kutoza fedha kwa ajili ya kugharamia kukuza ujuzi wa vijana wetu kwa lengo la kuzalisha ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubaliano yalikuwa kwamba asilimia moja ya tozo hizo iweze kupelekwa kwa ajili ya kuendeleza ujuzi wa vijana. Kwa mwaka 2021 na 2022 makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 291 na kwa asilimia moja ilipaswa shilingi bilioni 97 ziende kuendeleza ujuzi wa vijana wetu lakini mambo yalikuwa tofauti. Mwaka 2015/2016 walipeleka shilingi bilioni 15, 2016/2017 walipeleka shilingi bilioni 15, 2017/2018 walipeleka shilingi bilioni 15, 2018/2019 walipeleka shilingi bilioni 15, 2019/2020 walipeleka shilingi bilioni 18, 2020/2021 walipeleka shilingi bilioni 18. Kuanzia 2021 mpaka 2022 walipeleka shilingi bilioni tisa, 2022/2023 wamepeleka shilingi bilioni tisa. Hii imesababisha vijana ambao walikuwa wananufaika 42,000 imeshuka sasa mpaka vijana 12 peke yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Mpango, vijana 681,000 walipaswa wanufaike na Mpango huu ndani ya miaka mitano lakini kwa namna ambavyo wanapeleka…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, kengele ya pili hiyo. Mheshimiwa Balozi Mulamula, ajiandae Mheshimiwa Riziki.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Nimefuatilia kwa umakini sana wasilisho la Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na mjadala unaoendelea niseme tu kwamba wasilisho lake ni zuri sana. Linatupa mwanga wa mbele tunapokwenda na kutupa matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa kuiondoa mipango katika Wizara ya Fedha na kuiweka chini ya Ofisi yake. Niseme katika nchi zilizoendelea mipango ndiyo huwa inaelekeza, inaongoza hazina na siyo vinginevyo. Nimefurahi sana kuwaona Waheshimiwa Mawaziri hao wawili Mheshimiwa (namwitaga pacha) Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo wakiwa wameketi pamoja kama mapacha kwa kuwasilisha Mpango wa Maendeleo na Mtazamo wa Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni mara yangu ya kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Kitila Mkumbo kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii. Kama wengi walivyosema ni msomi mwenye upeo na mawazo mapana, ana uwezo mkubwa na ushawishi mkubwa. Kwa hiyo, sifa zote hizi niseme ni muhimu sana kwa Waziri wa Mipango na sifa hizi zinaonekana pia katika wasilisho lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusikiliza wasilisho la Mheshimiwa Mkumbo na Mpango wenyewe niseme nimevutiwa na mambo matatu. Moja ni kuhusu maendeleo vijijini, lakini ya pili ni mabadiliko ya tabianchi, ya tatu ni uchumi wa kijani na uchumi wa buluu *(green economy and blue economy)*. Najua wamegusa maeneo mengi lakini nasema maeneo haya matatu yakisimamiwa

vizuri yanaweza kuwatoa Watanzania wengi kwenye wimbi la umasikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia nimesikitishwa kwamba Mpango huu bado haujaupa umuhimu wa kutosha shughuli za utafiti na maendeleo *(research and development)* imepewa pesa kidogo sana chini ya Sekta ya Elimu ambayo ni kama 0.003% wakati lengo ni kuwa na 1% ya pato la Taifa. Bahati nzuri nimekaa hapa na Mheshimiwa Profesa Mkenda na ninaamini kwamba na yeye pengine ana uchungu kuona kwamba Sekta hii imepewa hela kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bahati nzuri nimekuwa kwenye vyuo vikuu kwa Chuo Kikuu cha *George Washington University* na nikatumia muda pia kwenye *Massachusetts Institute of Technology* nikiona wenzetu hela kubwa sana inaenda kwenye *R and D.* Kwa hiyo, wito wangu kwamba Mheshimiwa Profesa Mkumbo kwa kweli hii muipe umuhimu sana ili tutoboe. Hii kwa kweli hatuwezi kuendelea kuipa *peanut. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nimevutiwa maeneo matatu muda ukinitosha nitaweza kuyaongelea lakini nianze na kuhusu maendeleo vijijini. Tumesikia shule nyingi zimejengwa, vituo vya afya vimefunguliwa, maji yanasambazwa, mambo mazuri sana na kwa lugha nyepesi tuseme Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonyeshwa kuguswa sana na wananchi vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeguswa pamoja na kwamba nimekuwa na nyadhifa mbalimbali nimekuwa nimekaa nchi za nje lakini mimi ni mtoto wa kijijini kama pengine walivyo wengi hapa na nilikuwa najiita *I am a rural girl* kwa hiyo, nafuatilia sana. Mzee wangu marehemu Mheshimiwa wakati ule marehemu sasa Novat Rutageruka alikuwa akisema, “Ukitaka kupima maendeleo tumefikia wapi tumetoka wapi, tumefika wapi angalia hali ya kijijini.” Kweli alikuwa ananiasa kila wakati anasema nakusikia kwenye mihadhara

huko na watu wa *World Bank* mnatoa takwimu, mnazipata wapi mbona hamtuulizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema naguswa sana na hali ya umasikini *of course* na maendeleo vijijini yanayoendelea na ninaamini kama tutajielekeza kuwapa maarifa na mtazamo wanavijiji baada ya kuwapelekea hizi huduma mbalimbali. Tumesema sasa hivi vijiji vingi vimepata umeme, minara ya mawasiliano imesambazwa lakini wanaitumiaje katika kupata maendeleo ambayo tunayataka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kijijini kwetu sehemu imeweza kupata umeme lakini kwa watu wetu umeme ni taa na sisi ni watu ambao siyo kama watu wa Kilimanjaro siyo watu wa biashara sana kwa hiyo mtu anafurahia na anawasha taa pengine anaweka na *TV*. Nadhani wananchi wetu wanataka elimu tuwaelimishe kwamba huu umeme waanzishe viwanda vidogo vidogo, waongeze thamani kwenye mazao yao katika maeneo waliyonayo na hiyo *BBT* nasema kwamba hiyo *BBT* ya kilimo ipelekwe pia kwenye masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa natoa ushauri tu kwamba pengine tufikirie kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo Vijijini *(Rural Development Authority)*. Maana yake huko nyuma tulikuwa na Wizara zinazohusika na maendeleo vijijini. Nchi zilizopiga hatua kwenye maendeleo vijijini nyingi zina Wizara na taasisi hizi. Sasa sisi shughuli hii imesambaa kwenye TAMISEMI, Wizara mbalimbali kwa hiyo inakuwa ni vigumu katika kuratibu. Kwa hiyo mimi naamini pengine Mheshimiwa Profesa Kitila anaweza akamshauri Mheshimiwa Rais kuangalia uwezekano wa kuanzisha *Rural Development Authority,* namuona ana-*note* kwa hiyo nadhani umelipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabianchi pia haina mwenyewe na yenyewe. Mabadiliko ya tabianchi na yenyewe muangalie jinsi gani inaweza ikawa na taasisi mbali na *NEMC* ya kuweza kuangalia

maana yake ni eneo kubwa zuri sana hasa tukiangalia katika *carbon credit*. Sasa hivi mkutano wa *COP 28* unakuja, itatoka maazimio mengine nani anayachukua? Kwa hiyo, nadhani itakuwa vizuri pia katika kutazama uchumi wa *green economy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani itakuwa vizuri pia kuwa na hiyo katika kutazama *green economy*. Mambo ya uvuvi yameongelewa, lakini nasema hiyo ni sehemu ambayo kwa kweli hatujaitendea haki. Uvuvi tunauona kama ni wa watu maskini lakini ndiyo *potential* kubwa iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabla hujanigongea kengele nyingine, niseme uchumi wa *blue* nao kwa kweli tujifunze mengi kutoka Zanzibar kwamba wameanzisha Wizara inayohusika na uchumi wa *blue*. Hii ni kweli kuna fursa nyingi sana ambazo hatujazitendea haki. Maana yake nayo imesambaa katika Wizara mbalimbali na sekta mbalimbali. Tuondokane na dhana ya *sector approach*. Profesa Mkumbo tuondokane na *sector approach* tutazame dhana ya uchumi *in a holistic manner*. Kwa namna hiyo nadhani itaweza kuleta yale ambayo tunatarajia kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nimpongeze Mheshimiwa Tulia Akson kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa *IPU*. Ushindi wake umenipa hamasa kwamba mgombea wa nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola kwamba inawezekana. Tukijipanga vizuri na kutumia ushawishi wetu mkubwa kidiplomasia na Kimataifa aliotujengea Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Naomba mniunge mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa balozi umesema tukuunge mkono au umeunga mkono?

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sawa.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo yote, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Riziki, ajiandae Mheshimiwa Anastazia Wambura na tunakwenda dakika nane nane kutokana na idadi ya wachangiaji kuwa ni wengi.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia kuwepo hapa na kwa kutujaalia sote. Sina mengi ya kusema zaidi ya kumshukuru Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais yuko katika kipaumbele, hana ubaguzi, ana mapenzi na watu wote hata ikiwemo watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua Waziri wa Fedha ni balozi wa watu wenye ulemavu, katika Bunge la Bajeti alitoa ahadi ndani ya Bunge hili kuwa atatoa shilingi bilioni moja kwa ajili ya maendeleo ya watu wenye ulemavu katika Wizara ya Kazi, Ajira na Watu Wenye ulemavu. Kwa kweli watu wa Mheshimiwa Waziri wanatuangusha, ni kizunguzungu ambacho kinakuwa hakina mwisho, watu wenye ulemavu wanashindwa kufanya kazi zao na wanashindwa kufanya majukumu yao. Hizi hela alizozitenga Waziri shilingi bilioni moja mpaka leo hazijafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kwa hili ana uwezo nalo. Balozi wangu mtukufu, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba afuatilie hilo suala ili tuondokane na hilo iwe mwisho leo hapa. Tukitoka hapa tunazungumza ukurasa mmoja. Fedha za watu wenye ulemavu zimeingia Wizara ya Ajira, Kazi na Watu Wenye Ulemavu. Mheshimiwa Rais anawapenda walemavu, amekaa nao zaidi ya mara tatu anakula nao chakula Ikulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye ni balozi na ni mlezi wa watu wenye ulemavu, tunakwenda na mpira watu wenye ulemavu *AFCON,* hatuna bajeti na hatuna pesa tangu mwezi Julai. Ilibidi wakakae kambini, hakuna uwezo. Hivyo naamini kuwa balozi wangu atalifanyoia kazi na najua yeye anawapenda walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, natoa shukrani za dhati, Wizara ya Ujenzi tayari ime-*deal* na wakandarasi. Wakandarasi walikuja karibu mabasi, amefanya nao kazi na tunaonekana tunakwenda vizuri. Wizara ya Uchukuzi, wakandarasi wa *ATCL* mafanikio yanaanza kuonekana. Walisema wametoa shilingi bilioni 10 zimepelekwa Hazina; Hazina wanakwamisha, naomba Mheshimiwa Waziri akae nao chini watu wake, hawa watu ni wastaafu, wamenyanyasika kwa miaka mingi sana; wanahitaji wapewe hela zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watu wa *ATCL* peke yao, watu 70 wameshafariki sasa hivi, hawakupata mafao yao, ni miaka 10. Watu wa *TAZARA* wamekufa watu 100 mpaka sasa hivi hawajapata mafao yao. Tumekwenda Wizara zote nimepita kutembea nao wamesema hela zilishapelekwa tayari hazina. Sasa bila Waziri kukaa chini na hawa watu watatu sisi hapa hatuna jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake itakuwa kila siku hawa wanapanda juu, wanateremka chini. Hakuna majibu, lakini hela zilishatengwa katika bajeti iliyopita, mpaka leo hatujui mafao haya yako wapi. Naomba Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu na upendo ninaompenda, naomba alisimamie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjusi, nilisahau kwa muda mrefu. Hili ni pato ambalo nchi italipata kwa kupitia mjusi. Ujerumani inapata pato la *dollar* bilioni 3.8 kwa watu kutembelea katika eneo lile la *exhibition* ya mjusi. Leo mjusi ametoka Lindi nilitegemea Rais wa Ujerumani angepewa taarifa kuwa yule mjusi ametoka Lindi na akatembelea Lindi. Amechukuliwa amepelekwa maeneo mengine,

sikatai. Vitu walivyoenda kumwambia sijui kuna mafuvu la machifu je, gawio letu la mjusi Mkoa wa Lindi liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *dollar* bilioni 3.8 siyo hela ndogo. Mjusi ametolewa pale hakuna barabara na hakuna shule. Tangu Mwaka 2005 nazungumza lugha ya mjusi, ifikie mahali tujiulize. Haya ni mafanikio ya nchi yetu, wenzetu Namibia wamefuatilia wamelipwa trilioni 4.0 na zinawasaidia. Sisi leo unaona pale hatuna shule, hamna barabara wala nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Serikali inapambana lakini kuna hela nyingine ni *direct* huhitaji hata kutumia nguvu, ni hela za mjusi. Natamani nikutane na Rais mwenzangu, maana yake ni Rais wa herufi ndogo, Rais wa Mjusi nilitegemea na yeye tungekutana nikamwambia hiki kilio chetu cha mjusi tunatamani tunataka mapato ya mjusi. Tutaendelea kupigania ni haki yetu ya msingi, watu wa Mipingo, watu wa Matapwa…

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Riziki naomba anivumilie nilitamani ijibiwe kesho, lakini kwa kuwa ameendelea kulisemea na nampongeza kwa namna ambavyo amekuwa ukilisemea suala hili kwa nia nzuri na kwa kweli tunamuunga mkono kama Serikali na Wabunge wengine wote ambao wamekuwa wakilisemea suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ratiba ya Rais wa Ujerumani alipotembelea Tanzania, walikuwa wameweka *schedule* yao na waliona watembelee eneo lile kwa muda mfupi waliokuwa nao, lakini pili nimhakikishie kama Serikali tayari kupitia mazungumzo

ambayo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya na Rais wa Ujerumani, tunayo Kamati ya Kiserikali yenye taasisi zaidi ya nane ambayo itasimamia suala hili. Baadaye tutaendelea na majadiliano ambayo Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia ametoa baraka zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuko katika taratibu za kidiplomasia kupitia Wizara ya Mambo ya Nje ili sasa mazungumzo rasmi yaweze kuanza. Hiyo inahusianana na *art fact* zote pamoja na vifaa vingine ambavyo ni kwa ajili ya kumbukumbu ya Tanzania ikiwemo pia na mjusi pamoja na mengneyo. Tuone huko baadaye pia wakirudishwa watatunzwaje pamoja na mengine. Kwa hiyo, nampongeza niliona nisisubiri kesho niliweke hivyo sawa na waunga mkono wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki, taarifa hiyo.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Angellah Kairuki. Bunge la Kumi na Moja nilizungumza, Watanzanoia tuwe tunahudhuria mikutano kwa wingi ili tupate nafasi mbalimbali hizi katika umoja wa mataifa. Nampongeza Mheshimiwa Angellah Kairuki amepata nafasi katika *UNWTO,* hii ni nafasi kubwa kama Makamu wa Rais.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo tunasema tunataka watu waadilifu, watu wanaoona maono kuwa tuna haki ya vitu vyetu kufanikiwa. Kupitia mikutano hii yetu na Spika wa Umoja wa Madola, leo vilevile tuna Makamu wa Rais wa *UNWTO,* tuna Rais Dkt.Ndugulile…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MH. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nimalizie.

**MWENYEKITI:** Sekunde mbili malizia.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la fungu. Kuna shilingi 20,000 za wafanya biashara ndogondogo, tunapoteza nchi. Kama tukipiga hesabu 20,000 kwa watu 30,000 tuna shilingi milioni 600, Wizara nne tayari tutakuwa tumezifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante mwandikie Waziri. Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Neema Mwandabila na Mheshimiwa Kanyasu wajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuunda Wizara ya Mipango, lakini pia nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuiongoza Wizara hii. Vilevile, nawapongeza wawasilisjhaji wote wawili ambao ni Mawaziri wetu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwa uwasilishaji wao mzuri na kimsingi tumeelewa ambayo wametueleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kugusia kidogo tu maeneo mawili ya kiuchumi ambayo tumeyaona katika mawasilisho yao, la kwanza ni kuhusiana na *export* ambapo ukisoma yale majedwali ambayo ametuonesha Mheshimiwa Waziri wa Mipango, utaona kwamba kuna mabadiliko kwa miaka 20 kuna mabadiliko ya *export* zetu. Kuna bidhaa ambazo zimeongezeka *volume* zake, lakini kuna bidhaa ambazo zimeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie mfano mmoja ni dhahabu. Dhahabu miaka ya 2000 ilikuwa iko chini sana, kwenye 5% hivi, lakini kwa miaka ya 2020 tunaona dhahabu imeongezeka imefikia 39%. Sasa tukija kwa upande wa zao la korosho mazao kwa ujumla lakini hasa zao la korosho utaona linasuasua na *export* imepungua

kidogo. Hapa nataka kusema nini? Ni kwamba mifumo na *testimony* yetu nzuri ni dhahabu kwa sababu ukiangalia kwa mfano miaka ya nyuma dhahabu ilikuwa inauzwa kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo kulikuwa hakuna takwimu zinazopatikana, lakini mapato mengi yalikuwa yanapotea hatujui kimeuzwa kiasi gani. Baada ya kuimarisha mifumo yamewekwa masoko ya dhahabu na kodi zake zimekuwa ni *reasonable* na kwa maana hiyo wafanyabiashara wamehamasika sana na wanapeleka bidhaa zao au dhahabu zao kwenye vile vituo vya kuuzia dhahabu na tunaona sasa *exports* zimepanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kushauri kwa upande huu wa *exports,* tuangalie mifumo, tuimarishe mifumo, lakini tufanye utafiti wa kina na kwa maeneo haya utaona kwamba hata zile nchi ambazo walikuwa ni wateja wetu mwanzoni, kuna wateja ambao tumewapoteza lakini tumeongeza wateja wapya. Kwa hiyo tunahitaji tafiti zaidi katika eneo hili kusudi tuweze kuimarisha *exports* zetu ambazo pia ndiyo nguzo kubwa ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee eneo la pili ambalo ni matumizi ya gesi asilia. Tuna gesi nyingi kwa takwimu ambazo tunaambiwa tuna trilioni *57 cubic feet reserve* ya gesi ambazo ni nyingi sana. Sasa hivi tuna mradi ambao unataka kuanzishwa wa *LNG* ambao naamini kabisa tukiitumia vizuri gesi yetu tunakwenda kupanda kiuchumi, tutaboresha maisha ya wananchi kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza matumizi ya gesi, yataokoa kwa kiasi kikubwa matumizi ya fedha za kigeni kuagizia mafuta nje. Pili, itapunguza matumizi ya Serikali kwa upande wa fedha. Gharama ambazo zinatumika kununua mafuta zitapungua kwa sababu gharama ya gesi ni ndogo. Kwa mfano mmoja tu, mtu anatumia karibu Sh.80,000 kutembea kilomita 600 ambapo ukitumia Diesel kwa bei ya Sh.3,500 kwa lita unaweza ukatumia Sh.350,000 ambapo sasa utakuja kuona matumizi ya gesi ni *almost* robo ya

matumizi ya mafuta. Hii itasaidia pia kupunguza gharama za usafirishaji na gharama za usafiri kwa wananchi wetu na itasaidia sana kupunguza gharama za maisha ambazo sasa hivi wananchi wetu wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo upande wa afya. Naishukuru sana Serikali, tuna miradi 49 ya afya kule Mtwara inayoendelea, lakini nashukuru tumepata *MRI* na tumepata *CT scan* katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Kanda ya Kusini na tumepata *digital x-ray,* tunaendelea vizuri, lakini tuna tatizo moja, vifo vya wanawake. Kule Mtwara vifo vya wanawake kwa mwaka jana, mwaka huu wa fedha 2022/2023 ni 84 kati ya vizazi hai 39, ambapo ukipiga *average* kati ya vizazi 100,000 utakuta kwamba ni juu ya ile *average* ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa namna ya pekee kabisa Serikali ituangalie kule Mtwara, watuletee Madaktari au wataalam wa afya kwa sababu tuna upungufu wa 69% ya wataalam wa afya. Kwa hiyo, naomba sana pamoja na yote ambayo Serikali imefanya tupatiwe wataalam wa afya na hasa wakunga. Wakunga ni muhimu sana katika kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo suala la mazingira, tuna usafirishaji wa makaa ya mawe ambayo yanatokea Mkoa wa Ruvuma, yanasafiri kwa Bandari ya Mtwara. Tunapata adha kubwa sana, vumbi lile lina athari kubwa sana kwa afya za wananchi. Naomba tena, nilishawahi kuomba humu ndani, tuna taarifa kwamba kuna ujenzi wa bandari ambao unakaribia kuanza. Bandari ambayo itashughulikia usafirishai wa makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule usafirishaji uzingatie basi kuwekwa kwenye makasha ili kusudi kuzuia lile vumbi wakati wa usafirishaji barabarani. Hata wakati wa kupakua ule mzigo na kupakia kwenye meli shida ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kidogo suala la tembo ambalo tumesikia mauaji ni mengi sana. Naomba nishauri kidogo, tuweke mpango mzima wa kutumia *drones* ili kufukuza tembo …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, mwandikie Waziri.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, jiandae Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi pia kuweza kushiriki kuchangia katika mpango huu. Natamani leo nitumie nafasi yangu vizuri kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amefanya kazi nzuri sana ya kuleta fedha nyingi kwenye mikoa yote na hususan kwenye Mkoa wangu wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ambavyo madarasa mengi yamejengwa, vituo vya afya vingi vimejengwa. Kiukweli ukiangalia unaona kabisa ile ni nguvu ya ziada ambayo Mheshimiwa Rais anastahili pongezi, lakini pia katika barabara tumeona ametoa fedha nyingi kwa majimbo yote ambazo ni fedha nyingi kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kama ni kufanya kazi Mheshimiwa Rais Mama yetu Dkt. Samia anajitahidi sana. Pia, amshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuanzisha *dry port* katika Mji wetu wa Tunduma, Mkoa wa Songwe. Tumeona kuna hatua ambazo zinaendelea. Kwa hiyo nisipotumia nafasi hii kumshukuru nitakuwa simtendei haki yeye pamoja na timu yake nzima ambayo wanaratibu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kama *dry port* ikijengwa pale Mpemba tutaongeza wateja wengi wanaotumia bandari yetu ya Dar es Salaam lakini pia barabara zetu hazitaharibika. Pia, ajali zinazotokea katika ukanda huu wa barabara ya *Tanzam* zitapungua sana. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha ujenzi wa barabara nne katika Mji wa Vwawa, Tunduma ambapo mkandarasi yupo na wanaendelea na utaratibu. Kwa hiyo, hili pia natumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais, sitaacha kumshukuru kwa ruzuku aliyoweka kwenye mbolea. Bado tuna-*appreciate* kwamba alitusaidia sisi kama wakulima. Mkoa wa Songwe una wakulima wengi sana. Natumia *forum* hii pia kumwomba kaka yangu Bashe atusaidie kwenye suala la pembejeo za mbegu na viuatilifu pamoja na viua magugu na viua wadudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ilikuwa ni kubwa sana na tuliweza mbegu feki nyingi kiasi kwamba katika mikoa hii ambayo inazalisha mahindi wananchi wengi waliingia hasara. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Bashe aangalie ni namna gani ambavyo atafanya kuhakikisha wananchi mwaka huu hawatumii mbegu ambayo ni feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kusema kwamba Serikali yetu imekuwa ikiendelea kufanya kazi nzuri, tunafurahi, lakini kumekuwepo na maboma mengi ambayo wananchi wanajitolea kufanya kazi; wanafanya wanayajenga yanachukua muda mrefu kumaliziwa. Nawaomba Mawaziri wetu wenye dhamana ya afya, hususan TAMISEMI watusaidie kuhakikisha maboma haya yanaisha. Yamekuwa ni kero na wananchi wanapoteza ile *morale* ya kujitolea kujenga maboma mapya katika maeneo mengine. Kwa hiyo, hilo pia namwomba Mheshimiwa kaka yangu Mchengerwa aweze kuliangalia na kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitakuwa sijajitendea haki nisipozungumza suala la maadili, shule zetu nyingi hazina walimu wanawake. Nimefanya ziara kwenye Kata 30 katika Mkoa wangu, changamoto niliyoikuta ni shule nyingi za msingi na sekondari walimu hawapo. Mfano mzuri niliukuta katika Shule ya Kanga katika Wilaya ya Songwe. Walimu wapo 22 halafu walimu wanawake wapo wawili na ile shule takwimu inaonyesha mabinti ni wengi kuliko watoto wa kiume. Kwa hiyo, kwa hili pia namuomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Kaka yangu Mchengerwa waangalie namna ya kuwa na *distribution* nzuri ya walimu wanawake, kama hawapo basi ufanyike mkakati maalum wa kuajiri walimu wanawake ili waweze kusaidia ku-*maintain* maadili katika shule zetu ambazo zina watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kabla sijachangia mchango wangu namuomba Dada yangu Ummy, Waziri wa Afya, alinipa miezi sita ya Sera ya Lishe na katika mpango huu niliposoma sijaona sehemu inayoeleza suala la lishe. Namuomba anisaidie suala la lishe liweze kukamilika, Sera ya Lishe ni muhimu kwa Taifa hili kwa sababu hali ya utapiamlo katika nchi hii haijakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa narudi katika mchango wangu ambao nilidhamiria siku ya leo, niongelee masuala yanayohusu fedha zinazoletwa katika maeneo yetu. Tunajua Serikali inajitahidi kutenga fedha nyingi na inajitahidi kutoa maelekezo ya fedha nyingi iende kwenye miradi ya maendeleo. Wanatenga hizo fedha na wao wanaleta hizo fedha kwenye maeneo yetu, tunawashukuru sana. Kwa hili kwa kweli Wizara ya Fedha wamekuwa waaminifu kuleta fedha kwenye maeneo yetu. Nampongeza Mheshimiwa Mwigulu kwa hili wanatutendea haki sisi kama Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayokuja kujitokeza katika maeneo yetu ni kwamba kumekuwa na usimamizi duni wa hizi fedha kwenye maeneo yetu. Ninarejea kwenye kipengele cha udhibiti wa matumizi ya fedha katika huu mpango ambao Mheshimiwa Waziri ametupatia. Anasema fedha zote kutumika kwa

wakati, kumekuwa na miradi ambayo inavuka mwaka wa kwanza, mwaka wa pili, mwaka wa tatu tunamuomba Mheshimiwa Waziri na timu yake waangalie namna njema ya kufanya hii miradi isiweze kuvuka muda mrefu na wawe wanaibainisha tuwe tunaiona ili tujue kwamba ni miradi gani imekuwa sugu haitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachokuja kusikitisha ni kutoa fedha sawa katika maeneo tofauti lakini maeneo mengine miradi inaisha na maeneo mengine miradi haiishi. Maeneo mengine wanaongeza fedha nyingi juu yake wakati maeneo mengine unakuta hawajaongeza hata fedha kidogo. Natamani iwe hivi, kwenye kudhibiti fedha zetu hata ongozeko linaloongezeka liwe na uwiano. Haiwezekani uniambie wewe Halmashauri yako *Engineer* alikosea *estimation* kwa kiwango hicho mpaka wewe uwe na ongezeko kubwa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nilivyopita kwenye miradi mbalimbali katika ziara yangu. Unakuta shule inajengwa kunakuwa na ongezeko la zaidi ya shilingi milioni 150, sasa unajiuliza hivi hiyo shilingi milioni 150 ina maana kweli *Engineer* alikosea kwa kiwango hiki? Kwa hiyo na hili namuomba Mheshimiwa Waziri aweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi maalum kwa hawa Wakaguzi wa Ndani *(Internal Auditor),* hawa watu wanahitaji kujengewa uwezo wa kina, kwanza ni wachache. Mimi nashauri katika maeneo yetu, Halmashauri zetu, Wakaguzi wa Ndani waongezeke. Mbali ya hivyo watengewe fedha ya kutosha kuweza kuzunguka kwenye hiyo miradi zaidi wapatiwe vifaa vya usafiri ikiwa ni pamoja na magari ili waweze kufika maeneo hayo ya ukaguzi na kuweza kujua *value for money* ya hela zetu inakuwa ikoje.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nasema hivi, *force account* imekuwa ni kichaka cha uharibifu wa fedha zetu. Miradi mingi iliyotekelezwa kwa *force account* ni dhaifu na fedha nyingi inaharibika.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Costantine Kanyasu jiandae Mheshimiwa Yustina Rahhi ajiandae na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali nzima kwa kazi nzuri ambayo wanaendela kufanya. Namshukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Geita Mjini na wananchi wa Mkoa wa Geita, kama wiki moja au mbili zilizopita tulikuwa na mkutano mkubwa wa wachimbaji Dodoma, ambapo kwa sehemu kubwa wachimbaji walitoka Mkoa wa Geita. Tunashukuru kwa kukabidhi vifaa vya teknolojia ya madini, tunamshukuru sana na wananchi wanasema sasa wameingia kazini rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Mipango pamoja na Waziri wa Fedha kwa taarifa yao nzuri ambayo nimeipitia. Kama ambavyo malengo au shabaha ya mpango wenyewe imezungumza ni kuongeza thamani kwenye mazao tunayouza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuishauri Serikali, tunayo Sheria kwenye madini ambayo imeweka ulazima wa kuongeza thamani madini ya dhahabu kabla ya kuyauza nje. Kwa kufanya hivyo, Serikali ilitoa leseni za kujenga *gold refinery* na zimejengwa *gold refinery* nyingi lakini bado nashangaa ni kwa nini bado kuna kusita sita kwenye kutumia sheria hiyo kuhakikisha kwamba dhahabu yote inayouzwa nje imekuwa *refined*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kuna sababu kubwa ya kulazimisha hivyo? Kwanza; tunapeleka dhahabu nje ambayo tayari

itakuwa *branded* kama dhahabu yetu; Pili, tunaiongezea thamani na pia tunazifanya hizi *refinery* ambazo zimejengwa kwa gharama kubwa kufanya kazi iliyokusudiwa. Kwa hiyo, lengo hapa ni tusimamie hii sheria tuliyoiweka, tuweke malengo ya kuongeza thamani ya madini haya, tuhakikishe kwamba soko tunalolipata huko nje linatambua kwamba dhahabu hii inatoka Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapoondoka Tanzania *raw gold* kwenda nje kama *South Africa* au Uarabuni wanapoifanyia *refinery* wanai-*brand* wao kule kwa hiyo matokeo yake inapoteza uasili lakini sisi tunapoteza thamani yetu kwenye eneo hilo. Naishukuru sana Serikali pia kwa mchakato ambao imetoa ahadi kwamba inauanzisha ambao sasa inajipanga kufanya *high resolution airborne geophysical survey* ambayo itatusaidia kuijua vizuri nchi hii na kuangalia maeneo mahsusi ambayo yana madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi pamoja na mbwembwe zote tulizonazo eneo ambalo limefanyiwa utafiti ni kama asilimia 16. Tukiongeza, tukijielekeza kwenye kukamilisha utafiti kwenye eneo hili makato yanayotokana na madini sehemu kubwa yata-*double* yatakuwa mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali katika maeneo ya wachimbaji kuna vituo vya mfano vimewekwa viko vitatu. Kimoja kiko Rubete, kingine Rwamgasa ambapo wamejenga *CIP*. *CIP* hizi zingejengwa hata 30 au 50 Tanzania ili ziwasaidie wachimbaji wadogo kumaliza dhahabu kwenye mchanga. Sasa hivi teknolojia inayotumika inaacha dhahabu nyingi sana kwenye mchanga kwa sababu wanatumia *plant* na hizo *plant* ni lazima uje urudie kuchukua ule mchanga kuuingiza kwenye *plant*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali kwa kuwa dhahabu inatuingizia fedha nyingi za kigeni na kwa kuwa, tayari tumegundua asilimia 40 ya dhahabu Tanzania inatokana na

wachimbaji wadogo wadogo, isione aibu kuwekeza, tuwekeze ili tuweze kupata pesa nyingi zaidi kutoka kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, mwaka huu pia nilichangia, kwenye mchango wangu nilizungumzia habari ya kuongeza pesa za mauzo ya nje kutoka kwenye mazao. Sasa hivi tunapata pesa nyingi sana kutoka kwenye *avocado* na hii ilikuja yenyewe tukapata pesa nyingi. Tanzania kuna maeneo yanajipambanua kwa kulima migomba, kuna maeneo yanajipambanua kwa kulima nanasi. Nilizungumza duniani kuna *export* ya nanasi inayokadiriwa kufikia dola bilioni 30. Nanasi tulizonazo Tanzania ni kama vile madawa ya kienyeji kwa sababu huwezi kuzi-*export*. Nilisema tukiboresha eneo hili peke yake, Costa Rica wanapata dola bilioni moja kwa kuuza nanasi, Philippines wanapata dola bilioni 300 kwa kuuza nanasi, Nigeria wanapata zaidi ya dola milioni 100 kwa kuuza nanasi. Sisi hatuuzi nanasi lakini wakulima wa nanasi wapo, tunachotakiwa hapa ni kupata mbegu sahihi ambayo tunaweza kuuza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kwa kuwa wakulima wa nanasi wapo na tuna *BBT* inaendelea ni kuwapelekea teknolojia, kuwapelekea mbegu bora na kuwatafutia soko kama tulivyotafuta soko la *avocado* tukaanza kuuza nje tukapata mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine nataka kuzungumzia, kwanza naipongeza Serikali kwa kuonesha itapeleka trilioni 15.3 kwenye maendeleo sawa sawa na asilimia 33 nakupongeza sana. Juzi wakati tunajadili taarifa ya *CAG* ulitokea mjadala wa zaidi ya shilingi trilioni 200 ambazo zimeonekana zimekwenda nje kinyume cha utaratibu. Mawaziri wote wawili wa Fedha na wa Mipango walikuwa wanapinga na mimi nakubaliana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye repoti utakutana na hizo dola bilioni 140 kama pato la nchi lakini kwa mfumo ulivyo duniani Mheshimiwa Waziri wa Mipango ukiangalia kwenye *list financial flows* duniani pesa ambayo inavuja ni nyingi kuliko pesa

inayokusanywa. Pesa tunayoizungumzia hapa ni pesa ambayo haikupita kwenye vitabu vyako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili hii pesa shillingi trilioni 15.3 ambayo ni sawa na asilimia 33 iweze kufanya kazi yake vizuri lazima tujue kwamba *corruption* ime- imejizalisha, wamebadili mbinu. *Corruption* sasa hivi inakuwa *exported*, inakuwa *exported* kutokea kwenye *contract* na kutokea kwenye kazi ambazo watu wanazitengeneza leo

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kumwambia Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mheshimiwa Waziri wa Fedha tuwe na mpango madhubuti wa ku-*deal* na aina mpya ya rushwa ambayo inaweza, pesa zote hizi zisitusaidie kuona tunachokifanya kutokana na ukweli kwamba kuna watu tayari watakuwa wamejiandaa namna ya kuichukua. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Yustina Rahhi, jiandae Mheshimiwa Stella Fiyao na jiandae Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu kipindi kilichopita tulikuwa tunapanga pia vipaumbele na kupitisha bajeti yetu, lakini Mheshimiwa Rais ametoa fedha za utekelezaji wa mpango ambao sasa hivi unaendelea kutekelezwa na ametoa fedha nyingi sana. Nampongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa hivi tukiweka mpango wetu vizuri na vipaumbele vizuri kwa vyovyote vile utapata fedha na utatekelezeka. Pia, nampongeza kwa maono aliyonayo tulikuwa tumetamani sana irejeshwe Wizara ya Mipango na Uwekezaji ambayo sasa amewekeza na tunaomba isimamie rasilimali za Watanzania ziweze kutumika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kupanga ni kuchagua. Tuna mahitaji mengi sana ya wananchi na hasa ukienda vijijini mahitaji ni mengi, kuna barabara ni mbovu zinatakiwa zitengenezwe, kuna vivuko, kuna zahanati na kuna elimu lakini kwa sababu rasilimali hizi ni chache, hizi *resource* ni *scarce,* ni lazima tuwe makini kuona kwamba ni vipaumbele vipi vinatakiwa viingie katika mpango wetu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nampongeza Waziri kwa sababu amekuja na mapendekezo ya mwongozo, kwamba kati ya vipaumbele, kwanza ni kukamilisha miradi mikubwa iliyokuwa inaendela ikiwemo mradi wa reli, wa viwanja vya ndege na hasa huu wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ili tuweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni hitaji kubwa sana katika kuendeleza uchumi wa Tanzania, lakini sasa nchi mara nyingi tunaingia kwenye mgao wa umeme. Hili jambo ni baya sana, umeme unahitajika, kuna vijana kule wana viwanda vyao vidogo vidogo vya kuchomelea na kadhalika, sasa tunavyokata umeme, tunavyoweka mgao kwa kweli ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe tungeweza kuweka kipaumbele kikubwa kwa kuachana na hii changamoto ya upungufu wa umeme, kwa sababu kwanza rasilimali za kuzalisha umeme tunazo, tumebarikiwa na Mungu tunaweza kuzalisha umeme hata kutoka kwenye vyanzo vya jua, akazalisha mtu mmoja

mmoja tukaingiza kwenye gridi ya Taifa. Tunaweza kupata umeme pia kutoka kwenye vyanzo vya upepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaongea kila siku habari ya gesi asilia ambayo pia inaweza ikazalisha umeme. Tunaongea habari ya gesi kule Mchuchuma na Liganga ambapo watafiti wanasema kuna takriban shilingi bilioni mbili *potential* ambazo pia tungeweza kufua umeme kutoka huko wa kati ya *megawatt* 600 mpaka 900 tukaweza kuingiza kwenye gridi ya Taifa, tena kwa gharama ndogo ya shilingi 103 mpaka 108 kwa *unit*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kipaombele changu kingine ni kuwekeza katika viwanda. Tumeona nchi zote zilizofanya vizuri katika uchumi wamewekeza kwenye viwanda na sisi tunasema dhima ya uchumi wetu ni uchumi shindani. Tunawezaje kwenda kwenye uchumi shindani kama hatufikirii habari ya viwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto nyingi kwenye viwanda, tuna viwanda vidogo vidogo vingi ambavyo vinachukua karibu asilimia 98. Kwa mfano, tuna viwanda vidogo vidogo sana 62,400 ambayo ni asilimia 77 ya viwanda vyetu. Tuna viwanda vidogo 17,274 ambayo ni sawa na asilimia 21, tuna viwanda vya kati 684 ambayo ni asillimia 0.8 na tuna viwanda vikubwa 618 ambayo inaenda asilimia 0.76. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vidogo bado vina mahala pake. Tunajua umuhimu wa viwanda, vinaweza vika-*absorb* nguvu kazi kubwa ambayo kila siku inakimbizana na ajira. Vilevile, viwanda hivi vinasaidia, kwa mfano *agro-processing* viwanda, kufanya *value chain* ya mazao yetu na tukapata faida. Changamoto kubwa ya viwanda hivi vidogo vidogo ni mitaji. Serikali iwasogelee hao wenye viwanda vidogo vidogo, pengine ni vikundi vya kina mama, wengine wanafanya usindikaji wapate mitaji, *skills* na *knowledge* pamoja na masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nasema habari ya viwanda hivi vya kati na viwanda vikubwa kuviboresha, kwa mfano viwanda ambavyo mahitaji yake ni makubwa Tanzania. Kwa mfano, kiwanda cha mbolea tuna viwanda viwili tu vya mbolea, kiwanda cha Minjingu pamoja na *Intracom* ambapo inazalisha mbolea kidogo. Minjingu kinazalisha tani 100,000 na hiki kingine kinazalisha tani 250 mpaka tani 300 na mahitaji ya mbolea ni zaidi ya tani 1,000,000. Sasa tunaagiza na kuweka mbolea ruzuku, natamani nguvu zote hizi tungewekeza katika kujenga viwanda vya mbolea ili tuweze kujitosheleza kwa mbolea.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna viwanda vya saruji pamoja na chuma. Nasema Watanzania wamekubali kupata maendeleo na kujenga makazi bora, lakini saruji na chuma bado bei yake imekuwa ni kubwa sana. Naiomba Serikali iweze kuwekeza katika viwanda hivyo ili Watanzania waweze kwenda kwenye makazi bora. Tunajua ni matokeo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupeleka fedha nyingi katika *lower level* ambapo imeongeza mzunguko wa hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule ambapo Mama Lishe, vijana na maduka madogo madogo wameweza kuzungusha hizi hela na kwa ajili hiyo watu wameamua kujenga makazi bora, lakini ukienda saruji inauzwa ghali, chuma inauzwa ghali. Tuna uwezo mkubwa sana wa kuweza kuzalisha saruji yetu wenyewe pamoja na chuma kwa sababu malighafi zote ziko huku. Changamoto ni kusafirisha hizi malighafi kutoka kule kusini, kwa mfano gesi asilia inayotoka kwenye makaa ya mawe, huko chini tunaomba reli ijengwe. Wameongea sana Wabunge wa Songea na wote wa Kusini, kuna umuhimu sana wa kujenga reli. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele ya pili imepigwa, ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Stella na Gulamali karudi. Ataanza Mheshimiwa Gulamali halafu ataingia Sichalwe.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika mpango huu. Kwanza naanza kwa kuzungumzia suala la Bandari Kavu ya Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua hata Serikali inajua umuhimu wa mpaka wa Tunduma hasa kwa kuzingatia kwamba mpaka wa Tunduma ni lango kuu la *SADC*. Mpaka wa Tunduma unapitisha mizigo zaidi ya asilimia 73 inayoshuka katika Bandari ya Tanzania. Mizigo yote hii inapita katika mpaka wa Tunduma ambalo ni lango kuu la *SADC*. Katika michango yetu mbalimbali tumeendelea kuisisitiza Serikali na kuiomba, ione umuhimu mkubwa wa kujenga bandari kavu ndani ya Mji wa Tunduma ili kurahisisha huduma za usafirishaji wa mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu ni kwamba, tangu nimeanza kuusoma Mpango huu, sijaona mahali ambapo Serikali imeweka kipaumbele cha kuhakikisha inajenga bandari kavu katika Mji wa Tunduma ili kurahisisha huduma kwa watu ambao wanatumia mpaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike wazi kabisa kwamba sasa hivi mataifa yapo katika ushindani wa kibiashara ikiwemo Tanzania. Tunaona mataifa mengi ambayo yanaandaa mipango ya kujenga bandari kavu katika mataifa yao. Ni lazima Serikali ione umuhimu wa kujenga bandari kavu katika Mji wa Tunduma hasa ukizingatia kuwa ni lango kuu la *SADC* ili kurahisha huduma na kuendelea kuwashawishi watu ambao wanatumia mpaka huu wa Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua umuhimu wa bandari kavu na sisi sote tunaona namna Halmashauri ilivyolichukua jambo hili kama kipaumbele. Halmashauri ya Mji wa Tunduma imetenga zaidi ya ekari 2,000 kwa ajili ya kujenga bandari kavu ndani ya Mji wa

Tunduma. Tumeomba miundombinu, tumeona reli imepita katika lile eneo, tunaona hospitali kubwa imejengwa katika yale maeneo, tunaona stendi imejengwa katika yale maeneo. Tunaiomba Serikali ione umuhimu wa kujenga bandari kavu ndani ya Mji wa Tunduma ili kuleta ushindani wa kibiashara na mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kuzungumzia suala la kilimo. Nazungumzia upatikanaji wa mitaji katika Sekta ya Kilimo. Mimi ninatokea Mkoa wa Songwe, Mkoa ambao asilimia kubwa ya wananchi wake wanaishi vijijini na ni wakulima wakubwa, na ni wakulima wazuri kabisa ambao wanategemewa na Taifa hili. Tunaona katika pato la Taifa namna kilimo ambavyo kimekuwa na mchango mkubwa, zaidi ya asilimia 26 kilimo kinachangia katika pato la Taifa. Hivyo, kilimo ni kipaumbele kikubwa ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona katika upatikanaji wa mitaji ya sekta ya kilimo kwa mwaka 2022/2023, taarifa inasema zaidi ya shilingi trilioni 2.622 zilitengwa na benki kwa ajili ya shughuli za kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10, lakini katika fedha hii shilingi trilioni 2.622 ambayo ilitengwa na hizo benki, 7% tu ndiyo ilikwenda katika uzalishaji wa mazao, asilimia 93 ilikwenda katika biashara ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatari kwa Taifa letu. Tunaona namna watu ambavyo wamezama kwenye biashara na wamesahau kwenye suala zima la uzalishaji wa mazao ndani ya Taifa letu. Ndiyo maana tunatumia fedha nyingi kuagiza baadhi ya mazao nje kwa kuwa huku ndani tumeshindwa kuwekeza. Tuna wakulima wengi sana ambao wamejitoa kwenye suala zima la kilimo, lakini wengine wanashindwa tu kwa sababu ya mitaji. Tuna ardhi ya kutosha ambayo hata nusu, hata robo bado hatujaifikia, lakini bado tuna changamoto kubwa ya kuagiza baadhi ya vyakula nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali, ione umuhimu wa kuwekeza fedha nyingi ambazo zinatengwa na benki,

ziende kwenye uzalishaji wa mazao na siyo biashara. Ni lazima tuzalishe mazao ya kutosha, ni lazima tuzalishe mazao ya aina mbalimbali ya kutosha ndani ya Taifa letu na ikiwezekana tuuze nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona kuna changamoto. Ukisoma katika taarifa utaona ya kwamba Magereza yetu yanatumia zaidi ya shilingi bilioni 10 kila mwaka kwa ajili ya chakula. Wakati huo tunaona namna ambavyo Magereza yana ardhi kubwa na nzuri ya kutosha ambayo inaweza kutusaidia katika uzalishaji wa mazao. Changamoto kubwa ambayo Magereza wanashindwa ni kukosa mtaji na fedha za kuendeshea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali ione umuhimu wa kuwekeza fedha na kuwakopesha watu wa Magereza ili waweze kuzalisha chakula kingi na ikiwezekana wajiendeshe, wajikwamue kiuchumi na waweze kutusaidia katika suala zima la uzalishaji wa chakula ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumza jambo moja. Kumekuwa kuna changamoto, kwamba wakulima wetu wanatumia muda mwingi kupambana na kuhakikisha wanajikwamua katika suala zima la kiuchumi kupitia kilimo. Nasema wazi, tumeona katika mkoa wetu na maeneo mengine, Serikali imewatangazia wakulima kwamba iko tayari kununua mazao na wakulima bila kusita wamejitoa kwa moyo wote kuiuzia Serikali mazao. Ajabu ni kwamba, *NFRA* Wakala wa Chakula, inaeleweka hiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu ni kwamba, tangu mwezi wa Tisa, wa Nane, wa Kumi, watu wamechukua mazao lakini wakulima hawajalipwa fedha zao, pamoja na Serikali kuchukua haya mazao. Tunaomba, watu wamelipwa wachache na wengine bado hawajalipwa na ukizingatia katika mikoa yetu, tumeingia katika msimu wa kilimo. Huyu mkulima mnamweka kwenye eneo gani? Mimi ninachojua wakulima wanalima mazao wakiwa na malengo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri sana wa Mheshimiwa Mbunge, Serikali ilinunua mazao yenye thamani ya shilingi bilioni 194. Mpaka kufika siku ya jana, Serikali imemaliza madeni yote ambayo ilikuwa inadaiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella, Taarifa rasmi hiyo unaipokea?

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei Taarifa.

**MWENYEKITI:** Aaah!

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa kwa sababu, sisi mwezi huu na mwezi uliopita tayari tumeingia kwenye maandalizi ya kilimo. Mnawaletea wakulima wetu vidonda vya tumbo! Nina uhakika hata Momba huko Isanga hawajalipwa. Labda kama mmelipa jana, ndiyo mtuambie. Kama watu wamepimiwa mazao kutoka mwezi wa Nane wamelipwa jana, hii inakaa sawa? Kwamba hawa wakulima hawana malengo? Hakuna anayefanya kazi bila malengo. Acheni kuwasababishia wakulima umaskini usio na lazima. Ni lazima tuseme ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala zima la barabara. Sisi wote tunajua zaidi ya asilimia 80 mpaka 90 ya mizigo na abiria wanatumia barabara. Hivyo, ni wazi kwamba barabara ina mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa letu na maendeleo ya kijamii. Hata hivyo kumekuwa na changamoto, na ndiyo maana kila Mheshimiwa Mbunge anayesimama hapa, anazungumzia suala la barabara. Barabara imekuwa ni changamoto kwenye nchi yetu. Maeneo mengi barabara zinakufa, zina hali mbaya kabisa. Kuna

maeneo hata barabara za kuunganisha mikoa na mikoa zina hali mbaya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, lakini muda wangu mwingine ulichukuliwa na Mheshimiwa Waziri. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Haya. Mtaambizana nje huko. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Gulamali, jiandae Mheshimiwa Sichalwe na Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii niwe sehemu ya wachangiaji kwenye Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja. Natumia fursa hii kwanza kupongeza juu ya utekelezaji wa Mipango iliyopita na huu ambao tupo nao. Naunga mkono, nasema hongereni sana Wizara kwa Mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumeweza kuona Mipango iliyopita, utekelezaji umeenda siyo vibaya, unaenda vizuri. Mpango huu ambao tupo nao wa Bajeti ya shilingi trilioni 47 na fedha za miradi ya maendeleo, tuna shilingi trilioni 15 ambapo iko ndani ya makubaliano kati ya asilimia 30 mpaka 40, na mpango huu una asilimia 33. Kama fedha zote hizi ambazo tumezitenga za shilingi trilioni 15 tutazitoa na kuzipeleka kwenda kwenye miradi ya maendeleo, tuna hakika Taifa letu litapiga hatua kubwa na kuleta maendeleo chanya kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi kwa Serikali kuhakikisha fedha hizi ambazo tunazitenga kupitia mipango yetu, zitoke ziende kutekeleza. Tukifanya hivyo, Taifa litapiga hatua. Mfano, tumeweza

kuona Mpango huu ambao tunatembea nao, ambao unatekelezwa kupitia Bajeti ambayo tumepitisha mwaka jana 2022/2023, tulitenga fedha nyingi kwenye upande wa kilimo. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, ameleta mabadiliko makubwa sana kwenye Sekta ya Kilimo kwa fedha nyingi ambazo amewekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo zamani miaka miwili nyuma Bajeti ya Kilimo ilikuwa chini ya shilingi bilioni 250. Tumetoka shilingi bilioni 250 kwenye Bajeti ya Kilimo tunazungumzia karibu zaidi ya shilingi trilioni moja. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa nia ya dhati kuhakikisha kwamba anakikomboa kilimo chetu. Tumeona fedha nyingi zimetolewa kwa ajili ya kuboresha, kuchimba mabwawa makubwa na pia kujenga *schemes* za umwagiliaji. Hii inaonesha nia ya dhati ya kumkomboa Mtanzania maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika fedha hizi zinazotolewa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa. Najua Mpango huu ni mwendelezo wa kuhakikisha kwamba tunajenga mabwawa makubwa ya kuhifadhi maji. Tulikuwa tunalalamika miaka ya nyuma maji yanapotea na mvua zinanyesha; tunapata mvua za kutosha lakini hatujawekeza kwenye kuyapokea yale maji na kuyatengenezea mazingira ya kuyalinda kwa ajili ya manufaa ya kilimo, mifugo yetu na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili nawapongeza. Nataka kutoa ushauri kwenye masuala mazima ya uchimbaji mabwawa. Naweza nikatolea mfano Jimboni kwangu Manonga, Wilaya yetu ya Igunga. Tumepata fedha za kuchimba mabwawa, lakini moja ya changamoto ambayo tunaiona, tunaichukua ardhi kubwa, tunachimba mabwawa kwa ajili ya kupata maji, lakini mabwawa haya ni makubwa ambayo yanachukua karibu vijiji vinne au vitano. Sasa wanufaika wa bwawa zima unaweza kukuta ni vijiji viwili, vile vijiji vitatu maana yake wao hawatapata. Kama walikuwa wanalima, maana yake wakitoa lile eneo, hawatalima tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sisi pale Chomachankola tuna Kijiji kinaitwa Bulangamilwa, kutoka Kijiji cha Bulangamilwa mpaka Choma ni kilometa 12. Kijiji hiki ni sehemu ya vijiji vinavyotoa eneo kwa ajili ya bwawa kubwa kwa kilimo cha umwagiliaji. Wanaoenda kunufaika na bwawa hili ni Kijiji cha pili kinachoitwa Choma. Sasa hawa watu wa Bulangamilwa wanaotoa eneo lao ambalo ndilo wanalotumia kwa ajili ya kilimo. Wakishatoa lile eneo, hawana eneo lingine la kulimia. Tafsiri yake ni nini? Hao wananchi wanahitaji tutenge fedha za kuwapa angalau fidia wapate fedha waweze kwenda kutafuta maeneno mengine. Kumchukulia mtu eneo lake bure, haumpi fidia, unapelekea kumkosesha uhuru wake. Unamnyang'anya eneo ambalo alikuwa akipata uchumi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara, tutoe fidia kwa wale wananchi wa Kijiji cha Bulangamilwa na vijiji jirani Kwanzega, kwa maana ukichukua ardhi yake hatapata sehemu nyingine ya kupata uchumi. Naiomba sana Wizara. Unaponiambia kwamba utampa mashamba eneo la pili, hujaweka mpango wa kwenda kumnunulia na hujui unaenda kuchukua eneo la nani? Kwa sababu yale maeneo ya vijiji vingine yana watu ambao wanayamiliki. Fidia yenyewe haifiki hata shilingi milioni 200 au 300. Unaenda kuweka mradi wa bwawa la zaidi ya shilingi bilioni tano, lazima Serikali iweke fedha za kumfidia huyu ambaye anachukuliwa eneo lake ambaye hana tena sehemu nyingine ya kwenda kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na watu wa Mipango kuhakikisha kwamba watu wa Bulangamilwa wanaangaliwa. Mheshimiwa Waziri Bashe, kule Nzega ambako ni Nzega Vijijini, wananchi wanalia kwa sababu maeneo yao yanachukuliwa, na wewe ndiye mwenye eneo lile. Naomba sana mwangalie jinsi gani ya kuwasaidia hawa wananchi. Kwa sababu kuna wananchi wana makaburi ya wazazi wao wanatakiwa walipwe fidia. Kuna watu wana nyumba zao zinabolewa, wanatakiwa walipwe fidia, kuna watu wana majaruba ambao ndiyo uchumi wao, unapochukua na kuchimba bwawa inatakiwa

umpe fidia ili anapoenda akatafute sehemu nyingine kuliko kumwambia sasa atanufaika na bwawa wakati hana eneo lingine kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia Mheshimiwa Waziri, unapochukua lile eneo, tulipe fidia katika yale baadhi ya maeneo kwa sababu siyo fedha nyingi. Pia hawa watu wana uchumi. Kwa hiyo, tusiwafanye wananchi wetu wakawa maskini. Hatuwezi tukawaambia wananchi wetu sasa wahamie kwingine. Watapata fursa ya mabwawa, ndiyo, lakini hana ardhi ya kulima, analima wapi? Ardhi nyingine inayobakia ni dhahabu. Hawezi kwenda kuchimba dhahabu kwa sababu maisha yake ni kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Wizara, hawa watu mkichukua maeneo yao mwangalie namna bora ya kulipa fidia. Haiwezekani mumchukulie mtu eneo lake, umwambie utanufaika na hili bwawa, utaogelea humu, utavua samaki humu. Sasa kuvua samaki, ndiyo atavua, kama ataendelea kupata eneo lingine ambalo litamsaidia kuweza kufanya kilimo akapate chakula. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, mwangalie katika suala zima la haya mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mfano wa Choma lakini naamini ni nchi nzima tunafanya hivyo. Kwa wale ambao watanufaika na lile eneo la kupata maji, hiyo haina shida, watapata maji, yatakayoingia kwenye majaruba yao. Kwa wale ambao hawatanufaika na yale maji maana yake wapewe fidia ili wahame katika yale maeneo waende maeneo mengine waweze kuanza maisha mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo tutawatia watu wetu umaskini na hali ambayo italeta mgogoro mkubwa kati ya wananchi na Serikali yao. Nawaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo hili suala alichukue…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kengele ya pili.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Mpango, uko vizuri, lakini mwangalie jinsi gani ya kuboresha katika malipo ya fidia kwa watu mliochukua maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye huu Mpango wa Serikali wa Mwaka mmoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sichalwe, jiandae Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwanza naanza kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza mambo ambayo tuliyapendekeza kwenye Mpango uliopita. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwasilisha Mpango wao nasi tuweze kuongeza mawazo yetu waone kama vile yanafaa kwa ajili ya kusaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea katika maeneno mawili. Chanzo cha mapato, ni namna gani ambavyo tunaweza tukatumia mawazo haya yakatusaida kama Taifa kwa ajili ya kuongeza mapato. Jambo la kwanza, najaribu kuangalia yale maeneo ambayo kutoka kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi hususani kwenye upande wa vijana, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inasema: "kutengeneza ajira zisizopungua milioni nane katika Sekta Rasmi na isiyokuwa rasmi kwa vijana." Chanzo kimoja ambacho nitaongelea ndani ya nchi yetu ni pamoja na huduma za forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Huduma nyingi za kiforodha mfano Tunduma, Namanga, Holili, Kasumulu na maeneo mengine ambapo kuna Vituo vya Forodha, kumeonesha kuvutia sana

wananchi wengi kwenda kufanya biashara maeneo hayo. Namwomba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwamba 2021 ulikuja pale, ukatembelea kwenye lile eneo, tunaomba tupate Kituo cha Forodha. Licha tu ya kwamba itasaidia wana-Momba lakini vituo vingi vya Forodha vimeonekana kuwa chachu ya mapato kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tu mfano wa Tunduma, angalia mapato ambayo yanapatikana pale. Pia kwenye hivi vituo vya Forodha, licha tu ya kupata mapato, hata katika hali ya ulinzi, tunaongeza ulinzi kwenye nchi yetu kwa sababu tunakuwa tunaendelea kuikagua vizuri ile mipaka na kuzuia hata mambo ya magendo. Nakuomba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, uone tena, ukae na timu yako ya *TRA* mpitie lile eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea hapo hapo kwenye Kituo cha Forodha Tunduma, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Hivi mnaonaje kwenda kuyapunguza yale magari yote ambayo yamejaza msongamano pale Tunduma na kusababisha *jam* zisizokuwa za lazima? Kwa nini baadhi ya magari yasivutwe kwenda mpaka kule kwa Kakozi? Si ni matumizi mabaya ya barabara? Barabara iko wazi tu, nyeupe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa tunasubiri huo mfumo wa njia nne, basi tunaweza tukayavuta yale magari tukapunguza *jam* Tunduma ili watu wakaendelea kuvusha magari yao vizuri bila kuathiri shughuli nyingine. Mji mdogo lakini unaweza ukatumia zaidi ya nusu saa kwa ajili ya kupita kilometa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuongelea chanzo cha mapato ambacho kinaweza kikasaidia vijana, ni kwenye eneo la teknolojia. Wakati nasoma hotuba ya Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, kwenye ukarasa wake wa 51 pamoja na ukurasa wa 117 kwenye kipengele cha 3.3.2.2.1, nikajaribu kuangalia namna ambavyo yeye ameielezea teknolojia. Katika ulimwengu tulionao, matajiri duniani, kwa mfano nikiongelea

nchi ya USA wana mabilionea 735. China wana mabilionea 607 na nchi nyingine huko duniani. Hata hivyo, matajiri wengi hawa wanatokana na utajiri ambao unatokana na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili nimeandaa andiko fupi kwa kuangalia mwaka 2021 ambao toka nimeanza kuchangia mambo ya teknolojia mwaka 2022, naomba Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo apate pamoja na wewe mwenyewe upitie uone. Nimekuja na orodha ya matajiri duniani kama kumi hivi ambapo utaona utajiri wao wote mabilionea hawa unatokana na mambo ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwasome kidogo. Tajiri wa kwanza duniani mwaka huu wa 2023 ni Elon Musk ambaye ana utajiri wa dola za Kimarekani bilioni 240 ambao unatokana na kufanya biashara za teknolojia. Ana Kampuni ya *SpaceX* pamoja na *Tesla*. Tajiri wa pili ni Bernard Arnault lakini yeye anafanya mambo ya *fashion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tajiri wa tatu ni, Jeff Bezos ambaye yeye utajiri wake ni dola za kimarekani bilioni 154, ambaye ndiye mmiliki wa Taasisi ya Amazon, anafanya biashara za mtandaoni, tajiri wa nne ni Larry Ellison ambaye utajiri wake ni dola za kimarekani bilioni 146 naye ni mmiliki wa Kampuni ya *Oracle Cooperation* ni mambo ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tajiri wa tano kwa mwaka huu wa 2023 …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sichalwe pamoja na kuwajua hao matajiri, ungelisaidia Bunge utajiri wao walioupata kwenye teknolojia na walitumia mbinu zipi ili *work the talks* ambapo sasa hao matajiri hawasaidii kitu kama huelezi wamefanya nini ili Waziri aweze kuelewa, sawa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Halafu sasa hao matajiri waache, tutaambizana baadaye jioni.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nataka kusema nini hapa; orodha ya matajiri wote ambao tunawaona duniani hawa wote wametokana na kuwekeza kwenye teknolojia. Kwenye teknolojia ipi? Mapinduzi manne viwanda *(forth industrial revolution)* kwenye mambo ya *blockchain technology*, kwenye mambo ya *digital currencies* na kwenye mambo ya *artificial intelligence*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya Serikali yetu kutafuta mazingira mazuri na wezeshi ya kuruhusu vijana wa kitanzania kuonesha uwezo wao wa kiteknolojia ili na wao tuweze kupata matajiri wengi kama hawa duniani. Miundombinu yetu mingi iliyopo hapa Tanzania, hai-*support* vijana wengi kwenye kujielekeza katika teknolojia. Pia hakuna mazingira wezeshi ambayo Serikali imewawekea vijana ili waweze kuonesha uwezo wao na ubunifu wao ili tuweze kupata akina Elon Musk wengi kama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia watu wote hawa pamoja na kunikataza ndio hivyo hivyo. Mtu kama Mark Zuckerberg pamoja na mawazo yake ya ubunifu lakini unaona kabisa Serikali yao imewatengenezea mazingira ambayo wana-*support* ubunifu. Yeye ndie ambaye ndio mmiliki wa Mtandao wa *Facebook, Instagram, WhatsApp*, angalia mazingira gani ambayo wanapata, angalia ni mapokeo gani ambayo Serikali ina-*support* teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 tulipochangia sana kwenye mambo ya *blockchain technology* Mheshimiwa Rais ameshawahi kutoka hadharani na kuonesha ni namna gani ambavyo wataalam wanapaswa ku-*support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi kutaka kujua kwa nini nchi yetu wakati mwingine, inatukwamisha kwenye ku-*support* mambo ya teknolojia, angalia mpaka sasa hivi tulishachangia sana

hapa bungeni kuhusiana na kuruhusu Mfumo *PayPal* ili tuweze kulipa malipo ya *PayPal* kwenda nje ya nchi, lakini unaweza kukuta watanzania wengi ambao wanafanya biashara ili waweze kulipa kwa njia ya *PayPal* wao wanaruhusiwa kulipa lakini wao hawaruhisiwi kulipwa. Kwa mazingira kama hayo yanaonesha dhahiri kabisa kwamba nchi yetu bado haijatu-*support* hususan vijana kwenye mambo ya teknolojia. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mazigira wezeshi ya ku- *support* teknolojia yawezeshwe ili tuweze kupata matajiri wengi kama hawa duniani, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa hayo ndio ilitakiwa uyaseme, sio kutaja majina ya matajiri.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni kuwa-*motivate* Mawaziri pamoja na wewe mwenyewe.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa naongeza muda mpaka tutakapomaliza wachangiaji wote leo, kwa Mamlaka ya Kiti, muda tunaongeza mpaka tutakapomaliza wachangiaji wetu, Mheshimiwa Daktari Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi natumia nafasi hii kukushukuru wewe, lakini kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika Taifa letu la Tanzania lakini katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwashukuru hawa ndugu zangu wawili, Profesa Kitila na Daktari Mwigulu kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya ya kumsaidia Rais katika hizo Wizara mbili nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nina mambo machache sana na nitaanza na Profesa Kitila. Kwa Profesa Kitila nimekuwa nikitafakari ni jinsi gani tunaandaa hii miradi yetu mbalimbali kila mwaka kupitia, mpango wa maendeleo wa kila mwaka ambao tumeuvunja kwenye ule mpango wa maendeleo wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza huwa natafakari unakuta kwenye kijiji kimoja tumepeleka miradi mitatu, Mradi wa Maji, Mradi wa Umeme, Mradi wa Barabara lakini ukiangalia hii miradi yote haisomani, kwa lugha nyingine hakuna *convergency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningemshauri Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila, katika eneo ambalo Wizara ya Mipango inahitaji kutusaidia ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na *convergency invent*. Kwamba tunapoenda kwenye kijiji kimoja Mheshimiwa Rais amepeleka Mradi wa Maji, Mradi wa Umeme, Mradi wa Afya nini *interpretation* ya wananchi wa pale *in terms of invent,* hilo ni eneo la kwanza ningeliomba Mheshimiwa Waziri ulifanyie kazi. Tunahitaji kuja na *framework* ambayo ita-*tap* hizo *convergency intervention* zote tuone ni jinsi gani wananchi wapo *satisfied* na ile miradi yote iliyoenda katika eneo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la agenda ya vijana *(youth agenda)*. Tumeshafanya mambo mengi sana, Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa kwenye huduma za jamii, ninategemea sasa na ni matarajio yangu na ni matumaini yangu kuona huu mpango sasa una-*move* kutoka kwenye huduma za jamii kwenda kwenye agenda ya kuwaendeleza vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, agenda ya vijana ni *global agenda* na hasa hasa kwenye masuala ya kuwajenga kiuchumi. Kuna maeneo mawili nchi za wenzetu wamefanya na hasa hasa vijana ambao wapo *out of the school.* Tuna kundi kubwa la vijana waliomaliza shule ya msingi hawakufanikiwa kuendelea sekondari, waliomaliza sekondari hawakufanikiwa kuendelea vyuoni wapo mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mambo mawili, la kwanza tunahitaji sasa kuja na *comprehensive program* kwenye masuala ya elimu ujuzi. Katika hili eneo Ofisi ya Waziri Mkuu imefanya, lakini bado kuna changamoto. Changamoto ya kwanza tunawachukua vijana kutoka vijijini wanaenda kusoma Singida Mjini, kuna wengine wanashindwa kule kwa sababu ya gharama. Kwa nini tusianzishe *program* kama hizo za kuwajngenea ujuzi katika maeneo yao, kwenye zile *locality* zao, kwenye kata, kwenye tarafa ili kuwapunguzia huo mzigo wa wenyewe kusafiri kwenda kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo ambalo tunaweza tukalifanya vizuri sana na tukaja na mradi mkubwa wa kuwasaidia vijana wa kitanzania hasa wale waliomaliza shule ya msingi, waliomaliza sekondari hawakufanikiwa kwenda kwenye vyuo vya juu, ni kuwajengea ujuzi kwa kupitia mafunzo ya muda mfupi, miezi miwili, miezi mitatu, wakitoka pale tunaweza tukawa-*link* kwenye viwanda mbalimbali ambavyo vipo hapa. Hili ni eneo ambalo ni muhimu sana linaweza likatusaidia sana kwenda na hii agenda ya vijana ili tuweze kuwasaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni eneo la mradi wa *BBT* wa Bashe. Mheshimiwa Bashe *idea* yako ya *BBT it is a very brilliant idea,* lakini Mheshimiwa Bashe usipokuwa makini na hii *idea you will fail.* Naomba nikushauri kitu kimoja, hii *idea* ni *brilliant* sana kwa sababu kwanza una-*address youth agenda* lakini kuna tatizo moja la *selection bias.* Umewahamisha vijana kutoka Manyoni umewapeleka Morogoro *that is not sustainable. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri tu-*focus* kwenye maeneo yao tujikite kwenye ile *local economic development.* Kama aneo ni *potential* kwa kilimo wakusanye wale vijana wanaotoka kwenye lile eneo *BBT* ifanye kazi kwenye lile eneo, lakini kuwatoa Manyoni kuwaleta Dodoma, kuwatoa Manyoni unawapeleka Morogoro kimsingi haitakuwa endelevu. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo mimi ningekushauri kwamba Serikali iweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ushauri kwa ndugu yangu Daktari Mwigulu kwenye suala la bajeti, tuna miradi mingi ambayo umeitaja pale Serikali inaenda kuitekeleza lakini kwa upande wa Manyoni mimi ningeshauri jambo moja. Tuna miradi ambayo imetajwa sana kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa mfano Daraja la Sanza, kila mwaka Daraja la Sanza kila awamu Daraja la Sanza huwa linatajwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Rais safari hiii, ameruhusu angalau mkandarasi ameshapatikana sasa tunaomba Daraja la Sanza liende likaanze kujengwa. Kuna Daraja la Ngonjigo chini ya *TARURA* vilevile kuna Bwawa la Mbwasa Mheshimiwa Bashe, hili bwawa kwenye kila Ilani ya CCM lipo. Nakushukuru na wewe mwaka huu naona umeshaliweka sasa nategemea kwamba kwenye bajeti hii sasa litaenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kuna huu Mradi wako wa Mwalala, kituo cha pamoja cha ukaguzi wa magari. Huu mradi ni wa zaidi ya bilioni 30 ulisimama tangu 2016 ulishafikia asilimia 60 mmetumia zaidi ya bilioni tano imeshakuwa pori pale. Nikuombe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu zile ni fedha za watanzania twende tukauokoe huu mradi wananchi wanalalamika kwa nini mradi ulisimama tangu 2016 na mradi una tija naomba sana huu mradi safari hii kwenye bajeti hii, twende tukau-*revival* uanze kufanya kazi kwa sababu ni mojawapo ya miradi ambayo ina tija sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nirudie kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, lakini niwashukuru hawa Mawaziri wawili Profesa Kitila na Daktari Mwigullu kwa kazi kubwa mnayoifanya. Baada ya kusema haya naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR - KATIBU MEZANI:**

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.49 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 10 Novemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*